BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. | Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. | Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. | Mhe. | Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 5. | Mhe. | Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 6. | Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 7. | Mhe. | Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 8. | Mhe. | Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |
| 9. | Mhe. | Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais |
| 10. | Mhe. | Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 11. | Mhe. | Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki |
| 12. | Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 13. | Mhe. | Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais |
| 14. | Mhe. | Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 15. | Mhe. | Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **16.** | **Mhe. Hamad Rashid Mohamed** | **-** | **MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais** |
| **17.** | **Mhe. Maudline Cyrus Castico** | **-** | **MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais** |
| **18.** | **Mhe. Salama Aboud Talib** | **-** | **MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake** |
| **19.** | **Mhe. Sira Ubwa Mamboya** | **-** | **MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais** |
| **20.** | **Mhe. Juma Ali Khatib** | **-** | **MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais** |
| **21.** | **Mhe. Said Soud Said** | **-** | **MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais** |
| **22.** | **Mhe. Khamis Juma Mwalim** | **-** | **Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe** |
| **23.** | **Mhe. Mihayo Juma N'hunga** | **-** | **Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera** |
| **24.** | **Mhe. Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni** |
| **25.** | **Mhe. Harusi Said Suleiman** | **-** | **Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete** |
| **26.** | **Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri** | **-** | **Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani** |
| **27.** | **Mhe. Mohamed Ahmada Salum** | **-** | **Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi** |
| **28.** | **Mhe. Chum Kombo Khamis** | **-** | **Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake** |
| **29.** | **Mhe. Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake** |
| **30.** | **Mhe. Lulu Msham Abdalla** | **-** | **Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake** |
| **31.** | **Mhe. Juma Makungu Juma** | **-** | **Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini** |
| **32.** | **Mhe. Hassan Khamis Hafidh** | **-** | **Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo** |
| **33.** | **Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi** | **-** | **Naibu Waziri wa Kilimo,** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | | **Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo** |
| **34.** | **Mhe.** | **Abdalla Ali Kombo** | **-** | **Jimbo la Mwanakwerekwe** |
| **35.** | **Mhe.** | **Ali Khamis Bakar** | **-** | **Jimbo la Tumbe** |
| **36.** | **Mhe.** | **Ali Salum Haji** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **37.** | **Mhe.** | **Ali Suleiman Ali (Shihata)** | **-** | **Jimbo la Kijitoupele** |
| **38.** | **Mhe.** | **Ahmada Yahya Abdulwakil** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **39.** | **Mhe.** | **Ame Haji Ali** | **-** | **Jimbo la Nungwi** |
| **40.** | **Mhe.** | **Amina Iddi Mabrouk** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **41.** | **Mhe.** | **Asha Abdalla Mussa** | **-** | **Jimbo la Kiwengwa** |
| **42.** | **Mhe.** | **Bahati Khamis Kombo** | **-** | **Jimbo la Chambani** |
| **43.** | **Mhe.** | **Bihindi Hamad Khamis** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **44.** | **Mhe.** | **Hamad Abdalla Rashid** | **-** | **Jimbo la Wawi** |
| **45.** | **Mhe.** | **Hamida Abdalla Issa** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **46.** | **Mhe.** | **Hamza Hassan Juma** | **-** | **Jimbo la Shaurimoyo** |
| **47.** | **Mhe.** | **Hidaya Ali Makame** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **48.** | **Mhe.** | **Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)** | **-** | **Jimbo la Mtoni** |
| **49.** | **Mhe.** | **Jaku Hashim Ayoub** | **-** | **Jimbo la Paje** |
| **50.** | **Mhe.** | **Khadija Omar Kibano** | **-** | **Jimbo la Mtambwe** |
| **51.** | **Mhe.** | **Machano Othman Said** | **-** | **Jimbo la Mfenesini** |
| **52.** | **Mhe.** | **Makame Said Juma** | **-** | **Jimbo la Kojani** |
| **53.** | **Mhe.** | **Maryam Thani Juma** | **-** | **Jimbo la Gando** |
| **54.** | **Mhe.** | **Masoud Abrahman Masoud** | **-** | **Jimbo la Bububu** |
| **55.** | **Mhe.** | **Miraji Khamis Mussa** | **-** | **Jimbo la Chumbuni** |
| **56.** | **Mhe.** | **Moh'd Mgaza Jecha** | **-** | **Jimbo la Mtambile** |
| **57.** | **Mhe.** | **Mohamed Said Mohamed** | **-** | **Jimbo la Mpendae** |
| **58.** | **Mhe.** | **Mohammedraza Hassanaali Mohamedali** | **-** | **Jimbo la Uzini** |
| **59.** | **Mhe.** | **Mtumwa Peya Yussuf** | **-** | **Jimbo la Bumbwini** |
| **60.** | **Mhe.** | **Mtumwa Suleiman Makame** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **61.** | **Mhe.** | **Mussa Ali Mussa** | **-** | **Jimbo la Ole** |
| **62.** | **Mhe.** | **Mussa Foum Mussa** | **-** | **Jimbo la Kiwani** |
| **63.** | **Mhe.** | **Mwanaidi Kassim Mussa** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **64.** | **Mhe.** | **Mwantatu Mbaraka Khamis** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **65.** | **Mhe.** | **Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini** | **-** | **Jimbo la Dimani** |
| **66.** | **Mhe.** | **Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy** | **-** | **Jimbo la Chaani** |
| **67.** | **Mhe.** | **Nassor Salim Ali** | **-** | **Jimbo la Kikwajuni** |
| **68.** | **Mhe.** | **Omar Seif Abeid** | **-** | **Jimbo la Konde** |
| **69.** | **Mhe.** | **Panya Ali Abdalla** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **70.** | **Mhe.** | **Rashid Makame Shamsi** | **-** | **Jimbo la Magomeni** |
| **71.** | **Mhe.** | **Saada Ramadhan Mwendwa** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **72.** | **Mhe.** | **Said Omar Said** | **-** | **Jimbo la Wingwi** |
| **73.** | **Mhe.** | **Said Hassan Said** | **-** | **Mwanasheria Mkuu** |
| **74.** | **Mhe.** | **Salha Mohamed Mwinjuma** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **75.** | **Mhe.** | **Salma Mussa Bilal** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **76.** | **Mhe.** | **Shaib Said Ali** | **-** | **Jimbo la Chonga** |
| **77.** | **Mhe.** | **Simai Mohammed Said** | **-** | **Jimbo la Tunguu** |
| **78.** | **Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **79.** | **Mhe.** | **Suleiman Sarahan Said** | **-** | **Jimbo la Chakechake** |
| **80.** | **Mhe.** | **Tatu Mohamed Ussi** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **81.** | **Mhe.** | **Ussi Yahya Haji** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **82.** | **Mhe.** | **Viwe Khamis Abdalla** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **83.** | **Mhe.** | **Wanu Hafidh Ameir** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **84.** | **Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **85.** | **Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **86.** | **Mhe.** | **Zulfa Mmaka Omar** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| | | | | |
| | **Ndg.** | **Raya Issa Msellem** | **-** | **Katibu** |

**Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 27 Juni, 2018**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Shilingi Trilioni Moja Bilioni Mia Tatu na Kumi na Tano Milioni Mia Moja Kumi na Nne na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha uonaishia tarehe Thalathini Juni, mwaka 2019 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na Mambo mengine yanayohusiana na Hayo.

**Mhe. Spika:** Ahsante endelea.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati Mezani Mswada wa Sheria za Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto nae aweke Hati Mezani.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, naomba kutowa Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto katika kilele cha maadhimisho ya Ripoti ya Mtoto wa Afrika mwaka 2018.

**Mhe. Spika: U**naweka mezani Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, hutoi taarifa unaweka mezani.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:** Naomba kuweka Hati Mezani ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kuhusu taarifa ya Utekelezaji ya Haki za Watoto katika kilele cha Maadhimisho ya Ripoti ya Mtoto wa Afrika 2018. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili nae aje aweke taarifa mezani.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed (Mhe. Mwenyekiti Kamati ya Bajeti):** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Mswada wa Sheria za Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi

Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, naomba sasa pia nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo Wanawake na Habari ili nae aje aweke Hati Mezani.

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo Wanawake na Habari):** Mhe. Spika, kwa heshima kabisa naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii juu ya Taarifa ya utekelezaji wa Haki za Watoto katika kilele cha Maadhimilisho ya Ripoti ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2018. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 274

### Kero ya Kumbi za Starehe Usiku

**Mhe. Mohamed Said Mohamed (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) -** Aliuliza:

Katika kipindi cha hivi karibuni Serikali imeonekana kukaza kamba na kudhibiti kero za kumbi za starehe hasa baa na muziki nyakati za usiku. Hata hivyo, hali hiyo hivi sasa inaonekana kujirejea hasa maeneo ya shamba zenye shughuli za utalii karibu na makaazi ya watu, maeneo ya mjini n.k hali ni mbaya zaidi.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwa na operesheni maalumu ya kila baada ya miezi mitatu kuhakikisha kuwa kumbi za starehe hazileti bughdha kwa wananchi.

(b) Je, kwanini Serikali imepunguza kudhibiti kero hizo wakati mwanzo imeanza vizuri.

(c) Hatua gani kali sasa zitachukuliwa kwa zile kumbi za starehe zinazopiga muziki kwa sauti ya juu na kuleta kero kwa wananchi na wanafanya hivyo hata wakikatazwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ** – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 274 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba kumjuulisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba kwenye suala la kudhibiti kero zinazotokana na kumbi za starehe hasa nyakati za usiku bado Serikali haijalala wala kupunguza nguvu ya kulishughulikia jambo hili. Serikali inaendelea na utaratibu wake wa kukabiliana na vitendo vyovyote vile vinavyoashiria kuleta kero kwa wananchi kwa kisingizio cha starehe za mtu binafsi. Pamoja na hatua zote hizi, nakubaliana na ushauri wa Mhe. Mwakilishi kwamba katika kuhakikisha kumbi za

starehe hazileti bughudha kwa wananchi, Ofisi yangu haitasita kufanya operesheni maalum kwa kadri hali itakavyojitokeza.

(b) Kama nilivyojibu katika kifungu cha (a) Serikali kamwe haijapunguza kudhibiti kero zinazotokana na kumbi za starehe. Hatua mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na baadhi ya wakati hatua nyengine huchukuliwa kimya kimya ili kufanikisha zoezi husika.

(c) Kitendo cha mtu au watu kufanya jambo lolote litakalosababisha bughudha na kero kwa wengine kikiwemo hiki cha kumbi za starehe kupiga muziki kwa sauti kubwa ni kosa kisheria. Mtu yeyote au kikundi cha watu kitakachofanya kosa hilo na kuthibitishwa na Mahakama atahukumiwa kwa mujibu wa kifungu cha 83 cha Sheria Namba 7 ya 2014. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Spika, nikushukuru sana pamoja na majibu mazuri ya serikali ningeomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi amekuwa na tabia ya kuweza kuingia katika saa sita kwenye kumbi za starehe na kupiga marufuku na kwa kuwa sheria hiyo ipo. Je, serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi juu ya udhibiti wa sheria hiyo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:** Mhe. Spika, kama nimemfahamu vizuri Mhe. Mohamed Said Mohamed naomba nitoe majibu ya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ukweli ni kwamba Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi miongoni mwa majukumu yake ni kuhakikisha kwamba ni msimamizi wa shughuli zote zinazoendelea katika Mkoa wake zikiwemo za Kiserikali na zile za watu binafsi, lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha moja katika jukumu lake jengine ni kuhakikisha kwamba Mkoa katika wakati wote unakuweko katika hali ya ulinzi na usalama au amani na utulivu iwe inakuwepo muda wote katika Mkoa wake.

Hivyo basi wakati mwengine kwa kuwa baadhi ya wakati hupelekewa taarifa mbali mbali ambazo pengine anahitaji kuzithibisha kwamba kuona zina ukweli kwa namna ipi. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba si vibaya kwa kuwa mtu mwenye jukumu anapaswa kufuatilia kuweza kujua kwa uhakika lile ambalo linasemwa au ambalo limejitokeza. Hivyo Mhe. Mkuu wa Mkoa pamoja na sheria hii iliyokuwepo itaendelea kutumika lakini vile vile naye pale ambapo kunakuwa kuna haja ya kufuatilia mambo kama hayo basi vile vile naomba Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kwamba tumuwache Mhe. Mkuu wa Mkoa aendelee kufanya kazi yake kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo katika nchi hii. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Ali Suleiman Ali swali la nyongeza, aah! kuna majibu ya zaida kutoka kwa serikali kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi**: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri na sahihi kabisa aliyotoa Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri, napenda tu

kuongeza jibu la ziada kutokana na swali alililojibiwa kuwa serikali bado inaendelea kutoa taaluma kwa sababu suala ni kuwapa wananchi taaluma. Kwa hivyo serikali kupitia taasisi zake zinazohusika na masuala haya yote ya starehe ikiwemo Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo zote zinaendelea kutoa taaluma kwa mujibu wa sheria na kanuni zake zilivyo.

Lakini vile vile kwa sababu Mkuu wa Mkoa ndiye aliyepewa dhamana ya usimamizi wa sheria ile ya mambo ya vileo. Kwa hivyo anapofika pale ni wajibu wake kuhakikisha kwamba kama yeye ni Mkuu wa Ulinzi na Usalama katika Mkoa wake analinda amani, utulivu na hali ya vitendo ambavyo havikubaliki ndani ya nchi yetu, ni wazi kwamba kuna vitendo zaidi ya hivi vinavyofanyika katika kumbi za starehe na ndio mana Mkuu wa Mkoa anatekeleza wajibu wake katika kuhakikisha kwamba serikali inatimiza sheria zake na kanuni zake ilizoweka. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, tunaamini katika nchi zozote duniani zinakuwa na utaratibu wake unaojipangia katika sherehe za harusi au nyumba za starehe lakini katika jibu tulilojibiwa hapa kwamba utaratibu huu naamini unakiukwa. Je, kuna malalamiko kwa wananchi juu ya muda wa kufunga na kufungua kumbi za starehe. Ni muda gani hasa unaokubalika.

(b) Nani ana wajibu wa kutoa kibali kati ya Baraza la Sanaa na Sheha sababu kuna mkanganyiko kwa wananchi kujua hili kibali akachukuwe kiwe cha usalama kwa nyakati zote anazofanya shughuli zake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kumekuweko na manung'uniko na malalamiko baadhi ya wananchi kuhusiana kwamba kunakuwa na mkanganyiko baina ya kujua kwamba ni wakati gani na utaratibu gani ambao unaotumika kwa sasa wa kuendesha hizi shughuli za baa pamoja na kumbi hizi za starehe.

   Mhe. Spika, ni kweli kwamba kwa sasa katika siku ambazo ni siku za *week end* ni kuwa muda wa kufungua *bar* au sehemu za kumbi hizo kwa utaratibu wa sasa ni kwamba ni kuanzia asubuhi mpaka saa 6 za usiku, lakini vile vile katika siku ambazo ni siku za kazi basi ruhusa hii inatumika kuanzia saa 10 za jioni mpaka saa 6 za usiku. Lakini jambo hili ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara hawa wanakuwa wanaongeza muda na ndio mana pale unaposikia kwamba kunakuwa na malalamiko na manung'uniko yanatokea yanaanzia katika mazingira kama haya. Kwa hivyo Ofisi ndio inalazimika kuchukuwa hatuwa kwa wale ambao wamezidisha muda ambao umewekwa kisheria na si lengo kuwakomoa wafanyabiashara hawa na badala yake ni lile lile lengo la kudhibiti kuona amani na utulivu na katika vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa amani havitokezei katika maeneo haya.

b) Lakini vile vile Mhe. Spika, katika suala la nani kwamba anapaswa kutoa vibali. Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba Baraza la Sanaa lina wajibu mkubwa wao wa kutoa leseni, lakini vile vile na kuvisajili vile vikundi ambavyo vimekuwa vikijishughulisha ama na upigaji wa muziki na mambo mengine yanayofanana na hayo. Lakini vile vile na kutoza kodi kwa mujibu wa sheria zilizokuwepo. Lakini kwa upande wa Masheha wetu wamekuwa wao na utaratibu katika hili ni kuhakikisha kwamba wao wanatoa vibali ni wapi mziki ule unaweza ukapigwa kwa utaratibu upi katika maeneo ya Shehia zao. Hivyo niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika, kwa kupitia Baraza lako Tukufu Waheshimiwa Wajumbe watusaidie katka kutoa taaluma ili wananchi wetu waweze kufuata utaratibu huu bila ya kuepusha bughudha ambazo na manung'uniko hayo ambayo Mhe. Ali Suleiman Ali ameweza kuyaelezea.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa **s**wali limechukua muda mwingi twende kwenye swali la pili kwenye Wizara hiyo hiyo, swali linaulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na kwa niaba yake namuona Mhe. Ali Suleiman Ali.

**Nam. 275**

**Ongezeko la Nyumba za Ulevi Mjini Magharibi**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny Mhe. Jaku Hashim Ayoub)** – Aliuliza:

Mkoa wa Mjini/Magharibi umekuwa ndiyo kama Mji Mkuu wa Zanzibar ambao shughuli nyingi za kimaisha zinafanyika hapo. Hata hivyo, kadiri miaka inavyokwenda kumekuwa na ongezeko la nyumba za ulevi (*bar*) ambazo haziendani na silka na mila za Kizanzibari ambazo zinapaswa kulindwa ili zisichafuliwe kwa kisingizio chochote kile.

(a) Je, kwani Mkoa wa MjiniMagharibi umelazimishwa uwe Mkoa wa walevi kwa kujengwa baa kila sehemu.

(b) Serikali ya Mkoa haioni haja sasa kusitisha kabisa utoaji vibali vya kuanzisha *bar*.

(c) Hatua gani zitachukuliwa kuondosha baa zinazojengwa kwenye makaazi ya watu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ** – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 275 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kihistoria ya nchi yetu suala la vileo kabla ya Mapinduzi matukufu lilitungiwa Sheria ili kuweka udhibiti wa uuzaji na utumiaji wa vileo. Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 miongoni mwa Sheria ambazo tuliendelea nazo ni Sheria ya Vileo, Sheria ambayo hadi sasa inaendelea kutumika.

Katika hali hiyo na kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na kuimarika kwa shughuli za utalii wa ndani na nje, busara ilitumika kwa kuongezwa idadi ya maeneo ya kuuzia vileo yakiwemo mahoteli ya kitalii, nyumba za kulaza wageni pamoja na vilabu. Hata hivyo mustakabali wa wananchi wa Mkoa wa Mjini/Magharibi na Wazanzibari kwa ujumla katika masuala ya mila, silka na desturi na utamaduni wao kwa lengo la kulinda heshima na utu wao havina mjadala wala mbadala.

Kwa mnasaba huo, Mkoa wa Mjini/Magharibi haujawahi na wala hautarajii kulazimisha Mkoa huu na watu wake kuwa Mkoa wa walevi kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mustakabali wa watu wa Mkoa huu na taifa kwa ujumla.

(b) Mhe. Spika, kimsingi siwezi kupingana na hoja ya Mhe. Mwakilishi ingawa suala la vileo lipo kisheria. Suala la kusitisha kabisa utoaji wa vibali vya kuanzisha *bar* katika Mkoa wa Mjini/Magharibi linahitaji mazingatio mapana ya Sheria ili kubaini faida na hasara zake kwa jamii.

(c) Mhe. Spika, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa mara kwa mara imekuwa ikichukua hatua za kuwaelimisha wananchi juu ya haki yao ya msingi ya kuzipinga *bar* au kumbi za starehe zilizojengwa kwenye makaazi yao ambazo zinapelekea mmong'onyoko wa maadili katika jamii. Endapo pingamizi hizo zikibaini kuwa zina ukweli, hatua za kusitisha utoaji wa kibali cha uendeshaji wa *bar* hizo au kumbi hizo huchukuliwa na Bodi ya Vileo.

Mhe. Spika, sambamba na hilo endapo maamuzi ya Bodi hayakuzingatiwa uhalisia wa hoja zilizowasilishwa na wananchi wanatakiwa kutoa taarifa kupitia Masheha wao Serikali ya Mkoa kufuatilia kwa karibu na ikibidi hatua za kiutawala kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kusitisha leseni na kuzifungua *bar* au kumbi hizo za starehe.

Mhe. Spika, katika hatua za hivi karibuni Mkoa umezifungia nyumba 9 za kulaza wageni, *bar* 10 za starehe ambazo zimebainika kujishughulisha moja kwa moja na vitendo udhalilishaji na uvunjifu wa amani hapa nchini

**Mhe. Spika:** Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata swali la nyongeza, naona umerika basi namwita Mhe. Nadir Abdul-latif.

**Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf:** Bismilah Rahman Rahim Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa kuuliza swali la ziada lenye (a) na (b) kwa Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa eneo hili la Mbweni tu kuna *bar* zaidi ya 7 kati ya hizo hapo Matrekta ndizo zinazosababisha zogo kubwa kwa wanajamii na tayari wameshaleta ripoti, wameshashitaki kwa muda mrefu, lakini watu wenye *bar* wana fedha nyingi sana wanawashinda katika masuala ya kesi. Je, Mkoa itahakikisha vipi au lini wataweza kuzifunga *bar* zile mbili ambazo zinasababisha zogo wakati wote kwa jamii na kupotosha hasa silka na utamaduni wa Wazanzibari.

(b) Kwa kuwa soko la Kinyasini ambalo lipo ndani ya Jimbo langu la Chaani na soko lile ni la wananchi wa Jimbo la Chaani, lakini matukio yake wameenda kupewa watu sasa ambao wanatoka nje ya Jimbo la Chaani. Ni lini sasa tutakwenda mimi na wewe kuhakikisha kwamba watu wangu wote wanarejeshwa kama walivyokuwa mwanzo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, jibu swali (a) peke yake kwa sababu swali (b) halihusiani na swali la msingi Mheshimiwa. Ni swali zuri lakini lilete kwa maandishi kwa Mhe. Waziri.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu rafiki yangu Mhe. Nadiri Mwakilishi wa jimbo la wananchi Chaani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba hizi *bar* au shuhuli hizi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, kama kwa mujibu wa sheria na vile vile katika maelezo yangu nimeeleza namna ambavyo wananchi pale watakapoona kwamba kuna eneo ambalo haliendani au uendeshaji wa shughuli hizi hauendani na mila na desturi za maeneo husika katika maeneo hayo wanayoishi wananchi. Kwa hivyo ni utaratibu gani, ni kwamba tunawaomba wananchi waendelee kujitokeza pale muda ambapo unafika katika kuzifanyia pingamizi au kutoa pingamizi zao ili kusudi baadae hatua ziweze kuchukuliwa.

Kwa hivyo ofisi yangu mimi au Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa, haiwezi kwenda kufungia tu au kutoka kwenda kufungia maeneo ambayo tayari kuna sheria ambayo imefuatwa, kama tumeona kwamba mtu kafata utaratibu lakini baadae au sheria anakwenda kinyume na utaratibu kama vile ambavyo alivyoomba ile leseni. Sasa kama kuna tuhuma au kuna mashaka ambayo yameanza kujitokeza. Mheshimiwa naomba tushirikiane na wananchi wetu ili kusudi kufuata utaratibu huo na naamini kwamba hatua zitachukuliwa kwa sababu serikali haiko katika kuwalinda watu waovu. Mhe. Spika, naomba nikushukuru.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini vile vile nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharib katika kusimamia maswali mbali mbali yanayohusiana na mambo haya ya vileo.

Lakini mbali na kusimamia huko kumekuwa na changamoto kubwa sana la kuongezeka madanguro katika maeneo mbali mbali ya Mkoa wa Mjini/Magharibi hususan katika Jimbo la Kikwajuni katika maeneo ya Rahaleo na Mwembeshauri. Je, serikali inachukua hatua gani za dharura ili kuhakikisha madanguro haya ambayo husababisha kuondoa maadili ya Wazanzibari katika maeneo hayo niliyoyataja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni Mhe. Nassor Jazira swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama ambavyo nimetangulia kusema kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa imekuwa ikifanya kazi kubwa sana katika kuona kwamba amani na vitendo vyovyote vile vinavyoashiria uvunjifu wa amani katika Mkoa huu na kwengineko vinaendelea kuchukuliwa na kudhibitiwa kwa hali yoyote vile kwa namna yoyote vile ambavyo vitaweza kujitokeza.

Mhe. Spika, kwa kupitia fursa hii naomba niwapongeze sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na hususan Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kufanyika ambao ni ushahidi wa kila mmoja anaona.

Mhe. Spika, ni kwamba kama kuna idadi kubwa ya madanguro ambayo yameanza kujitokeza katika Mkoa huo ni imani yangu kwamba Mhe. Mkuu wa Mkoa na viongozi wenzake wananisikia. Kwa hivyo naamini kwamba jambo hili tutaendelea kulifanyia kazi lakini vile vile nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kwamba na yeye aendelee kushirikiana nasi katika kuona kwamba tunatoa mashirikiano ili kuyabainisha kwa sababu mambo mengine inawezekana kwamba watu wamechukua vibali kwa sura nyengine lakini wanachotekeleza ni mambo mengine mawili tofauti. Kwa hivyo tusaidie Mheshimiwa pale ambapo tutahitaji kupata msaada kutoka kwako ili kutusaidia kubainisha katika maeneo kama hayo na hatua zitaendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa sheria, ahsante Mheshimiwa.

**Nam. 204**

**Uhaba wa Wanasheria wa Watoto Pemba**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub): -** Aliuliza:

Kwa muda mrefu kumekuwa na upungufu wa mwanasheria wa kesi za watoto kisiwani Pemba aliyekuwapo ni mwanasheria mmoja ambaye hatoshi, kesi zote anakwenda peke yake Wete, Chake Chake, Mkoani na Micheweni na kusababisha kushindwa kufanyakazi zake kwa ufanisi.

Je, Serikali haioni ulazima wa kuongeza wanasheria wengine ili kesi za watoto zisimamiwe kwa uweledi na watoto wapate haki zao kisheria.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi Wa Umma na Utawala Bora** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye kifungu (a) lenye Nam. 204 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba bado hakuna Mahakimu wa Mahakama Maalum za Watoto. Kesi za watoto zinasikilizwa na Mmahakimu wa mikoa miwili ya Pemba mara

moja kwa wiki. Hivyo wanasheria wa Mahakama hizo huendesha kesi za watoto siku husika.

Mhe. Spika, kwa sasa hivi Serikali haioni haja ya kuweka mwanasheria maalum wa kuendesha kesi za watoto kisiwani Pemba kwa sababu Pemba hakuna Mahakama Maalum ya Watoto na pia wanasheria wetu wote wa Serikali waliopo wana uwezo wa kusikiliza kesi hizo za watoto, ahsante.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pili niseme tu kwamba kadhia kubwa katika nchi yetu ambapo wananchi wengi wanalalamika juu ya adha wanayoipata watoto wetu katika kesi mbali mbali, na mara nyingi tunategemea wanasheria wawepo na kuwasaidia watoto hawa kwa kipindi kinachofikia. Lakini katika jibu Mhe. Naibu Waziri amesema tu kwamba kwa upande wa Pemba kesi hizo huwa zinasikilizwa kwa kipindi maalum. Kwa kuwa kesi hizo zinatokea mara kwa mara na zipo nyingi, hivyo haoni pana mpango wa makusudi kuekewa siku maalum zikaongezwa siku kwa ajili ya kuliondoa tatizo hilo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi Wa Umma na Utawala Bora:** kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa siku hizi ambazo Mahakimu hawa wa Mikoa katika Mikoa yote miwili ambapo Mahakama ya Wete na Mahakama ya Chake Chake Mahakimu hawa huwa wanasikiliza kesi tunaona kwamba wanatosha, lakini kwa mujibu wa kesi ambazo zilizokuwepo lakini pale ambapo tutakapoona kwamba wingi wa kesi umekithiri zaidi basi ni vyema tunaweza kufanya hivyo ambavyo ulivyopendekeza au ulivyouliza kuongeza siku badala ya moja zikawa mbili au zaidi hizo nashukuru.

**Nam. 262**

**Ukarabati wa Jengo la Kihistoria la Beit-El-Ajaib Zanzibar**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said** - Aliuliza:

Katika juhudi za kuendeleza Zanzibar na wananchi wake na hasa maendeleo katika utalii Serikali haina budi kuimarisha vivutio vya utalii kama vile Mji Mkongwe pamoja na nyota ya Mji huo Beit-el-Ajaib lakini kwa kipindi kirefu jengo hilo lipo katika hali mbaya sana hata kuweza kuanguka au kushindikana kukarabatiwa na kurudi katika hali yake ya uhalisia.

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kukaa vile jumba la Beit-el-Ajaib ni kuipotezea mapato Serikali.

(b) Je, Serikali haioni kuwa tunaweza kulipoteza jumba la Beit-el-Ajaib ambayo ni hazina yetu na tukajuta.

(c) Je, Serikali imefikia wapi kuhusu matengenezo ya Beit-el-Ajaib.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleima Sarahani Saidi Mwakilishi makini wa Jimbo la Chake Chake swali lake Nam. 262 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali inafahamu vyema kuendelea kukaa vile Beit-el-Ajaib kunaipotezea mapato hasa kwa vile mpaka wakati wa kupata athari ndilo jengo lililokuwa likiingiza mapato kuliko yote yaliyo chini ya Idara hii.

(b) Mhe. Spika, aidha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajua kwamba Beit-el-Ajaib ni hazina kubwa kwa Zanzibar na dunia kutokana na vigezo vya kisanii, usanifu majengo na hata vionjo vya kisanaa na utamaduni na kwamba kupotea hazina hii kunaweza kutupelekea kujuta na kupotezea kumbukumbu muhimu kwa nchi yetu.

(b) Mhe. Spika, juhudi kubwa imekuwa ikichukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Oman na *UNESCO* ili kuliokoa jengo hilo. Hivi sasa sehemu hizo tatu tayari zina "*Project Write up"* inayokubalika ambapo Serikali ya Oman ndie Mfadhili Mkuu ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Sarahani Said:** Nashukuru sana Mhe. Spika, na nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya ukweli ambayo amenipa.

Mhe. Spika, na mimi naomba kidogo nichukue dakika moja nielezee kidogo naomba tu kwa sababu lazima nielezee kutokana na historia hii.

**Mhe. Spika: H**apana Mheshimiwa usichukue dakika nzima Mheshimiwa, uliza kwa ufupi sana

**Mhe. Suleiman Sarahani Said: A**hsante Mhe. Spika, kutokana na kadhia hii ya Beit-el-Ajaib, Mhe. Naibu Waziri amekiri kutokana na kwamba utalii wetu wote asilimia kubwa Beit-el-Ajaib ndio ilokuwa inatutilia mapato. Lakini Mhe. Spika, kulikuwa na kadhi kubwa ya kuambiwa kwamba *UNESCO* hajatoa kibali kwa muda mrefu, lakini pia sasa hivi tumekuja na suala la kusema kwamba mfadhili kutoka Oman ndie atakayetufanyia suala hili.

(a) Mhe. Spika, hichi si kiwanja kwamba kinasubiri mpaka siku yoyote atakapokuja, hili ni jengo na ni jengo kongwe na wakati wowote linaweza kuporomoka. Mhe. Naibu Waziri namuuliza. Je, amefikia wapi yeye na mfadhili mkuu wa Oman kuleta *deadline* ya kuanza kwa ukarabati huu.

(b) Mheshimiwa ni kwamba kwa vile alisema ndio linalotoa mapato. Naomba Mhe. Naibu Waziri aniambie kwa siku lilikuwa linaingiza mapato kiasi gani na tokea lifungwe limeshaingiza hasara kiasi gani.

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri jibu swali (a) kwa sababu swali (b) naona litahitaji takwimu ambazo sidhani kama utakuwa unazo hapo. Kwa hivyo jibu swali (a), hilo la pili liache lije kwa maandishi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:** ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahani Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli mara nyingi tulikuwa tunaambiwa serikali inasema kwamba inasubiri kibali cha *UNESCO*, lakini kwa taarifa tu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa faida ya wananchi wa Zanzibar na Baraza lako Tukufu napenda nijibu kwamba sasa hivi tayari mfadhili yule Oman ameshafika hapa na tumeshatiliana saini na mikataba ya kulifanyia ukarabati jengo hili na tayari kuna *contractor* wa mwanzo mzungu tayari ameshaingia hapa kwa kuanza kazi hii wakati wowote kuanzia sasa, ahsante Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pia nimshukuru Mhe. Suleiman Sarahani kwa swala lake la nyongeza.

Mhe. Spika, ni kweli maandalizi yote ya kuanza ujenzi wa Beit-al-Ajaib yamekamilika na ni kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tayari mkataba umesainiwa wa ujenzi huo unaomshirikisha mfadhili wetu Serikali ya Oman. Na ni kweli Mhe. Spika, kwamba utaratibu wa ujenzi Mji Mkongwe una Kanuni zake na taratibu zake. Kwa hivyo ilichukua muda kutokana na kuwasiliana na wenzetu wa *UNESCO,* lakini sasa kila kitu kipo sawa na baadhi ya maandalizi yameanza ikiwa pamoja na kuondoa vifaa muhimu vilivyokuwa ndani ya jengo lile kuvipeleka katika jengo la jirani iliyokuwa nyumba ya kulelea watoto ili kazi ianze na karibuni hivi tunategemea meli yenye baadhi ya vifaa kwa ajili ya ujenzi huu kuwasili nchini na shughuli zimeanza rasmi.

Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe. Suleiman na wananchi wote kwamba ujenzi ule utaendelea vizuri na jengo lile linadhibiwa vizuri ili lisianguke. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

**Nam. 251**

**Kuimarisha Kilimo cha Zao la Muhogo Zanzibar**

**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil (Kny: Mhe. Ali Khamis Bakar) –** Aliuliza:

Naipongeza Serikali ya China kwa kutoa (*Offer*) tenda kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu Wizara ya Kilimo kuliimarisha zao la muhogo kwani wanahitaji kwa kiwango kikubwa bidhaa hiyo nchini kwao.

Na kwa kuwa Zanzibar ina vijana wengi ambao hawana ajira itatoa fursa ya kuwaajiri vijana hawa.

(a) Je, Wizara ya Kilimo imewasiliana na Serikali ya China ili kujua aina gani ya muhogo ambayo inahitajika kwa ajili ya soko hilo.

(b) Je, Serikali imeshajihisha vipi wakulima wa zao hili ili waweze kulima zaidi ili kufikia mahitaji ya soko linalohitajika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe.Mwakilishi swali lake Nam. 251 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Lakini kabla sijamjibu swali lake naomba nitoe maelezo mafupi tu kuhusu zao hili la muhogo. Zao hili la muhogo limeshuhulikiwa sana hapa Zanzibar na tafiti nyingi sana zimefanyika na tulikuwa tunashirikiana na Nigeria katika kufanya tafiti za muhogo na tulitoa mbegu za aina mbali mbali. Hivi sasa tunazo mbegu za muhogo aina nne ambazo tumezipendekeza. Kuna mbegu hii aina ya Machui, kuna mbegu ya Kizimbani, kuna ya Kama na ya Mahonda. Zao hili la muhogo kwa kweli ni zao ambalo linaota kila mahala hapa Zanzibar na linatumika kama zao la pili kwa chakula ukiacha mchele.

Mhe. Spika, uzalishaji wa muhogo hapa Zanzibar ni tani 160, kati ya hizo 55 zinatumika kwa chakula zilizobaki huwa zinatumika ama kwa kusaga unga, ugali au chipsi na kadhalika. Kwa hivyo uwezo wa kusafirisha Zanzibar hadi hivi sasa tunaweza tukasafirisha tani 50 kupeleka huko China. Sasa kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakar Doholo ni kwamba.

a) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi imepata taarifa kuhusu kuwepo kwa soko la muhogo Jamhuri ya Watu wa China. Kwa hivi sasa Wizara inaendelea kufanya mawasiliano na Taasisi husika ili kufahamu kiwango, sifa na aina za muhogo zinazohitajika

b) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inapenda kumuarifu Mhe. Mjumbe na Baraza lako Tukufu kwamba baada ya Wizara kupata taarifa sahihi kuhusiana na kiwango sifa na aina ya muhogo unaohitajika nchini China, hatua za kuwahamasisha na kuwaelimisha wakulima zitafanyika kwa mujibu wa utaratibu. Hata hivyo tunasema kwa mahitaji yetu tunaendelea kuhamasisha vikundi mbali mbali za muhogo lakini tutakapofanya biashara tutawahamasisha wafanyabiashara kwa mujibu wa zile *recommendation* watakazozitaka wao watu wa China ahsante.

**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi tena kwa kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kwa kuwa kakiri kwamba soko lipo nchini China na hii ni *export product* na itachukua muda kusafirisha ikiwa soko limeshakubali kutoka Zanzibar hadi China. Je elimu gani na *technic* gani

wizara imejiandaa kuwapa wakulima ili muhogo ule uweze kufika China katika hali yake ya asili, katika jibu hilo la msingi atakalonipa atakubaliana na mimi kama taaluma hiyo ni muhimu kwa sababu muhogo hata nchi za Ulaya wananunua kutoka Afrika lakini wanatumia mishumaa, huu mshumaa wa kawaida kufanya uwe *coated* ndipo uwe muhogo wa asili wakati wa kuliwa. Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, mbinu zitakazotumika kuwashajahisha wananchi kwanza ni kuhamasisha walime kwa wingi kwa sababu tunafahamu kwamba zao la muhogo watakalolihitaji watu wa China ni jingi sana, watahitaji si chini ya tani 300 kwa mwaka hadi tani 700 kwa mwaka au na zaidi ya hapo na sisi uzalishaji wetu bado mdogo, nimesema tani hamsini. Kwa hivyo tutahamasisha wazalishe kwa wingi kwanza ili tuweze kukidhi haja ya soko, lakini pia tutashirikiana na wenzetu Bara kwa sababu sisi hatuwezi kutosheleza hata tukifanya vipi, wanahitaji muhogo mwingi sana kwa sababu matumizi yao ni mengi, wanataka kutumia kwa ajili ya kutengeneza *starch*, kutengeneza biskuti, kutengeneza mambo mengi tu.

Kwa hivyo tutahamasisha kwanza kuzalisha kwa wingi na kuzalisha mbegu ile inayotakiwa ambayo itakuwa na *bright matter content* yaani tuseme itakuwa na *starch* asilimia si chini ya arubaini kwenda mbele, usiwe muhogo ambao mchege wenye maji mengi wenye nini, uwe na *starch* nyingi, unga unga ule uwe mwingi, ndio muhogo ambao utatakiwa. Kwa hivyo baada ya kuthibitisha tu tutahakikisha mbegu tulizonazo zinafaa lakini tutathibitisha kwamba pia wanazalisha viwango vile ambavyo vinahitajika na muhogo wanaotaka kuupeleka China ni muhogo mbichi na nafikiri kwa masharti yao walioyokubaliana wenzetu kule Bara na kwa sababu soko letu ni moja sote ni Watanzania, basi tutakubaliana namna tutakavyolisafirisha hilo zao ili lifike China vile ambavyo linavyotakiwa.

Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lakini kabla ya kumuuliza swali Mhe. Naibu Waziri nimpongeze kwa majibu yake na maelezo yake ambayo mara nyingi anapoyatoa maelezo hayo kabla ya kujibu swali ndani ya *'Order Paper'* yetu inakuwa hayamo kwa hiyo tunakuwa tinapata shida sana kusikiliza majibu yake na maelezo ya kabla ya majibu. Kwa hiyo tungemuomba sana Mhe. Naibu Waziri anapotoa majibu na maelezo kwanza yale maelezo tuyaone humu kwenye *'Order Paper'* ili na sisi tujuwe tunauliza swali gani la nyongeza.(*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako umetaja aina nne hapa za muhogo ambazo zinalimwa sana na Wizara ya Kilimo ndio inazifahamu, lakini kama tunavyofahamu kwamba ndani ya wakulima wetu wanaolima zao hili la muhogo tunafahamu kwamba kuna mbegu zaidi ya saba ambazo ni nzuri na zinafahamika. Je, kuna kitu gani ambacho wizara na wakulima hakuna mawasiliano baina ya kujua hizi mbegu mpaka leo hii tunajiwa mbegu nne ambazo wizara ndio wanazifahamu, wakati tunafahamu kwamba kuna mbegu zaidi

ya saba. Hizi nyengine zinatoka wapi na zinalimwa na wakulima gani na kwa nini zikalimwa wizara ambapo hawazifahamu.(*Makofi*)

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba nimjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake alilouliza kama ifuatavyo.

Ni kweli kuna mbegu zaidi ya tano hilo tunalikubali na zipo zaidi ya tano liko hata ishirini zaidi ya hizo, lakini tunazikusanya hizi mbegu tunazifanyia utafiti pale Kizimbani nafiri uliwahi kuyaona mashamba ya muhogo, mashamba ya utafiti pale Kizimbani ni aina nyingi sana za muhogo. Sasa tumeziona hizi nne ndio zile ambazo zinaweza zikasaidia sana kwa sababu zinahimili maradhi, zinastahamili ukame, zinastahamili wadudu hata kama zinashambuliwa lakini mashambulizi yake sio makubwa kama zinavyoshambuliwa zile mbegu za aina nyengine na wakati huo huo pia hata utamu wa muhogo, watu wengi wanapenda ile mihogo mitamu hawapendi michungu. Kwa hivyo hizi *varieties* tunazotoa aina tulizozitoa ni zile mbegu ambazo zina utamu aina fulani kimuhogo si utamu wa sukari lakini ni utamu wa kimuhogo.

Mhe. Spika, napenda nimthibitishie kwamba tunajua zipo kweli mbegu nyingi sana hapa Unguja za muhogo kwa sababu muhogo ni chakula cha jadi hapa Zanzibar. Hivyo tutaendelea na tafiti zaidi kuona zile ambazo zitazidi kuwa bora tuziingize ziwe pamoja na jumla hii ya nne ili ziwe tano, sita, saba hata kumi na kuendelea.

Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kuniona kupata fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini nina swali la nyongeza.

a) Nilitaka kujua umetuambia katika majibu yako kwamba Zanzibar tunazalisha tani 160 za muhogo. Ni utaratibu gani ambao unaotumika ili kuweza kupata takwimu hii ya tani hizi 160.

b) Nilitaka kujua umesema umewahamasisha wakulima katika kuwapatia mbegu hizo nne ambazo umezitaja hapa, lakini nilitaka kujua kuhamasisha umewapa mbegu tu au unawatembelea kabisa hawa wakulima kuona jinsi gani ya uzalishaji wao na wanalima kitaalamu ili tukaweza kupata mahitaji yale ambayo tunayatarajia tupate muhogo wa kula sisi na wa kupeleka huko China.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mheshimiwa mwenye *experience* kubwa sana kwenye Baraza hili Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake kama ifuatavyo.

a) Utaratibu wa takwimu na kama tunavyofahamu tuna mabwana na mabibi shamba wengi sana huko mashambani ingawa kuna baadhi ya sehemu hawajafika, lakini tunategemea tutawaongeza ili kila sehemu iwe na bwana au bibi shamba kukusanya hizi takwimu,

lakini pia tunakusanya takwimu hizo mwahala mule ambamo munatoka muhogo na kuingia kwa mauzo na kadhalika. Kwa hivyo tunajua inawezekana ikawa takwimu si sahihi moja katika mambo ambayo tutayashughulikia sana ni kuhakikisha kwamba takwimu tunazozichukua ni za uhakika na za kweli na tutashirikiana na wale watu wa *data hub* wa Dar es Salaam kuzitafuta zile *gadget* ambazo zitawezesha kukusanya *data* za ukweli huko vijijini.

b) Kwamba wakulima wanatembelewa nimesema kuna mabwana shamba na mabibi shamba huko, lengo wawafuate wakulima na wawaelimishe na *recommendation* mbali mbali za kilimo ili waweze kuzalisha zaidi na hivyo hivyo tuna Kitengo chetu cha Elimu kwa Wakulima nacho kinapika huko kinawaelimisha wakulima wetu ili waweze kuzalisha zaidi. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi ni kwamba hawa watu wanafuatiliwa na wanafahamishwa pale ambapo hawajafika inawezekana ikiwa hawajafika kwa bahati mbaya lakini pia tutathibitisha kwamba wanafanya vile ambavyo tunakusudia wafanye.

**Mhe. Spika:** Majibu ya nyongeza kutoka kwa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika niendelee kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa kuendelea kujibu maswali ambayo yanaonesha wazi kwamba yamefanyiwa ufuatiliaji na taarifa zake zinavyotolewa kwamba zina usahihi wa aina yake. Lakini Mhe. Spika, ningependa tu kutoa taarifa kwa wananchi hususan wakulima wa zao hili la muhogo.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea wawekezaji wa aina tatu kutoka miji tofauti nchini China na wawekezaji hawa ndio wamefanya mazungumzo na Wizara ya Kilimo upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wameweza kukubaliana mahitaji ya kuwapatia muhogo kwenda soko la nje la China kwa tani zinazodi zaidi na zisizopungua tani mia tatu kwa mwaka. Kama tunavyolijua zao la muhogo linavyozalishwa halizalishwi mara mbili kwa mwaka isipokuwa kwa mbegu maalum zinazoweza kustahamili uzalishaji mara mbili kwa mwaka.

Mhe. Spika, lakini kiwango hiki wenzetu wale wawekezaji wametaka zaidi ya tani mia saba kwa mwaka, lakini kutoka na tafiti zilizofanywa ndani ya nchi yetu Tanzania tumekuwa na uwezo wa kwanza kuona tuanze na kiwango cha tani mia tatu. Mazungumzo hayo yamekamilika na mahusiano mazuri tuliyonayo baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Wizara zetu hizi mbili, tumekubaliana sisi kuweza kuongeza idadi hiyo endapo tunauwezo wa kuzalisha. Kilichokuwepo hapa ni kwamba muhogo unaotakiwa na watu wa China ni ule ambao una uwanga zaidi, kuna mihogo kama tafiti zinavyoonyesha kama alivyouliza Mhe. Hidaya ipo muhogo wa aina nyingi sana na uzalishaji wake unatoa aina tofauti ya muhogo. Kwa hivyo wenzetu wa China wametaka ule muhogo wenye *maximum milled* ya *starch* ambayo inaweza ikapatikana hapa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara.

Kuna swali mheshimiwa limeulizwa juu ya usafirishaji. Kama tunavyojua sio suala zima la uwekaji wa muhogo una matatizo. Majumbani mwetu tukiuweka muhogo leo, ndani siku mbili hususan huu muhogo wenye *starch* nyingi, muhogo mtamu hauwezi kuhimili kukaa ndani ya siku tatu, unavunda unaleta mabadiliko ya rangi na unatoa ile haiba na uwezo wa kuwa na zao lenye viwango la kusafirisha. Kutokana na mnasaba huo wenzetu tayari wametengeneza *laboratory* ya kuhakikisha kwamba muhogo una viwango unaposafirishwa na kuwekwa kwenye kontena unavumilia kwa siku zile za usafirishaji kutoka Tanzania hadi utakapofika China.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa Zanzibar hatuna sehemu ya kufanya kiwango hivyo lakini kama yalivyo mazao mengine, vile vile tunaposafirisha nje ya nchi yanapaswa yapate viwango kupitia kwa wenzetu Tanzania Bara. Kwa hivyo kwa kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake, sisi hizi tani hamsini ambazo tupo tayari kuzipeleka na wananchi wenye uwezo wa kulima muhogo kwa wingi, waendee kulima muhogo kwa wingi ili tuweze kuzipeleke tani hizo, zitapelekwa kwanza Tanzania Bara ziwekwe mpangilio wake wa kuweza kuhifadhi ili ziweze kusafiri.
Nashukuru sana tena majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo kwa majibu yake lakini uwezo huo tunao wa kuweza kuhifadhi muhogo ili ukaweza ukafika kule bado ukawa una *status* ile lile ikiwa wameutaka mkavu au wameutaka mbichi, wakulima sasa hivi ni kuongeza jitihada ya kulima muhogo na Wizara ya Kilimo itashirikiana na wakulima ili kuhakikisha inaratibu taratibu za kusafirisha kwenda nje ya nchi.(*Makofi*)

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe pamoja na umuhimu wa swali hili naomba kutoa nafasi ya upendeleo kwa Mhe. Mtumwa Suleiman Makame ili aulize swali la nyongeza.

**Mhe. Mtumwa Suleiman Makame:** Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya upendeleo.

Kwanza namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu majibu yake kwa madaha. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri katueleza kwamba soko la muhogo lipo na kwa kuwa hapa kwetu Zanzibar kuna wakulima wengi sana wa muhogo. Je, kwa kila tani inatakiwa kiasi gani ili wananchi wazidi kuhamasika kulima muhogo huo. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Mhe. Naibu Waziri majibu. Mhe. Waziri mwenyewe ninadhani yupo tayari.

**Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Spika na mimi niendelee sana kumshukuru Mhe. Mtumwa Suleiman Makame kwa swali lake ambalo limejaa ufundi. Kwanza pongezi zake na mimi nazikubali napende ijulikane wazi kwamba kwa Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na alivyoeleza Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba Mheshimiwa anapojibu huwa anaelewa ule ufahamu wa kitu.

Mhe. Naibu Waziri ni mtu ambaye ana utaalamu wa kilimo, ameanza *certificate* kwenye kilimo, amefanya *diploma* kwenye kilimo, ana *degree* kwenye kilimo, amefikia mpaka *level* ya *PhD* kwa masuala ya kilimo. Kwa hivyo anapofika hapa anapoanza kutoa maelezo kidogo ile taaluma yake hupenda aipeleke kwa wananchi ili ifahamike. Ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi wakatuvumia wakamuona Mheshimiwa kwamba anawafahamisha wananchi katika kuwapa

taaluma ya elimu ambayo yeye mwenyewe amerowa nayo na ameizoewa na anaifahamau ipasavyo.(*Makofi*)

Baada ya hapo napenda kumjibu Mhe. Mtumwa Suleiman Makame swali lake. Zao kwa wenzetu wa China wana bei nzuri tena sana. Hapa petu muhogo hatujajua vipimo sana vya kuupimia lakini wenzetu wanapima kwa tani ambayo inaweza ikagawika kwa kilo, sasa ukitizama wastani wa bei walizozitaka wao muhogo kwa kilo unaweza ukafika hata dola mbili. Kwa hivyo kama muhogo utafika dola mbili na unavyojulikana uzito wa muhogo ni mizizi michache ambayo itakuwa pengine ni elfu nne na kidogo. Kwa hivyo ukitizama bei hizi ambazo wenzetu Wachina wameanza kuzikisia ni suala lenye mvuto wa bei, tofauti na muhogo unavyouzwa kwetu sisi. Fungu la elfu moja linaweza likafika kilo moja na nusu ambapo sasa kwetu sisi itakuwa ni elfu nne utakaposafirishwa kwenda China. Kwa hivyo kutokana na takwimu hizo bado tuwahamasishe wakulima soko lipo, bei nzuri na wao wanaweza wakafanikiwa. Mhe. Spika, si hili tu hata vanilla. Juzi wenzetu wa China wametueleza kwamba vanilla imepanda kutoka dola mia saba mpaka dola mia tisa kwa kilo, kitu ambacho soko hili linaonesha linavutia kuliko masoko mengi sana ya uzalishaji wa mazao ambayo yanaweza kuzalishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba sana kuwahamasisha wakulima na wakwezi waendelee kurudisha mazao yetu ya kilimo hapa Zanzibar. (*Makofi*)

Ahante sana Mhe. Spika.

**Nam. 246**

**Ujenzi wa Viwanda Zanzibar**

**Mhe. Ali Suleiman Ali – Aliuliza:**

Katika harakati za kuitikia wito wa Zanzibar ya Viwanda, wananchi wameitikia wito huo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda mbali mbali hapa nchini. Katika harakati za ujenzi wa viwanda hivyo.

Je, Waziri ni viwanda vingapi vimejengwa hadi sasa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) swali lake Nam. 246 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika harakati za kuitikia wito wa Zanzibar ya viwanda, matokeo ya kuanzia 2016 mpaka sasa ni kama ifuatavyo:-

a) Miradi minne imeanza majaribio ya uzalishaji wa viwanda kama vifuatavyo:
   i) *Sansi Group of Companies*: Kiwanda cha Maji – Kombeni,
   ii) *Meesab Packaging*: Kiwanda cha Mifuko ya Karatasi – Maungani
   iii) Kiwanda cha Mafuta ya Nazi: *Amaan Industrial Park.*
   iv) Kiwanda cha Mabati: *Amaan Industrial Park.*

b) Miradi miwili imo katika hatua mbali mbali za uanzishaji miradi yao baada ya kukamilisha taratibu na *ZIPA* ni kama vifuatavyo:-

i) Kiwanda cha Vifaa vya Uvuvi.
ii) Kiwanda cha Vipodozi.

c) Maombi mapya ya kuanzisha miradi ya viwanda chini ya *ZIPA* ni kama ifuatayo:-

i) Kiwanda cha Uzalishaji wa Rangi.
ii) Kiwanda cha Uhunzi wa Bidhaa za Chuma.
iii) Viwanda vya Matofali kwa kautumia teknolojia ya kisasa.
iv) Kiwanda cha Usonara ya Usarifu wa Vito vya Thamani.
v) Kiwanda cha Kuzalisha simu za Mkononi.
vi) Kiwanda cha Chumvi.

Mhe. Spika, ahsante sana.

**Mhe. Ali Suleima Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa azma kuu ya kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa ya viwanda na ndio mwelekeo ya sera ya Chama cha Mapinduzi, lakini katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri ametuambia kwamba hivi sasa katika swali (a) alilolijibu kuna viwanda vinne ambavyo vimo katika majaribio.

1. Kiwanda cha Maji Kombeni
2. Kiwanda cha Mifuko ya Karatasi Maungani
3. Kiwanda cha Mafuta ya Nazi *Amani Industrial Park*
4. Kiwanda cha Mabati huko huko Amani

a) Je, katika majaribio hayo ni mafanikio gani yamepatikana hadi sasa.

b) Kwa kuwa muelekeo wa viwanda ni msingi wa kuongeza biashara kutoka Zanzibar kwenda nje ya nchi. Ni ni soko gani tunalitegemea litapelekwa bidhaa hizi pindi zikipatikana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, mafanikio makubwa yaliyopatikana kwanza hawa waliokuja kuzalisha viwanda kuitikia wito wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuja kuanzisha viwanda ambayo Sera ya Chama cha Mapinduzi ndio inayoitaka Zanzibar ya Viwanda na Tanzania ya Viwanda.

Mhe. Spika, lakini mafanikio ya pili katika viwanda hivi vinne kuna ajira mbali mbali zimezuka hapa ambayo ni mafanikio makubwa na hili ni kimbilio la kila nchi ambayo inataka kuanzisha viwanda kwa madhumuni ya watu wake kupata ajira. Vile vile viwanda hivi mheshimiwa vinalipa kodi ambayo ndio inayoleta tija katika mambo yetu mbali mbali kama hospitali, barabara na mambo mengine. Hayo ni mafanikio makubwa mheshimiwa yaliyopatikana kwa majaribio ya viwanda hivi vinne.

b) Mhe. Spika, naomba kumjuilisha Mhe. Mwakilishi kwamba kuhusu soko hii kwanza ni Sera ya Chama cha Mapinduzi kwamba tunataka Zanzibar ya Viwanda, tunataka na Tanzania ya Viwanda. Mheshimiwa naomba kumjuilisha Mhe. Mwakilishi na Wawakilishi wengine kwamba nchi zote duniani zilipoanza kuendelea zilikuja na Mapinduzi ya Viwanda. Mhe. Spika, leo China tunaijua ni nchi inayoendelea kwa sababu ina viwanda, Uingereza tunaiita nchi iliyoendelea, Marekani na Canada kwa sababu ya viwanda. Mhe. Spika, Sera ya Chama cha Mapinduzi inaitaka Zanzibar ya Viwanda na inaitaka Tanzania ya Viwanda.

Mhe. Spika, anauliza soko ni kwamba nchi za wenzetu kwa mfano Canada na nchi nyengine zina utaratibu ufuatao. Ili nchi iendelee lazima kuwe kuna uzalishaji wa ndani mwingi na uingizaji wa bidhaa uwe kidogo, hiyo ndio *theory* ya uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumwambia kwamba kama soko bidhaa za ndani zitatosha, basi Wizara ya Biashara na Viwanda inayo sheria ya kulinda wazalishaji wa ndani. Aidha, kwa kuwaongezea kodi wale wanaoingiza au kwa kuwafungia kabisa na nchi za wenzetu wanafanya hivyo. Kwa mfano, nchini Uingereza, Ufaransa duniani ndio inayozalisha nyama kwa wingi na nyama yake ni bora na nzuri, lakini hairuhusiwi kuingia Uingereza kwa sababu ya kuwalinda wazalishaji wa ndani.

Mhe. Spika, kadhalika na Denmark pamoja na Amsterdam wanazalisha maziwa kwa wingi lakini hayaruhusiwi kuingia katika soko huria la Uingereza kwa sababu ya kuwalinda wazalishaji wa ndani. Na sisi kwa sababu tuna sera ya viwanda tunataka Zanzibar ya viwanda na Tanzania ya viwanda tutahakikisha wazalishaji wetu wa ndani tunalinda kwa bei yoyote ili watu wetu wapate ajira na tupate kodi.

**Mhe. Hidaya Ali Makame:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona tena ukaweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake lakini napenda kumuuliza swali kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Waziri ametwambia katika mafanikio ambayo yanapatikana ikiwemo ni ajira na mimi kama ni mwakilishi anayewakilisha vijana Mikoa yote hapa Zanzibar nataka kujua ni vijana wangapi ambao tayari wamefaidika na hizo ajira ambazo tayari zimeanza katika miradi minne hii ambayo imeanza majaribio.

b) Pia katika majibu yako hapa miradi minne ambayo umeitaja ni Kiwanda cha Mafuta ya Nazi pale Amani. Mhe. Naibu Waziri nataka kujua kwa sababu tunafahamu Zanzibar nazi imekuwa ni shida kuliko kitu chochote, imefikia bei ya nazi moja ni shilingi 1,500/-, tunataka kujua. Je, haya mafuta ya nazi ambayo tayari kiwanda hiki kimeshaanza majaribio hizi nazi zinatoka wapi. Kama zinatoka hapa Zanzibar ni wakulima wangapi wa zao hili la nazi ambao wanaendelea kufaidika na kuimarika kwa kuanzishwa kwa majaribio ya Kiwanda hiki cha Mafuta ya Nazi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, vijana ni wengi ambao wamefaidika katika viwanda hivi vine. Kwa kweli idadi ya namba halisi ya vijana hao ni wangapi hiyo naomba nimjibu kwa maandishi. Lakini katika viwanda hivi vinne vyote mimi nimevitembelea na wafanyakazi wa pale ni vijana ambao wamefaidika. Namuomba atambue kwamba jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Sera ya Viwanda ni kuwawezesha vijana kupata ajira kama walivyopata ajira katika hivi viwanda vinne.

b) Mhe. Spika, ni kweli anavyosema kwamba nazi zimekuwa shida lakini naomba kumwambia nazi ni shida lakini zipo, nazi Zanzibar zipo bado kuna watu hawali mafuta isipokuwa chakula cha nazi ingawaje bei yake tu imepanda kutokana na sababu mbali mbali. Kwa hivyo nazi zote zinazozalishwa Kiwanda cha Mafuta ya Nazi kutoka pale Amani ni nazi kutoka Zanzibar, kwa sababu nazi bado zipo, minazi ipo ingawaje ni michache kidogo lakini ipo na bado nazi kidogo bei imepanda lakini zipo ukienda sokoni hapo sasa hivi nazi zimejaa zinapatikana. Mhe. Spika, nazi zipo na kuna watu wanarudia kusema hawali chakula cha mafuta lazima wale chakula cha nazi, nikiwemo mimi kwa sababu ndio utamaduni wetu. Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** *Bimsilahi Rahman Rahiim.* Mhe. Spika, naomba kumuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b) Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa wafanyabiashara wote nchini Zanzibar wanategemea sana Wizara ya Biashara na Viwanda pia kupitia *Chamber of Commerce. H*adi hivi leo tayari wizara yako imekaa na wafanyabiashara wakubwa wa Zanzibar ili kuweza kushauriana na kujadiliana vipi wataweza kujenga viwanda.

b) Kwa kuwa nchi nyingi sehemu ambazo wameziweka za viwanda zina sehemu maalum na Zanzibar tumeona mtu anajifungulia kiwanda sehemu anazotaka yeye. Je, wizara yako imejipanga vipi kutafuta maeneo yaliyokuwa ya nje ya mji kwa ajili ya viwanda vyote ikiwa cha saruji na vyenginevyo ili kuweza kuhakikisha kwamba *pollution* haipatikani na haiathiri wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Waziri wa Biashar na Viwanda:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Spika, naomba kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba hayo ni matangazo ya kila siku hata katika bajeti yetu tumesema, na wafanyabiashara mbali mbali tumo katika harakati za kuwahamasisha wakae, na *ZIPA* ipo njiani kutafuta miradi mbali mbali katika kuhakikisha wafanyabiashara, wawekezaji wanafungua viwanda hapa Zanzibar. Sisi tunafanya kazi yetu ya kuweka mazingira bora, mazingira sahihi ya kuiwezesha Zanzibar iwe ya viwanda. Hilo jukumu tunalifanya na tunaendelea kulifanya na inshaallah naamini wazi miaka kadhaa ijayo itakuwa Zanzibar ya viwanda kama ilivyokuwa zamani.

b) Mhe. Spika, naomba kumjulisha rasmi Mhe. Mwakilishi kwamba kuna maeneo maalum yametengwa ya viwanda Zanzibar kwa kila Wilaya. Kwa mfano, nitakupa Wilaya ya Kati pale Dunga Jeshini kuna eneo kubwa sana ambalo pale ndio itakuwa *industrial park* kwa eneo lile la Wilaya ya Kati. Vile vile Chwaka kama unakwenda Marumbi upande wa mkono wa kulia pana eneo kubwa nalo litakuwa Wilaya ya *Kati Industrial Park* kwa Wilaya ile. Kwa hivyo kuna maeneo maalum tumeyatenga kwa sababu ya viwanda kwa ajili ya kutaka kutekeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi inayotaka Zanzibar ya Viwanda. Mhe. Spika, ahsante.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa miwani yako ipo pahali sio pazuri sana, ipo kikomoni. *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Waziri mwenyewe wa Biashara na Viwanda kwa majibu ya nyongeza.

**Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda:** Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri amejibu vizuri sana maswali yote mawili.

Mhe. Spika, lakini nataka nitoe nyongeza tu ya ziada kuhusu suala zima la wizara yetu kukaa na wafanyabiashara kuwashajihisha kuweka viwanda. Nimeona nisimame niseme wazi na kwa roho safi, tunajitahidi kukaa na wafanyabiashara waliopo hapa Zanzibar na waliopo nje ya Zanzibar, Dar es Salaam na kwengine kuwaomba wafanyabiashara wa Zanzibar waje waweke viwanda. Ni masikitiko yangu makubwa sana Mhe. Spika, na nasema kwa roho safi, maana yake juzi nilikuwa sipo nilisikia mimi. Ningewaomba hao waliomo ndani ya Baraza la Wawakilishi kwanza wakaweka viwanda kwa sababu watu wanasema uanze wewe kucheza ngoma ndio na wengine wanaweza kukufuata.

Bahati nzuri wawekezaji walioko nje wanauliza huko Zanzibar kuna nani ambaye tunaweza kushirikiana naye. Tunawasomea yupo huyu, yuko huyu lakini sio wengi wanaoagiza vyakula sio wengi ambao wameweka viwanda wa Unguja na walioko nje, wanaoagiza nguo sio wengi wanaoweka viwanda, mimi wakati mwengine nawakuta ndani ya ndege nawapa hotuba humo humo ndani ya ndege, acheni njooni muweke viwanda Zanzibar, hawako tayari.
Mhe. Spika, jengine tuna fursa nzuri za vivutio sasa hivi, nzuri sana hazipo popote sehemu hizi. Juzi tumefungua sasa hivi mtandano wa kufanya usajili, mtandao ule umebadilisha utaratibu mzima wa kuweka usajili. Zamani wafanyabiashara wengi walikuwa wanakimbia wanapokuwa wanafungua vitu vyao hawasajili ukweli wa mtaji wao walikuwa wanaficha, wakikwambia mtaji wa shilingi milioni 10 kumbe zaidi ya milioni 10. Tumeondosha hofu ya kujificha sasa hivi wote wanaotoka nje mtandao katika masuala ya viwanda wanalipa milioni 2 tu *registration*. Kwa

hivyo jamani nasema hivi tunajitahidi lakini tuanze sisi wenyewe tuliopo Zanzibar tuwekeze. Kufanya biashara ya mchele, kwenda kununua nguo havisaidii pesa zinakaa nje, wekeni mitaji, kuna siku nilizungumza na mfanyabiashara mmoja nikamwambia kwa nini mnakwenda kuwekeza Dar es Salaam. akanambia kule ndio kwenye manufaa yangu. Hiyo haiwezi kujenga tunajitahidi, tunakaa nao wakati wote.

Mhe. Spika, narejea tena wito wangu wafanyabiashara mliopo Zanzibar acheni peke yake kuagiza vyakula na kuagiza nguo, wekezeni kwenye viwanda, fursa ni nzuri, sasa hivi vivutio vizuri, njooni huu ndio wakati msije mkalaumu wakaja watu wengine wa nje mkaja mkasema nyinyi mnaachwa pembeni.

Mhe. Spika, ahsante sana.

**Nam. 180**

**Utaratibu wa Meli Kufanya Safari Usiku**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub)** - Aliuliza:

Baada ya matukio ya ajali za baharini mara mbili nchi mwetu katika kipindi cha miaka michache iliyopita serikali imepiga marufuku safari za meli nyakati za usiku. Lakini katika siku za hivi karibuni utaratibu huo umerudi kimya kimya kwa meli za abiria na mizigo kufanya safari kisiwani Pemba nyakati za usiku.

(a) Je, kitu gani kimesababisha meli kuanza safari za usiku kwenda Pemba.

(b) Je, serikali imejiridhisha vipi kuwa hali ya usalama imezingatiwa katika safari hizo.

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 180 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kufuatia ajali zilizowahi kutokea nchini mwetu huko nyuma, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukuwa hatua za dharura za kupiga marufuku meli za abiria kusafiri usiku ili kutoa fursa kwa serikali kujipanga vizuri na katika kuimarisha usimamizi wa sekta ya usafiri baharini.

Mhe. Spika, kwa sasa zipo meli tatu zinazofanya kazi ya kusafirisha abiria baina ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, ikiwemo MV. Mapinduzi II, *Sealink I* na *Sealink II*. Katika kipindi cha mwezi wa Disemba, 2017 meli ya MV. Mapinduzi II na *Sealink II* zilipata hitilafu za kiufundi na kupelekea kusimama kufanyakazi kwa muda kwa ajili ya matengenezo. Kutokana na matukio hayo, kulibakia meli moja tu inayosafirisha abiria baina ya Pemba na Unguja jambo ambalo lingeweza kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi wetu.

Kwa nia njema na serikali ya kuwaondolea wananchi usumbufu wa usafiri baina ya Unguja na Pemba, wizara kwa kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini ilifanya mazungumzo na uongozi wa Kampuni ya *Azam Marine* na kuwaomba meli ya *Sealink I* kuongeza safari baina ya Pemba na Unguja ili kupunguza tatizo la usafiri kwa wananchi wetu na serikali ilitoa kibali maalum kwa meli hiyo kusafiri usiku ili kupunguza tatizo la usafiri.

Mhe. Spika, pamoja na kutoa kibali maalum cha meli ya *Sealink I* kusafiri usiku, serikali ilichukua hatua za ziada za kuimarisha usalama kwa wakati wa usiku ili kuhakikisha kuwa meli haipakii abiria zaidi ya kiwango kilichoruhusiwa kisheria.

Mhe. Spika, kwa sasa meli ya MV. *Sealink II* na MV. Mapinduzi II zimeshamaliza matengenezo na MV. *Sealink II* imeshaanza kazi na vile vile MV. Mapinduzi II nayo iko katika hatua za mwisho wa uhakiki na hivi leo ninavyosema watu wa Kampuni ya Lloyd wanafika nchini kuja kujiridhisha na hatimae kuiruhusu ianze kazi.

**Mhe. Ali Suleiman Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Usafirishaji kwa majibu yake mazuri. Pili, nimuulize swali dogo kama ifuatavyo.

Kwa kuwa tulikuwa na matatizo ya meli zetu mbili ambazo moja ni MV. Mapinduzi II na *Sealink* ambazo zilikuwa na matatio lakini zimesharejea katika hali ya kawaida na inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu meli yetu ambayo tegemezi kwa wananchi wetu na nafuu huenda ikamalizika na kupewa ruhusa kufanya kazi.

Kwa kuwa utaratibu mzuri kiusalama uliwekwa wakati wa mchana tu vyombo hivi vitembee, na kwa kuwa meli hizo tatu zitakuwa tayari. Je, utaratibu ule utarudi tena meli zile zitembee mchana badala ya usiku.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:** Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kweli kwamba meli zile zilikuwa zinatembea mchana kwa sababu zilikuwepo. Sasa hivi wakati meli zote tatu zitakapokuwa zinafanya kazi mchana kwa kuwa jambo lile lilikuwa ni la dharura, kwa hiyo hazitotembea usiku na hizo meli tatu zitatosha kupeleka abiria mchana ili kulinda abiria wetu kupata matatizo.

**Nam. 190**

**Bandari Bubu Mkoa wa Kaskazini Pemba**

**Mhe. Omar Seif Abeid –** Aliuliza**:**

Kwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba una bandari bubu 162 kwenye maeneo mbali mbali ambazo miongoni mwao zina maeneo mazuri kwa ajili ya uekezaji na miongoni mwa maeneo hayo wapo wawekezaji ambao wapo tayari kuekeza na Serikali itajipatia mapato, maeneo hayo ni Fundo, Ukunjwi kishukashi, Njao, Gando na Mtambwe kwa Wilaya ya Wete na kuanzia Rasi Kiuyu, Shumba Mjini, Msuka, Makangale, Mkiang'ombe na bandari kuu kwa Wilaya ya Micheweni.

(a) Je, katika maeneo hayo niliyoyataja kuna maeneo mangapi ambayo yapo na bandari bubu ambazo zina mazingira ambayo yanafaa kwa ajili ya uekezaji.

(b) Je, serikali haioni kuwa kukosa kuyatumia maeneo ya bandari bubu kwa ajili ya uekezaji ni moja kati ya mambo yanayotoa fursa kwa watu wabaya kuzitumia bandari hizo.

(c) Je, ni lini serikali italisimamia kikamilifu swala zima la bandari bubu kwa kuwataka na kuwapa vibali wawekezaji ambao wanaomba kuelekeza kwenye maeneo tulioyataja.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 190 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kazi ya kuzibaini kwa majina na idadi bandari zilizopo katika mwambao wa bahari ya Hindi ilifanyika Tanzania nzima kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa walioko katika kanda za Pwani na pia katika kanda za maziwa. Bandari zisizo rasmi au kama alivyoziita Mhe. Mwakilishi mwenyewe bandari bubu katika utaratibu wa serikali hazitambuliki wala haziko kwenye Mamlaka ya bandari ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

(b) Mhe. Spika, bandari zilizoko chini ya mamlaka ni zile tu ambazo zinatambulika rasmi na kwa Zanzibar zipo tano, Unguja mbili na Pemba tatu. Maeneo ya bandari bubu kwa vile sio rasmi si salama kwa uwekezaji, kwani watu wanaofanya magendo mara nyingi huwa wanayatumia. Kwa hiyo, kupendekeza yatumike kwa vitega uchumi isije ikawa ndio njia ya kuyatumia vibaya kwa maana ni vigumu kuyasimamia maeneo hayo.

(c) Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kwamba, suala zima la uwekezaji linasimamiwa na *ZIPA* kwa mujibu wa sheria ya "*Zanzibar Promotion Authority Act*" na ndio waliyopewa maeneo maalum ya uwekezaji. Lakini pia kwa mujibu wa sheria hiyo hiyo *ZIPA* pia wanao uwezo wa kupendekeza eneo lolote la uwekezaji. Pindipo *ZIPA* wakiona maeneo hayo ya bandari bubu yanafaa kwa uwekezaji, watachukua hatua zinazostahiki.

**Mhe. Omar Seif Abeid:**Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri kwa majibu yake lakini kwa kuwa idadi hii ya bandari bubu ambazo tulizitaja sisi au niliziulizia swali nimezipata baada ya risala iliyosomwa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwenye kazi za kamati ilipokwenda kutembelea maeneo hayo. Na kwa kuwa alisema yeye kwenye jibu lake kwamba utambuzi huu unafanywa na wizara yake kwa kushirikiana na Wakuu wa Mikoa kwa ukanda mzima wa bahari ya Hindi.

a) Je, Mhe. Waziri haoni kwamba iko haja sasa ya wizara yake kukaa pamoja na hao Wakuu wa Mikoa wakazihakiki na wakazibaini bandari hizo ili yeye asiwe na hesabu nyengine na ukenda kwa Mkuu wa Mkoa nako ukawa na hesabu nyengine.
b) Je, katika hizo bandari tano alizozitaja kwa Unguja ni ipi na ipi na Pemba ni ipi na ipi. Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**Mhe. Spika, idadi ya bandari nilizozitaja zilifanyiwa uhakiki na watu wanaohusika, na sisi kama wizara na watu wetu walishiriki na ndio maana wakawa na taarifa hii. Lakini kama kuna taarifa tofauti siwezi kusema kwamba haiko sawa na kama amependekeza hivyo basi watu wetu wapo watakwenda kushirikiana na Mkuu wa Mkoa anayehusika ili kwenda kuhakiki. Kwa sababu ni hao hao ndio waliotoa taarifa hizi na sasa ni wao ndio wanaosema kwamba sio sahihi, basi tutakwenda tutahakiki. Kwa sababu kuzijua hakuna ubaya isipokuwa tu kuzitumia ndio tatizo kwa chini ya serikali yetu.

(b) Alitaka kujua ni bandari zipi. Unguja nimesema ziko mbili iko Forodhani na Mkokotoni na Pemba tumesema ziko tatu nazo ni Mkoani, Wete na Kigomasha.

**Nam. 105**

**Uhakiki wa Maeneo ya Uwekezaji**

**Mhe. Omar Seif Abeid** – Aliuliza:

Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali, lakini kabla ya kujibiwa swali langu ningependa nifanye marekebisho kwa ruhusa yako kidogo. Kwa sababu hapa tulitaja Unguja tu lakini ilikuwa dhamiri yangu ni kujua Unguja na Pemba. Kwa hivyo nilitaka nizijue je, katika uhakiki huo ni maeneo mangapi ambayo nayo yamehusika na uwekezaji kwa upande wa Pemba. Baada ya marekebisho yaho naomba swali langu Nam. 105 lijibiwe. ahsante sana.

Kwa kuwa serikali inafanya uhakiki ili kuweza kuyabaini maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji. Na kwa kuwa yapo maeneo ambayo yalishatolewa vibali kwa wawekezaji kwa muda mrefu sasa, na miongoni mwa waliopewa vibali wameshindwa kuyaendeleza, pamoja na kwamba kwenye hati ya ukodishwaji imeelezwa muda ambao wanatakiwa kuwa wameshayaendeleza, lakini bado hadi leo wamezungusha ukuta bila kujenga kitu chochote.

(a) Je, katika uhakiki huo ni maeneo mangapi ya Nungwi, Kiwengwa, Michamvi, Paje kwa upande wa Unguja ambayo yametolewa hati kwa muda mrefu na bado hayajaendelezwa.

(b) Je, ni upi uamuzi wa serikali kwa watu ambao wamezungusha makuta maeneo ambayo wameshindwa kuyaendeleza kwa muda waliopewa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati** – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 105 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, uhakiki wa maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu umeanzia katika Mkoa wa Kaskazini ambapo Nungwi 7, Matemwe 9, Kiwengwa 5, Pwani Mchangani 8 na Mkokotoni 1. Hatua kama hiyo inaendelea kwa Mkoa wa Kusini Unguja ikiwemo Michamvi na Paje, kwa kubaini maeneo ambayo hayajaendelezwa na Makampuni ambayo hayalipi kodi ya ardhi.

(b) Mhe. Spika, serikali inaendelea na zoezi la uhakiki kwa Unguja na Pemba kuyabaini maeneo ambayo hayajaendelezwa ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Maeneo hayo ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyozunguushwa ukuta. Taratibu za kuyarudisha serikalini tayari zimeanza kwa miradi 34. Ahsante sana.

**Mhe. Omar Seif Abeid:** Mhe. Spika, nakushukuru ingawa nilitaka na marekebisho hakunifanyia kwa upande wa Pemba, lakini tuendelee nadhani mara ya pili atakuja kunifanyia marekebisho.

Mhe. Spika, sasa kwa kuwa maeneo haya kayataja na imekuwa ni kilio na kataja kwamba kuna maeneo kwa Unguja kama alivyoyataja na kwa Pemba hakuyataja na dhamiri yetu ni hiyo. Je, kwa yale ambayo yameshaanza kurejeshwa serikalini kuna wawekezaji yeyote ambaye amejitokeza kuyaomba maeneo hayo na nyinyi mukaanza utaratibu wa kuwapatia ili kukidhi ile haja ya kuwa na uwekezaji endelevu. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kwamba katika maelezo yangu nimesema tukimaliza Unguja basi tunaingia Pemba. Kwa hivyo niliwahi kumjibu kama alinifahamu vizuri. Lakini katika yale maeneo ambayo tayari yanarudi serikalini wanapewa wawekezaji wengine ambao wanajitokeza kwa kadri masharti tunavyokuwa tunakubaliana. Ahsante sana.

**Nam. 144**

**Utaratibu wa Wawekezaji wa Kampuni ya Ras-Al-Khaimah Juu ya Utafiti wa Mafuta na Gesi Asilia**

**Mhe. Suleiman Sarahan Said (Kny. Mhe. Simai Moh'd Said)** – Aliuliza:

(a) Je, ni eneo gani la nchi kavu pamoja na baharini walilopewa Kampuni ya Ras Al Khaimah kufanya utafiti wa mafuta na gesi asilia.

(b) Je, mkataba wa kufanya kazi hiyo umefungwa lini na wapi.

(c) Je, endapo patatokea migogoro baina ya kampuni hiyo na SMZ, ni mahakama ipi itatumika katika kutatua migogoro kitu ambacho hutokezea mara nyingi katika sekta hii ya mafuta na gesi asilia.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati** – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Kampuni ya *RAKGAS* kutoka Ras-al-Khaimah imepewa eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na eneo la bahari ndogo linalovizunguka visiwa hivyo (Kitalu cha Pemba – Zanzibar).

(b) Mhe. Spika, kimsingi ili kazi za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ifanyike kwa mujibu wa Sheria, serikali inalazimika kuingia Mkataba na Kampuni *(Petroleum Sharing Agreement – PSA)*. Hata hivyo, hadi sasa hakuna mkataba wowote uliofungwa baina ya serikali na kampuni hiyo, isipokuwa kazi hiyo kwa sasa inafanyika kwa kibali maalum (*conditional permit*).

(c) Mhe. Spika, endapo patatokea migogoro baina ya Kampuni hiyo na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mahakama itakayotumika katika kutatua migogoro hiyo ni Mahakama za Zanzibar kama inavyoelezwa katika Sehemu ya Tisa ya Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar ya mwaka 2016.

**Mhe. Suleiman Sarahan Said:** Mhe. Spika, nashukuru na nishukuru majibu ya Mhe. Naibu Waziri, lakini kama alivyosema kwamba utafutaji huu hauna *sign* unakwenda kwa kibali cha *conditional permit.* Sasa nimuulize kibali hiki ni cha muda gani.

Swali la pili ni kwamba, lini kampuni hii italeta kauli ya uchambuzi wake kuhusu mafuta.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Ni kwamba kibali hiki ni cha muda mpaka watakapomaliza kufanya huu utafiti, kwa sasa wamemaliza Unguja kwenye mtetemo na Mwezi Julai wanaanza kwa upande wa Pemba ambako tunategemea takriban miezi minne au mitano watakuwa wamemaliza na hapo wakimaliza sasa ndio wataleta hizo taarifa. Ahsante sana.

**Mhe. Hamida Abdalla Issa:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuniona na mimi kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwa kuwa suala la mafuta na gesi linasimamiwa na *ZPRA* na juzi tu ndio tumesikia kutangazwa kwa Bodi ya *ZPRA.*

(a) Je, ni utaratibu gani ulitumika kutoa kibali maalumu *(conditional permit)* kabla ya Bodi ya *ZPRA* kutangazwa ili kukidhi matakwa ya kisheria.

(b) Je, wizara kutoa kibali bila ya kupitishwa na Bodi ya *ZPRA* si kwenda kinyume na utaratibu uliopangwa kisheria. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Ni kwamba hakuna utaratibu uliokuwa umekiukwa na ndio maana mpaka sasa hakuna mkataba. Kwa hivyo, mkataba ndio utafanywa kwa kusimamiwa na hii bodi ambayo imetengenezwa. Lakini hatuwezi kukaa shughuli nyengine zisiende kwa sababu tu labda mwenyekiti hajachaguliwa na ukikumbuka kwamba hii tetesi ya mafuta haikuanza jana na juzi ni ya muda na ukizingatia hawa *RAKGAS* hawakuwa wakwanza *just* wamekuja kuvaa viatu vya kampuni ambayo inaitwa *ANTRIM* ambayo ilikubaliana huko zamani na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kipindi kile kabla ya kutengeneza *PRA* yetu Zanzibar na kuwa mafuta tunasimamia wenyewe. Sasa ni muendelezo wa yale ambayo mazuri yalifanywa hapo kabla. Ahsante sana.

**Nam. 214**

**Bohari ya Dawa Pemba na Ukosefu wa Mfamasia**

**Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub)** - Aliuliza:

Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko katika vituo vya afya kuchelewa kupelekewa dawa kutoka Bohari ya Dawa hali inayosababisha wananchi kununua dawa hizo kwa maduka binafsi. Sambamba na hilo kwa upande wa Pemba ni muda mrefu sasa hakuna Mfamasia ndiyo maana hata maduka ya dawa kwa wanaokata Bima hakuna.

(a) Je, wizara inachukuwa hatua gani kurekebisha hali hii inayojitokeza kila wakati.

(b) Ni lini wizara itapeleka Mfamasia Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** – Aliuliza:

Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 214 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba wizara yangu ilipata changamoto ya ucheleweshwaji wa upelekaji wa dawa katika vituo vya afya. Tatizo hili lilitokana na ucheleweshwaji wa dawa kutoka kwa wazabuni kwenda Bohari Kuu ya dawa Zanzibar kutokana na sababu mbali mbali.

Mhe. Spika, sasa naomba nijibu swali (a) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sasa tatizo la ucheleweshwaji wa dawa katika vituo vya afya limeshamalizika na hatutegemei kutokea tena. Kwani katika hatua za kuliondoa tatizo hilo, wizara yangu ilikutana na kufanya mazungumzo na wazabuni wa dawa na kuwataka wahakikishe wanaleta dawa hizo kwa wakati na kwa ukamilifu. Aidha, wizara kupitia Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar inatoa fursa ya maombi ya dharura kwa kituo au hospitali husika pindipo yatatokea mahitaji ya ziada.

(b) Naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba, katika kutatua suala la ukosefu wa wafamasia kule Pemba, wizara yangu tayari imeshaajiri na kupeleka wafamasia wawili (2), kwa ajili ya kusimamia masuala ya dawa na inatarajia kupeleka wafamasia wengine mara tu uajiri wa wafamasia hao utakapofanyika. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Ali Suleiman Ali naona ameridhika. Mhe. Naibu Waziri ahsante, wakati wa maswali umekwisha Waheshimiwa na nina matangazo machache lakini muhimu. Tangazo la mwanzo Waheshimiwa linahusiana na kuundwa kwa Kamati Teule ambalo nitalisoma.

Waheshimiwa Wajumbe wakati wa majadiliano ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 Tarehe 28 Mei, 2018; Mhe. Hamza Hassan Juma alitumia Kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2016, kuliomba Baraza la Wawakilishi kuunda Kamati Teule itakayofanyia kazi suala la Majengo ya Skuli zilizojengwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambayo yanaonekana kukosa ubora, ikiwemo kuvuja kwa baadhi ya majengo hayo katika kipindi kifupi tu baada ya kujengwa kwake. Baada ya hatua hiyo, pamoja na ufafanuzi wa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baada ya mjumbe mtoa hoja kutoridhika na ufafanuzi uliotolewa, Baraza liliamua kuunda Kamati Teule kushughulikia suala hilo.

Kamati Teule iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia hadudirejea zifuatazo:

1. Ni kuchunguza viwango vya ubora wa majengo mapya ya skuli 19 za sekondari Unguja na Pemba;
2. Kuchunguza ushiriki na mawasiliano baina ya Mkandarasi, Mshauri elekezi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika hatua mbali mbali za ujenzi wa skuli mpya 19 za sekondari;
3. Kuchunguza na kupendekeza namna bora ya kuepuka hasara katika ujenzi wa majengo kama hayo na
4. Kuandaa ripoti na mapendekezo kuhusiana na kadhia hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, Wajumbe wa Kamati Teule ya Kuchunguza Majengo Mapya ya Skuli za Sekondari Zanzibar ni kama hivi ifuatavyo:

Wa kwanza kabisa, sio wa kwanza kwa maana ya kuwa ndio mwenyekiti wa hiyo kamati, watajichagua wao wenyewe miongoni mwao watampata mwenyekiti, lakini wa kwanza kabisa ni

mtoa hoja Mhe. Hamza Hassan Juma, Mjumbe wa pili ni Mwalimu, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, Mjumbe wa tatu ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mjumbe wa nne ni Mhe. Mussa Foum Mussa na Mjumbe wa mwisho na wa tano ni Mwalimu, Mhe. Rashid Makame Shamsi. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo hiyo ndio itakayokuwa Kamati Teule kuhusiana na uchunguzi wa kadhia hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe tangazo jengine linahusiana na Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Kabla ya kuzitaja hizo kamati pia naomba nisome maelezo mafupi kama ifuatavyo:

Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kuwa Baraza hili la Tisa lilianza Machi,2016 na hivyo linakaribia kufikia nusu ya muhula wake wa miaka mitano. Kwa mujibu wa Kanuni ya 107(4) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2016 uhai wa kamati hizi tulizoziunda unakaribia mwisho wake. Kwa hivyo, napaswa kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kipindi kilichobakia cha maisha ya Baraza hili.

Kwa msingi huo, nimefanya uteuzi wa Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa utaratibu ufuatao:-

a) Kuwaondoa katika Kamati baadhi ya Wajumbe walioteuliwa kuwa Naibu Mawaziri.

b) Kuwabadilisha Kamati baadhi ya wajumbe ambao ni Wajumbe wa Baraza hili lakini pia ni Wajumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano hasa kwa kamati zenye wajumbe wawili wawili wa aina hiyo.

c) Kuwabadilisha Kamati baadhi ya wajumbe ambao shughuli zao zinaonekana kuwa na mgongano wa maslahi na Kamati wanazozitumikia sasa. Suala hili la mgongano wa maslahi katika shughuli zetu za Baraza na Kamati zake ni jambo la muhimu kuzingatiwa kama lilivyosisitizwa katika Kifungu cha 49 na 50 vya Sheria ya Kinga, Fursa na Uwezo wa Baraza la Wawakilishi na Kifungu cha 3 na 4 cha Jadweli la Pili ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016.

d) Kuwabadilisha kamati baadhi ya wajumbe ambao wamejiendeleza kitaaluma katika fani mbali mbali na hivyo kuwa na sifa za kufanya kazi katika kamati nyengine.

e) Kuwahamisha baadhi ya wajumbe ili kuziwezesha kamati kufanya kazi kwa ushirikiano zaidi (*team work*).

Waheshimiwa Wajumbe, kimsingi sikufanya mabadiliko makubwa katika kamati zilizopo sasa, isipokuwa kwa kuwahamisha wajumbe wachache kwenda kamati nyengine kutokana na sababu ambazo tayari nimeshazitaja hapo juu.

Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nisome majina ya wajumbe na namna walivyogawanywa kwenye kamati hizo na mara tu baada ya kuakhirishwa kwa kikao hichi cha asubuhi, kamati zote zikutane kwa ajili ya kuwachagua Wenyeviti na Makamu

Wenyeviti na nitaomba nipatiwe majina ya viongozi hao wa kamati zote na nitayatangaza majina hayo katika kikao cha jioni au kama jioni hakitakuwepo nitayatangaza katika kikao cha kesho asubuhi.

Ahsanteni sana Waheshimiwa.

Baada ya tangazo hilo Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba kwa heshima na taadhima nitangaze kamati pamoja na wajumbe ambao watakuwa wanazihudumia kamati hizo. Ikumbukwe kwamba, hivi sasa nataja wajumbe tu waliomo kwenye hizo kamati mpaka hapo hao wenyeviti watakapochaguliwa. Kwa hivyo, mtu wa mwanzo katika kila kamati hayupo hapo mwanzo kwa sababu ya umuhimu wake hapana, yupo hapo kama mjumbe tu wa hiyo kamati yenyewe inayohusika. Naomba nianze kamati ya mwanzo kabisa ni Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Wajumbe wa kamati hiyo ni:

**KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Panya Ali Abdalla | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mtumwa Suleiman Makame | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ame Haji Ali | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mussa Ali Mussa | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Talib Enzi Talib | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Karima Abdulwahab Alawy | - | Katibu |

***Wizara husika:***

***i. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi***

***ii. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais***

**KAMATI YA SHERIA, UTAWALA BORA NA IDARA MAALUM**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | - | Mjumbe |
| 2. | Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Maryam Thani Juma | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ali Khamis Bakari (Doholo) | - | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | - | Katibu |
| 9. | Ndg. Ali Alawy Ali | - | Katibu |

***Wizara husika:***

***i. Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora***

***ii. Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ***

**KAMATI YA ARDHI NA MAWASILIANO**

Itakuwa na Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
2. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Mjumbe
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
4. Mhe. Khadija Omar Kibano - Mjumbe
5. Mhe. Hidaya Ali Makame - Mjumbe
6. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
7. Mhe. Said Omar Said - Mjumbe
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
9. Ndg. Mwanaisha Moh'd Kheri - Katibu

**Wizara zinazohusika;**

i. Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati pamoja na
ii. Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji

**KAMATI YA USTAWI WA JAMII**

Itakuwa na Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mjumbe
2. Mhe. Tatu Mohammed Ussi - Mjumbe
3. Mhe. Amina Idd Mabrouk - Mjumbe
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar - Mjumbe
5. Mhe. Nassor Salim Ali - Mjumbe
6. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
7. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu
8. Ndg. Aziza Wazir Kheri - Katibu

**KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (*PAC*)**

Kamati hii itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mjumbe
2. Mhe. Shaib Said Ali - Mjumbe
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
4. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mjumbe
5. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
6. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
7. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil - Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
9. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu

Kamati hii itasimamia wizara zote za SMZ

**KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO**

Kamati hii itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini - Mjumbe
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Mjumbe
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
5. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe
7. Ndg. Said Khamis Ramadhan - Katibu
8. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

Wizara zitakazohusika:

i. Wizara ya Fedha na Mipango
ii. Wizara ya Biashara na Viwanda
iii. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

**KAMATI YA MAENDELEO YA WANAWAKE, HABARI NA UTALII**

Kamati hii itakuwa na Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Seif Abeid - Mjumbe
2. Mhe. Zainab Abdalla Salum - Mjumbe
3. Mhe. Makame Said Juma - Mjumbe
4. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe
6. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Mjumbe
7. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
8. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu
9. Ndg. Mussa Issa Mussa - Katibu

Wizara zitakazohusika na kamati hii ni :-

i. Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale

ii. Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto

iii. Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**KAMATI YA BAJETI**

Wajumbe wa Kamati hii Waheshimiwa ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) - Mjumbe
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Mjumbe
3. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma - Mjumbe
4. Mhe. Simai Mohammed Said - Mjumbe
5. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali - Mjumbe
6. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Mjumbe
7. Mhe. Abdalla Ali Kombo - Mjumbe
8. Ndg. Abdalla Ali Shauri - Katibu
9. Ndg. Kassim Tafana Kassim - Katibu
10. Ndg. Asha Said Mohammed - Katibu
11. Ndg. Shaib Fadhil Shaib - Katibu

Wizara zitakazosimamiwa na Kamati hii ni zote za SMZ zitasimamiwa na Kamati hii.

**KAMATI YA MAADILI NA KINGA ZA WAJUMBE:**

Kamati hii itakuwa na Wajumbe kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
3. Mhe. Shehe Hamad Matar - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini - Mjumbe
5. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Mjumbe
7. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
8. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu

Waheshimiwa Wajumbe kamati ya mwisho. Lakini sio ya mwisho kwa umuhimu ni :-

**KAMATI YA SHERIA NDOGO NDOGO:**

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:-

1. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Mjumbe
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
4. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Said Mohammed - Mjumbe
6. Mhe. Shaib Said Ali - Mjumbe
7. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
8. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu
9. Ndg. Haji Jecha Salum - Katibu

Waheshimiwa Wajumbe hizo ndizo zitakazokuwa kamati zetu za kudumu na nichukuwe nafasi hii kwanza kukupongezeni sana Waheshimiwa Wajumbe wanakamati kwa kamati ambazo zilikuwa kabla ya hizi zinazokuja hivi sasa, mtaona kwamba mabadiliko tuliyoyafanya sio makubwa sana lakini yote hiyo pia inatokana na utendaji uliotukuka na ambao mmeufanya katika vipindi vilivyopita vya kamati. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba sasa ile bidii mlioionesha na ule uzuri wa kazi ambazo mlizifanya zitaweza kuzidi mara dufu ya zile ambazo mlizifanya hapo kabla.

Waheshimiwa Wajumbe pia mtagundua kuwa kuna baadhi ya Wajumbe wameangukia kwenye kamati mbili mbili. Hilo nafikiri lisiwe linakutieni mashaka sana kwa sababu zile kamati nyengine ambazo zimepata watu kwa mara ya pili sio Kamati za Kisekta. Kwa hiyo, kazi zitakwenda kama tunavyozitegemea. Nisisitize tu katika mambo makubwa sana ambayo yalikuwa yakizisumbua kamati zetu katika kazi kipindi kilichopita ni suala la mahudhurio.

Waheshimiwa Wajumbe kazi za Kamati ni kazi za Baraza la Wawakilishi. Unapohudhuria kikao cha Kamati umehudhuria kikao cha Baraza la Wawakilishi umuhimu uko pale pale. Kwa hiyo, tujihimu sana katika kuhudhuria kwenye vikao vya kamati hata kama itakuwa kama iko Pemba wewe uko Pemba lakini uko kwenye kazi ya Baraza la Wawakilishi na mtakumbuka Sheria yetu ya Kinga. Sheria yetu ya Kinga inakupeni kinga hata huko utakapokuwepo *as longer* unafanya shughuli zinazohusiana na Baraza la Wawakilishi.

Baada ya machache hayo Waheshimiwa naomba nikupongezeni sana na baada ya hapo sasa niweze kumwita katibu ili kuangalia shughuli zetu zinazoendelea. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Naomba kutumia Sheria ya Baraza la Wawakilishi Kanuni 42.

Mhe. Spika, naomba kwa idhini yako nitoe taarifa kwa maslahi ya Zanzibar lakini nisingelipenda ijadiliwe wala nisingelipenda kupoteza muda lakini iwe nimeifikisha *message* hiyo ili tupate tamko la serikali. Naomba idhini yako.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa endelea.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, kwanza nashukuru bila ya kupoteza muda. Mhe. Spika, kipindi cha karibuni mfanyabiashara wa Zanzibar ambae alikamatwa na dhahabu hapa Zanzibar Airport na kwa sababu dhahabu haizalishwi Zanzibar. Hilo hatuna pingamizi nalo aliekwa Mazizini alipotoka Mazizini akapelekwa moja Dar es Salaam ambako ndiko kwenye dhahabu hilo halina pingamizi wala halina tatizo.

Lakini Mheshimiwa jana kwa kauli ya Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda karafuu zetu zimekamatwa Tanga magunia kumi halafu Naibu Waziri anasema tunafanya majadiliano eti tunawaomba ndugu zetu wa Tanganyika au Tanzania Bara kujadiliana nao kuzirejesha zile,

wakati dhahabu mfanyabiashara wa Zanzibar nchi kamili na hili halina pingamizi kwa sababu dhahabu si yetu lakini karafuu zetu tunajadiliana kwa kitu gani?. Mhe. Spika, ninachosema hapa tunataka wahusika waje Zanzibar wahukumiwe Zanzibar mara moja.

Naomba kauli ya serikali vyenginevyo tutakuwa tunaogopa siku zote, hii ni nchi hapa tumepitisha Katiba yetu tuna Maraisi wawili ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tena Marais wao wote sawa Rais John Pombe Magufuli na Rais Ali Mohamed Shein tuko sawa ndani ya Muungano.

Mhe. Spika, naomba tamko la serikali kuhusu karafuu zetu kuletwa mara moja bila ya kuwaomba bila ya kujadiliana nao. Ahsante Mhe. Spika. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante Mheshimiwa nafikiri serikali imekusikia Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama kuna chochote.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mheshimiwa nakushukuru kwa kunipa nafasi namshukuru sana ndugu yangu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali aliyetoa hoja hii.

Mhe. Spika, ningependa niseme yafuatayo, Naibu Waziri wa Wizara ya Biashara na Viwanda alichosema anajadiliana na wenzao kwa upande wa Tanzania Bara. Mhe. Spika, suala la kuzungumza na kujadiliana ni utaratibu wa kawaida katika uendeshaji wa serikali na masuala yanayohusiana na shreria ni mambo ambayo yanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria kutokana na tukio lilivyotokea na kutokana na kosa lililotokea.

Kwa hiyo, Mhe. Spika, kuhusu suala la karafuu kwa nini wanajadiliana ni kwamba pia na upande wa Tanzania Bara wanazalisha karafuu. Kwa hiyo, lazima tuwe na vidhibiti vya kutosha vinavyoonesha kwamba karafuu zilizokamatwa pale ni karafuu zinatoka upande wa Zanzibar, mara litakapokubalika hilo hatua na taratibu zitachukuliwa kama ambavyo Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali ameshauri.

Utaratibu wetu ni wa kawaida pale itakapothibiti kuwa karafuu hizo ni za Zanzibar zitarudishwa Zanzibar na watuhumiwa watashitakiwa Zanzibar. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Waheshimiwa kabla hatujaendelea kwenye hoja kabla sijamwita tena katibu nilisahau kutoa tangazo moja.

Kwanza Waheshimiwa maana yake napata vi-*memo* hapa Waheshimiwa wale wabunge waliomo humu ambao tumewachagua kwanza wajielewe wao ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo wana haki na kila kitu ambacho kinatokea hapa. Kwa hiyo, wanaweza hata wakagombea maana yake wengine wameanza kupata wasi wasi labda hawaruhusiwi kwa sababu ya Ubunge walionao. Hapana unaruhusiwa kugombea utakavyoshinda huko baada ya kampeni ni masuala mengine, lakini gombea chochote ambacho una haki ya kugombea kwa hapa.

Baada ya hapo nitoe tangazo dogo kwamba hizi kamati kwa sababu leo leo nimetaka zifanye chaguzi nisome tu mpangilio kama ifuatavyo:-

- Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Kamati ya Ustawi wa Jamii. Pahali ambapo watapatumia kwa uchaguzi wao ni *cafeteria* wote wawili *cafeteria* yetu kubwa nafikiri wataweza kujigawa vizuri halafu wakafanya hizo chaguzi.

- Kamati ya *PAC*. Watatumia Ukumbi wa *VIP II*

- Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo. Watatumia chumba cha Kamati namba 3

- Kamati ya Ardhi na Mawasiliano. Watatumia chumba cha kamati namba 2

- Kamati ya Bajeti. Watatumia Afisi ya Mshauri wa Baraza

- Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii. Watatumia *reading room*.

- Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum: Wao watatumia Ukumbi wetu *conference room*.

Baada ya matangazo hayo Katibu sasa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Shilingi Trilion Moja bilioni Miatatu na Kumi na Tano Milioni Mia Moja na Kumi na Nne na Laki Tatu Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali

*(Kusomwa kwa Mara ya Pili)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wa kikatiba chini ya kifungu 106 kinachomtaka waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya serikali kila mwaka unapoanza.

Kwa heshima kubwa naomba sasa na kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi (1,315,114,300,000) Trilioni moja bilioni mia tatu kumi na tano, milioni mia moja kumi na nne na laki tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni 2019 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kukushukuru kwa dhati wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa ambayo yametuwezesha sisi

Wizara ya Fedha na Mipango kuandaa na kuiwasilisha Bajeti ya Serikali ambayo kwa mwaka huu wa fedha 2018 ilipitishwa na Baraza lako tukufu mwisho baada ya kuchangia Bajeti za Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae na kumalizia na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Pili nawashukuru sana kwa mapenzi yenu kwa serikali na wananchi wa Zanzibar, bila ya nyinyi kukubalia bajeti hii sisi watendaji wa Wizara ya Fedha, Mipango na Serikali kwa ujumla tusingeweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kuidhinishwa kwa bajeti za wizara zote hizo kunapelekea msaada wa makisio na matumizi kutoa uwezo kwa serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali Jumla ya shilingi bilioni mia saba na mbili milioni mia moja na sitini na mbili kutumika kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi bilioni mia sita kumi na mbili milioni mia tisa hamsini na mbili na laki tatu kutumika kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha pia serikali kukopa ndani na nje fedha kwa ajili ya matumizi ya ndani kwa mwaka wa fedha unaoishia tasrehe 30 Juni 2019. Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya kifungu cha 5 kifungu (i) cha mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu 10 kifungu cha kwanza kinazungumzia

(1) Jina fupi
(2) Tafsiri
(3) Utoaji ya Shilingi (1,315,114,300,000) mia tatu kumi na tano milioni mia moja kumi na nne na laki tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.
(4) Makisio ya Fedha zilizokubalika
(5) Kina vifungu vidogo vinne kinazungumzia Uwezo wa kukopa Waziri mwenye dhamana ya Fedha.
(6) Kina vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa waziri katika maombi ya zaida kwa lengo la kukabili matumizi ya dharura pale haja itakapotokezea.
(7) Marejesho ya Mkopo na Riba
(8) Kukubaliwa Mipango ya Maendeleo
(9) Kukubaliwa kwa Fedha zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo
(10) Mfuko wa pamoja wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya mafupi mswada huo naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kuujadili na hatiame kuupitisha mswada huu ili uwe ni sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2018/19. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hoja imetolewa Waheshimiwa imeungwa mkono. Sasa moja kwa moja naomba tuende kwenye majadiliano na naomba nimwite Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwa ajili ya mchango. Kuna jina hapa umeomba kuchangia Mheshimiwa.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, katika mchango huu ambao uliowasilishwa kuhusu kodi ya sheria.

Mhe. Spika, mimi niombe tu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar…

**Mhe. Spika:** Mhe. Mohammedraza Hassannali samahani naambiwa kumbe sio Mswada huu ni ule wa pili ndio utakaochangia ahsante. Naam! Mhe. Hamza Hassan hamia kwenye *microphone* nyengine hiyo, njoo mbele Mhe. Hamza kwenye *podium* hapo.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:**Mhe. Spika, nilikuwa ninataka muongozo wako kwa sababu tumezoea utamaduni Mhe. Waziri akisha kusoma anafuatilia Mwenyekiti wa Kamati. Sasa naona hatujapata ripoti ya kamati waka-*comment* kile ambacho Mhe. Waziri alichokiwasilisha ili na sisi tukaweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri lakini vile vile kuona maoni ya Wajumbe wa Kamati, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Hamza Hassan Juma nilivyofuatilia ni kwamba ule Mswada wa pili kwa sababu iko miwili hii huu nadhani tunaupitisha tu halafu ule wa pili ule ndio anakuja Mwenyekiti wa Kamati ya Bejeti kuja kutowa maelezo na ndio huu ambao sasa utachangiwa na Waheshimiwa Wajumbe. Hii nafikiri tunapitisha tu hapa ni maombi ya fedha, labda nisome Kanuni ni Kanuni ya 100 (3).

Baada ya hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya serikali kukubaliwa Waziri anayehusika atawasilishwa Mswada wa matumizi katika Baraza ambao utapitishwa kwa mujibu wa utaratibu wa kupitisha Miswada isipokuwa hautopelekwa kwenye Kamati ya Kudumu na utasomwa kwa Mara ya Kanza, ya Pili na ya Tatu katika mkutano huo huo kwenye Kanuni ya 100 (3). Mhe. Hamza hivyo ule unaofuata sasa ndio Mwenyekiti ile Hati aliyoiweka mezani ndio atakuja sasa kuisoma, ahsante nafikiri imekaa sawa kwa hivyo naomba tuendelee.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

**Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Shilling Trilioni Moja Bilioni Mia Tatu na Kumi na Tano Milioni Mia Moja Kumi na Nne na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoshia Tarehe 30 June, 2019 na Kuruhusu Utoaji na Uhailishaji wa Fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.**

| | |
|---|---|
| Kifungu cha 1 | Jina Fupi |
| Kifungu cha 2 | Tafsiri |
| Kifungu cha 3 | Utoaji wa Shilingi 1,315,114,300,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali |
| Kifungu cha 4 | Makisio ya Fedha Zilizokubalika |
| Kifungu cha 5 | Uwezo wa Waziri Kukopa |
| Kifungu cha 6 | Uwezo wa Waziri wa Maombi ya Ziada |
| Kifungu cha 7 | Marejesho ya Mkopo na Riba |
| Kifungu cha 8 | |

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8 kimeeleza juu ya mpango wa maendeleo na tunaipongeza serikali kwa kufikisha asilimia 43 ya mambo ya maendeleo. Tungeiomba tu serikali ipeleke pesa hizi kwa wakati pesa za maendeleo ili tuone basi *progress* na bajeti yetu imekubaliwa ipasavyo, ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mohamed Said tunauchukua kama ushauri wa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati iliyopita ya Bajeti tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu cha 8 | Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo |
| Kifungu cha 9 | Kukubaliwa kwa Fedha Zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo |
| Kifungu cha 10 | Mfuko wa Pamoja wa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:**Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria umeupitia mswaada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali bila ya marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liiukubali naomba kutoa haja.

**Mhe. Spika:**Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wale waliokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Waheshimiwa Wajumbe sasa Mswada huo utakuwa umepita rasmi imeshakuwa sheria.(*Makofi*)

## MSWADA WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2018

*(Kusomwa kwa Mara Pili)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena na kuniwezesha mimi kusimama mbele ya Baraza hili tukufu kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2018.

Mhe. Spika, kuwasilishwa kwa Mswada huu kunaashiria kukamilika kwa mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha na kuidhinishwa kwakwe na Baraza lako tukufu. Naomba nikupongeze wewe binafsi Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza kwa jinsi munavyoliongoza Baraza letu hili kwa ufanisi mkubwa.

Namuomba Mwenyezi Mungu mtukufu atuwezeshe kumaliza shughuli zetu hizi kwa mafanikio. Aidha namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohamed said Mohamed pamoja na Makamo wake Mhe. Bahati Khamis Kombo na Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati hiyo kwa uweledi waliouonesha katika kujadili mapendekeo ya Mswada huu na ushauri wao ulipelekea marekebisho kadhaa katika Mswada ninaouwasilisha.

Mhe. Spika, Mswaada wa Sheria ya Fedha kutokana na mapitio ya kila mwaka yanayofanywa na Serikali katika mfumo wake wa kodi pamoja na sheria nyengine zinahusiana na mapato, mapitio

hayo hubainisha maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho kwa kuwekwa vifungu vipya, kuviimarisha vifungu vilivyopo pamoja na kuviundoa vifungu vyenye kasoro katika baadhi ya sheria zetu. Mhe. Spika, Mswada huu unawasilishwa una madhumuni yafuatayo:-

1. Kuimarisha ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya serikali kuwekwa utulivu wa mfumo wa kodi nchini pamoja na kujahisha uwekezaji na ulipaji kodi kwa hiari.

2. Kutoa unafuu kwa walipa kodi kwa kuwaongezea muda wa kuwasilisha *return* pamoja na muda wa kufanya malipo.

3. Kuimarisha udhibiti wa biashara za magendo kwa lengo la kulinda mapato ya serikali.

4. Kuongeza kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa Baraza la Taifa la Biashara na kuwa Katibu wa Baraza.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka 2018/2019 umegawika katika sehemu kuu nane. Sehemu ya kwanza inahusiana na masharti ya utangulizi na pia inajuumisha jina fupi na muda wa kuanza kutumika.

Sehemu ya pili inahusiana na marekebisho mbali mbali ya sheria ya uratibu na usimamizi wa kodi nambari 7 ya mwaka 2009, kwa kufanya yafuatayo:-

i. Kutoa muda ndani ya siku 15 kutoka tarehe ya kuanza biashara kuwa ni muda kwa mlipa kodi kuomba kusajiliwa na Kamishna.
ii. Kuongeza muda wa kuwasilisha *return* kuwa ni ndani au kabla ya siku 20 ya kila mwezi kufuatia mwisho wa kipindi cha kufunga hesabu
iii. Kuweka ulazima ya kumbukumbu kwa njia tofauti za kieletroniki kuweza kuchukuliwa au kuzingatiwa katika ushahidi panapotokezea tatizo.
iv. Kuongeza muda wa kulipa kodi inayostahiki kulipwa kuwa ni ndani au kabla ya siku 20 ya kila mwezi kufuatia mwisho wa kipindi cha kufunga hesabu na pia kutoa nafasi kwa muda mwengine uliotajwa ndani ya sheria nyengine husika kuweza kutumika.
v. Kumruhusu mlipa kodi kuuomba kwa Kamishna kwa maandishi kuongezewa muda wa kulipa muda wa kulipa kado chini ya Sheria ya Kodi na kuweka utaratibu wa kufuatwa na Kashmina wakati atakapopokea maombi ya kuongezewa muda.
vi. Kumtaka Waziri katika kutumia uwezo wake wa kusemehe kodi yote au sehemu ya kodi inayostahiki kulipwa iwe ni kwa kushauriana Kamishna *commissioner* na kutangazwa katika gazeti rasmi.

Mhe. Spika, sehemu ya tatu inajuuisha marekebisho ya sheria ya ushuru wa stempu nambari 7 ya mwaka 2017.

i) Kwa kumpa uwezo waziri kusamehe ushuru wote ambao unastahiki kulipwa chini ya sheria husika baada ya kuwepo sababu za msingi za maslahi ya umma kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa katika kanuni zitakazotungwa chini ya sheria hii na kutangwaza katika gazeti rasmi.

ii) Kutoa msamaha wa ushuru wakati wa uhaulishaji wa mali isiyohamishika ikijumisha ardhi na majengo bila ya kuwepo na malipo pale mali hizo zinapohusihwa kwa utaratibu wa urithi au hakiba baina ya mzazi au mlezi kisheria na mtoto.
iii) Kutoa msamaha wa kutolipa ushuru kwa mradi wowote uliodhinishwa chini ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar iwapo msahama huo umetolewa chini ya sheria hiyo.
iv) Kutoa msamaha wa kutolipa ushuru kwa mashirika ya ndege yanayouza tiketi za safari za kimataifa.

Mhe. Spika, sehemu ya nne inahusiana na marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi nambari 1 ya mwaka 2006 ambayo inatambua mfumo usio rasmi kufuatwa katika utaratibu unaokubaliwa mbele ya Bodi na Baraza.

Sehemu ya tano ni marekebisho ya Sheria ya Kutoza Kodi ya Mafuta Nambari 7 ya mwaka 2001 ambayo inafuta kifungu cha 5 cha sheria hiyo.

Sehemu ya sita ni marekebisho ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Vitega Uchumi Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2004 ambayo inaelekeza kwamba utaratibu wa msamaha wa kodi ya ardhi unatolewa na waziri chini ya sheria hii uwe kwa mujibu wa jadweli la kwanza la sheria hiyo.

Sehemu ya saba Mhe. Spika, ni marekebisho ya Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nambari 1 ya mwaka 2003 kwa kufanya yafuatayo:-

i) Kuweka tafsiri ya maneno magendo, ofisa na baharia katika kifungu cha 2.
ii) Kuongeza sehemu mpya ya pili (a) inayohusiana na uwezo wa KMKM wa kuzuia magendo
iii) Kuongeza vifungu vipya 25(a) na 25(b) vinavyohusiana na makosa ya magendo
iv) Kurekebisha kifungu cha 31 kinachohusiana na zawadi kwa maofisa na watu wanaosaidia kupelekea kukamatwa kwa washtukiwa wa makosa ya magendo.

Mhe. Spika, sehemu ya nane ni marekebisho ya Sheria ya Baraza la Biashara Nambari 10 ya mwaka 2017 kwa kurekebisha kifungu cha 15 kwa kuongeza jukumu kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi wa Baraza hilo kuwa Katibu wa Baraza.

Mhe. Spika, baada ya maelezo haya naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuujadili na hatimae kuupitisha Mswada huu ili uwe Sheria ya Fedha ya mwaka 2018.

Mhe. Spika naomba kutoa haja.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mhe. Waziri na imeungwa mkono. Sasa naomba kwa heshima na taadhima nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili aweze kuja kuwasilisha, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.(*Makofi*)

**Mhe Shehe Hamad Matar (**Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti) **:**Ahsante Mhe. Spika kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti naomba kuwasilisha hutuba ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na maoni ya Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha na baadhi ya Sheria za Fedha za Kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhabiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusina na hayo.

Mhe. Spika,ni wajibu wetu kutanguliza shukurani kwa Mwenyezi Mungu, Mtukufu kwa neema zisizo na idadi anazotujaalia na pia kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kama tulivyojipangia**.** Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, pamoja na wasaidizi wako Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Wenyeviti wa Baraza, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa hekma na umahiri mkubwa unaouoneshwa katika kuliongoza Baraza letu.

Mhe. Spika, umoja na ushirikiano mzuri wa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti umeisaidia sana Kamati katika kukamilisha jukumu la kuupitia na kuuchambua Mswada huu. Hivyo, kwa dhati kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano waliouonesha wakati tukipitia Mswada huu. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mohamed Said Mohamed — Mwenyekiti
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo — Mjumbe
4. Mhe: Zulfa Mmaka Omar — Mjumbe
5. Mhe. Asha Abdalla Mussa — Mjumbe
6. Mhe. Shehe Hamad Mattar — Mjumbe
7. Mhe. Simai Mohammed Said — Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati makatibu wa Kamati ya Bajeti, kwa msaada wanaoipatia Kamati, nao naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo;

1. Ndg. Abdalla Ali Shauri — Katibu
2. Ndg. Asha Said Mohamed — Katibu
3. Ndg. Kassim Tafana Kassim — Katibu

**UCHAMBUZI WA MSWADA**

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kufanya mabadiliko katika baadhi ya Sheria zinazohusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya Serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo, ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa Sheria hizo.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwasilisha Mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu ambapo bila ya shaka utasaidia kuongeza ufanisi na udhibiti mzuri wa mapato pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi na biashara inayotokea duniani. Mhe. Spika, miongoni mwa Sheria zinazofanyiwa marekebisho na Mswada huu ni Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya 2003 ili kukipa uwezo zaidi kikosi cha KMKM katika kupambana na magendo ambayo yanachangia katika kupunguza ufanisi wa ukusanyaji mapato ya Serikali.

Mhe. Spika, kimsingi kamati inaunga mkono na inapongeza juhudi hizo. Hata hivyo, kamati inapata hofu juu ya ufanisi wa udhibiti wa magendo, kwa kuwa bado kuna changamoto ya udhibiti wa magendo ya ndani ya nchi ambayo bado hayajawekewa mikakati imara katika kuyadhibiti. Hivyo, ni imani ya kamati kuwa marekebisho haya ambayo kimsingi yatawapa uwezo na nguvu zaidi maafisa wanaohusika na kuzuia magendo, yatafanikisha udhibiti wa magendo ya aina zote na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, kama ilivyokuwa kwa bajeti ya mwaka 2017/2018, kwa mara nyengine tena serikali haikusudii kuongeza kodi yoyote mpya kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019. Kamati inaipongeza serikali kwa dhati juu ya hatua hiyo ambayo kimsingi ina dhamira ya kuwapunguzia mzigo wa maisha wananchi. Hata hivyo, kamati inapenda kuikumbusha serikali kuwa, hatua hiyo ya kutoongeza kodi inapaswa kwenda sambamba na juhudi za usimamizi wa mapato kwa kupunguza mianya ya uvujaji wa mapato na kuwezesha kufikiwa malengo yaliyokadiriwa kutokana na vyanzo vya mapato vilivyopo.

## MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA MSWADA

Mhe. Spika, kamati iliupitia mswada huu na kufanya marekebisho mbali mbali, katika vifungu tofauti, baadhi ya marekebisho ya msingi yaliyofanywa na kamati ni pamoja na kifungu cha kifungu cha 20 cha mswada kinachorekebisha Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam.1 ya 2003, ambapo kamati ilipendekeza kufutwa maneno “cha miaka saba” yaliyopo mwisho wa kifungu cha 4A(2)(d) na kuweka badala yake maneno “kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano”.

Mhe. Spika, kamati imependekeza marekebisho hayo kwa kuzingatia uzito wa kosa na mazingira ya kosa hilo lilivyoweza kufanyika.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yaliyofanywa ni marekebisho ya kisarufi ambapo baadhi ya vifungu vimerekebishwa ili kuvifanya visomeke vizuri na vilete maana iliyokusudiwa. Marekebisho mengine ni kuweka usawa wa maneno baina ya Mswada wa Kiswahili na Mswada wa Kiingereza ili miswada hii iendane na kuleta maana halisi iliyokusudiwa.

Mhe. Spika, kamati pia imependekeza kufuta baadhi ya maneno ambayo yanaonekana hayaleti maana yoyote katika vifungu hivyo na kufanya marekebisho yanayotokana na makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana usahihi wa maneno hayo.

Mhe. Spika, kwa ufafanuzi zaidi wa marekebisho ya mswada huu, naomba Waheshimiwa Wajumbe wapitie waraka wa kamati waliopatiwa ambao unaonesha mapendekezo yote ya marekebisho ya mswada ambayo kamati imeyapendekeza.

### Hitimisho

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nikushukuru tena kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya kamati kuhusu mswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa

utulivu na umakini wakati nikiwasilisha maoni ya kamati. Pia naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati wakichangia bajeti ya serikali ambayo bila ya shaka itaweka msingi mzuri kwa Kamati ya Bajeti ijayo kuhusu maeneo ya kuyafanyia kazi, kwani kumalizika kwa bajeti hii, ndio mwanzo wa matayarisho ya bajeti ijayo.

Mhe. Spika, nawaomba wajumbe wauchangie na hatimae kuupitisha mswada huu, kwa lengo la kuipa fursa serikali kuanza kutekeleza bajeti ya mwaka 2018/2019. Aidha, napenda kutoa wito kwa serikali kusimamia vyema mapato yatakayokusanywa na matumizi yake ili ufanisi wa bajeti hii upatikane kama inavyotarajiwa.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Mohammedraza Hassanali.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** *(hapa sehemu kidogo tu haikusikika sauti)*.

....kwa ushauri na angalizo kwa Wizara ya Fedha na Mipango, *ZRB* pamoja na *TRA* kwamba kumekuwa na mifano mingi Mhe. Spika katika ukusanyaji wa kodi lakini uvujaji wa kodi. Mhe. Spika, nina mfano mmoja mzuri. Miaka minne iliyopita *Venta* walikuwa wategа uchumi ambao wamejenga makuti, haingii sauti eeh! Mhe. Spika, naomba dharura wameniambia haisikiki sauti.

**Mhe. Spika:** Unaweza kuhamia *microphone* nyengine tu Mhe. Mjumbe. Endelea Mhe. Mjumbe.

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kwa sababu ilikuwa *Hansard* haijaingia na nikupongeze uamuzi wako.

Vile vile Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na hii Kamati ambayo iko chini ya Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa iliwasilishwa kwa ufasaha na kwa usikivu kabisa. Mhe. Spika, mimi naunga mkono marekebisho haya ya Sheria ya Kodi kwa asilimia mia moja. Lakini Mhe. Spika, naomba kutoa angalizo kwa Wizara ya Fedha na Mipango chini ya *TRA* na *ZRB*, bado naona suala la ukusanyaji wa kodi, tuna haja bado kodi zipo na tunaomba tuwatumie wafanyabiashara na sisi sote tuwe waadilifu wa kulipa kodi.

Mhe. Spika, kipindi cha miaka minne ushahidi ninao, kulikuwa na wategа uchumi ndugu zetu wa Kitaliana pale *Venta* na waliweka vitega uchumi na matokeo yake walikuwa wanadaiwa karibu *over 3 billions* na *TRA Income tax* na sehemu nyengine za *ZRB*. Lakini Mhe. Spika, ushahidi ninao siku ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mzee wetu Balozi Seif Ali Iddi alipoitisha kikao cha pamoja Ofisini kwake pale Shangani, *this four years ago* ili kuona kwamba wale Wataliana wategа uchumi walikuwa wameshapata harufu ya kutaka kukamatwa, basi Mhe. Spika siku ile baada ya Makamu wa Rais Balozi Seif Ali Iddi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, alipoitisha Kikao mmoja ambaye ni Kamishna Mstaafu ambaye amemaliza huko nyuma leo sisi yeye, alikwenda akawavalisha mabuibui wale kuwatorosha uwanja wa ndege. Matokeo yake Mhe. Spika, serikali imekula hasara, wale wananchi wanyonge ambao walipeleka matunda pale

ya ku-*supply*, keroti, muhogo na vyengine ikawa kesi iko Mahakamani. Kwa hivyo matokeo yake Mhe. Spika, serikali imebidi ifidie gharama zile za kwenda Mahakamani kufuta kesi.

Sasa Mhe. Spika, mimi sioni sababu kama wategа uchumi wawe Wazanzibari au wawe kutoka nje, sioni sababu ya wafanyabiashara kutolipa ambapo inafikia mabilioni unajiuliza kuna nini. Kwa hivyo nataka nitoe tu angalizo kwa *ZRB, TRA* na Wizara ya Fedha na Mipango, kwamba jambo kama hili litakuwa linatuumiza. Matokeo yake wale wameondoka wamejenga makuti, pesa wamepata na wananchi ndio walioumia.

Lakini isitoshe hivi karibuni Mhe. Spika, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar alikwenda na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed, walikwenda kwenye kiwanja cha mpira na walitoa kauli pale kusema hivi, kwamba yule mtega uchumi kakopa benki wananchi wanadai pale na ule mradi haupo. Matokeo yake Mhe. Spika, kama kakopa benki ina maana ile benki ya wananchi. Kwa hivyo ni lazima tuwe waangalifu sana katika masuala kama haya, kwa sababu utakuta serikali ina nia nzuri lakini lazima tuwe waangalifu katika masuala kama haya. Hatuwezi kumuacha mtu anaendelea amekwenda kukopa benki, anadaiwa na wakulima pesa hajatoa hayupo wala hatujamsikia kama kapanda karantinga ya kupelekwa Mahakamani katiwa ndani, siku nyengine na huyo atakuwa kakimbizwa.

Sasa Mhe. Spika, mimi naiomba sana serikali kwamba hili suala uwe na hoja maalum, lakini unaacha kodi bilioni moja, bilioni mbili au milioni 500, halafu unamwambia kwamba aah! lipa kidogo kidogo. Ni lazima kuwe na hoja maalum na serikali ieleweke. Mimi niombe sana suala la kodi lisiwe mjadala, umefanya biashara lipa kodi, una *assets* tuone *assets* zako, ndio ni lazima uwe na *surrender* za *assets*. Lakini unadaiwa bilioni mbili unaweza nyumba yako ya bilioni 200, *we are the loser, there are not the loser*. Kwa hivyo Mhe. Spika, niiombe sana Wizara ya Fedha na Mipango najua kuna watendaji Alhamdulillah. Ukitaka kumchinja nyani usimtizame uso wake.

Mhe. Spika, jengine katika suala hili la kodi. Mhe. Spika, humu ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya wananchi wetu tulikuwa tunapiga sana vita vya unga *cocaine* sote humu kila siku. Lakini leo baadhi ya wafanyabiashara au baadhi ya wananchi, sio kila anayepepesuka ni mlevi, utamkuta mtu ana nyumba ya kifahari, ana gari yenye thamani ya zaidi ya dola milioni 100, hana leseni, hana *tin number* na wala hana chochote unajiuliza *this is money laundering* au pesa za *cocaine*. Maana yake Mhe. Spika, ni lazima tuwe wakweli, wananchi wetu wa Unguja na Pemba na Tanzania kwa ujumla tunazidi kuwaumiza. Tunakwenda kumkamata dagaa kibua lakini papa yuko wapi mpaka leo aliyekwenda kupelekwa kwenye karandinga. Kwa hivyo Mhe. Spika, katika kuzidisha kodi *ZRB* na *TRA* na sehemu nyengine watizame *recitation* za magari. Halafu watu waulize hiyo ndio nchi kote duniani. Bwana wee! wewe una gari yako milioni 200, huna *tin number* una nyumba mbili, hatuna tatizo la kuwanyang'anya hatuko huko kwa Mwenyezi Mungu, basi tulipe asilimia 20 ya kodi au tuoneshe vipi hii gari umeweza kuipanda ya milioni 200.

Mhe. Spika, hii nchi ni yetu sote na lazima tuone kwamba tunaweka kwenye utawala ubora. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naomba kuwepo na taratibu, vyenginevyo tutakuwa na *money laundering* humu Zanzibar, tutakuwa na *cocaine* wananchi wetu wataumia na sisi sote tutakuwa tunapiga kelele, kazi yetu serikali itakuwa tukawajengee tutumie mamilioni ya pesa tuwajengee

wale walioathirika na *cocaine* halafu ni sifa hiyo. Kwa nini iwe ni sifa, unamwambia yule papa kwamba lete tu *cocaine* sisi serikali tutajenga majengo mengi Unguja na Pemba ya kuwaelimisha hawa wavuta *cocaine,* tuwe wakweli kwa Mwenyezi Mungu Mhe. Spika. Mhe. Spika, mimi niombe sana kwamba hili ni suala letu na ni janga la taifa. Sio Zanzibar, sio ulimwengu, sio Tanzania. Jana Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa anasikitika siku ya *cocaine* Mkoa wa Iringa umekuwa ni janga la vijana wavuta *cocaine,* kuanzia miaka 15 mpaka miaka 35, Waziri Mkuu jana kwenye *ITV*.

Mhe. Spika, ninachoomba kwamba hili suala la kodi bado tusukume, wananchi tuwaelimishe na wafanyabiashara tubadilike akina Raza. Lakini tuwe na muongozo, lakini leo mtu mfanyabiashara hana *tin number*, hana leseni wala hana chochote ana makontena mia analeta hujui pesa zile za *laundering*, wala hujui pesa hizi kama za *cocaine*, halafu wanamuona hatuna tatizo tuwaulize tusije tukafika hapa tukazongwa na hii Zanzibar Mhe. Spika, kesho kutwa hapa tutakuja kuingiliwa na silaha, ikiwa vitu kama hivi vipi na tume ngapi zipo hapa zimeundwa zimekwenda wapi. Kwa hivyo, lazima tuwe na uangalifu. Mhe. Spika, mimi natoa angalizo tu kwa taasisi hizi zifanye usajili, zitizame na hayo ma-*go down* yatizamwe yanafanya biashara gani na mara nyingi sasa hivi kumekuwa na mtindo sisi wafanyabiashara kuhamisha mizigo usiku siku za *week end*, utakuta *week end* ndio inaondoshwa mizigo, *where is the reason.*Kwa hivyo, Mhe. Spika, niwapongeze sana *ZRB* na niwapongeze sana *TRA* na Kamati nzima, lakini na sisi lazima tuwe waangalifu, tusipokuwa waangalifu tutakuja kuumizana, tutakuwa siku zote hapa tunazidisha bajeti, wanaita *sober* ya kuwajengea hawa. Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja, nashukuru sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Raza, anayefuata Mhe. Hamza Hassan Juma na ajiandae Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mhe. Hamza Hassan karibu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kutia nyama tu katika Mswada huu aliouleta Mhe. Waziri. Kimsingi sina tatizo na Mswada huu naunga mkono kwa asilimia mia moja na kwa sababu mswada huu umekuja tu kuweka sheria ili yale ambayo tuliyoyapitisha yaweze kupata nguvu za kisheria.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ili nisipoteze muda sana niende tu moja kwa moja katika vifungu. Mhe. Spika, kwa kweli kitu ambacho ninakipongeza ni kuwa kila siku tunasema kwamba Mhe. Waziri wetu wa Fedha na Mipango ni msikivu sana, kwa sababu kwa kweli hapa katikati kidogo wafanyabiashara walikuwa wakitulalamikia sana kuhusu ile *harassment* iliyokuwa inafanyika hasa katika suala zima la ulipaji wa kodi, na hata ule muda waliowekewa kurejesha zile *return.* Kwa kweli baada ya malalamiko na sisi malalamiko yale tukayawasilisha serikalini kwa kupitia kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa kweli tunamshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kufanya marekebisho haya, kwa kuongeza muda wa kuongeza zile *return*, lakini vile vile kuwa na muda wa *negotiation*. Hapa katikati mpaka lugha zilikuwa zinabadilika, wengine walikuwa wakisema sasa hivi *ZRB* wameshakuwa wababe, kwa kweli ilikuwa hali sio nzuri. Sasa hivi tunamshukuru sana Mhe. Waziri baada ya kusikia kile kilio chetu ametusikiliza na ameweza kufanya haya marekebisho.

Mhe. Spika, chengie ninachotaka kusema hapa katika kifungu cha 8 ambacho ni marekebisho ya kifungu cha 57, anasema kwamba;

Kifungu cha 8

> "Waziri anaweza kushauriana na Kamishna kwa ajili ya kusamehe kodi au sehemu yoyote ya kodi kwa ajili ya kuilipa ile kodi yenyewe".

Mhe. Spika, katika suala hili kitu ambacho nakiomba ni kwamba viongozi wetu mara nyingi wawe waadilifu na kwa bahati nzuri sasa hivi kuna Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wetu ni mwadilifu sana na ni mtu ambaye hana ubabaishaji wala kizungumkuti. Lakini kimsingi kwa kweli katika eneo ambalo serikali mara nyingi, serikali zetu za kiafrika huwa zinakosa mapato sana hapa katika hii misamaha ya kodi. Kwa hivyo, kitu ninachokiomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri aendelee na moyo huo huo ili tuhakikishe kwamba serikali yetu ile kodi inayosamehewa iwe inawarudia wananchi. Mara nyingi hapa kodi ambazo zinasamehewa ni zile ambazo zinawagusa moja kwa moja kupata unafuu kwa wananchi au kuongeza *investment* katika nchi.

Mhe. Spika, nije katika suala zima la uhaulishaji wa majengo. Mhe. Spika, moja katika jambo ambalo lilikuwa linawafanya watu wafanye mambo kiholela na kinyume cha sheria, katika masuala mazima ya kurithisha mirathi pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, kwa sababu watu walikuwa wanaogopa zile ada au kodi ambazo zilikuwa zinalipishwa, kwa hivyo, utakuta watu wanarithishana kinyemela nyemela bila hati zozote. Lakini kwa kuondoa hizi kodi au hizi ada kwa kweli itaweza sana kutusaidia kwa wananchi wetu kuridi katika kufuata sheria za nchi.

Kwa haraka Mhe. Spika, nilikuwa nakuja kwenye hiki kifungu cha 15 ambacho kinazungumzia kuhusu suala la hizi sheria za *ZIPA*. Mhe. Spika, hapa nilikuwa nataka niongeze ili Mhe. Waziri aje atusaidie tu maelezo, kwa sababu kulikuwa kuna malalamiko kwa kiasi fulani kwa wawekezaji wa *Penny Royal* ambao walipewa ardhi na serikali, lakini kuna baadhi ya kodi ambazo walikuwa wanaziomba kwa muda mrefu zilikuwa kama kikwazo katika kuendesha ule mradi wao. Lakini hivi karibuni tulipotembelea kule Matemwe kwenye ile kadhia ya hoteli tulikwenda pale tukaona kidogo zile harakati angalau zinaendelea, kwa hivyo inawezekana yale mambo Mhe. Waziri ameshayarekebisha au kama bado au kama kuna vikwazo vyengine kwasababu kulikuwa kuna tatizo la baina ya Sheria ya Ardhi na Sheria ya Uwekezaji ya *ZIPA* kupitia Wizara ya Fedha. Sasa nafikiri hili wakitusaidia vile vile na sisi tutapata kujua ni nini ambacho kinachoendelea hasa kwa sababu ukiangalia uwekezaji ule wa *Penny Royal* uwekezaji mkubwa ambao tunategemea utasaidia sana kuongeza idadi ya watalii lakini vile vile kuongeza ajira, lakini vile vile kuongeza pato la Taifa.

Mhe. Spika, nakuja haraka haraka katika sehemu ya Mswada wa Sheria kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo. Mhe. Spika, mimi kwa kweli hapa naendelea sana kuipongeza serikali kwamba tunajaribu kuangalia kila ambapo tunahisi kuna mianya ya ukosefu wa fedha, kuna mianya mengine kwa kweli serikali inatunga sheria nzuri. Sasa kitu ambacho hapa ninachokiomba. Mhe. Spika, KMKM hawa kwa kweli tunawapa majukumu makubwa sana na ni wajibu wao kwa sababu wale ni sawa sawa kusema ni askari na ndio maana

wakabidhiwa na silaha. Lakini sasa katika kupambana na masuala haya ya magendo basi ni vizuri tukaweza kuwaboreshea vile vifaa vyao, wakawana *radio calls,* kwa sababu mpaka sasa hivi *KMKM* wanatumia zaidi simu za mkononi.

Mhe. Spika, katika kupambana na magendo inatakiwa kila katika *point k*uanzia *point* moja, kuanzia *A,B,C* mpaka *Z,* kila kinachozungumzwa na wenzake wanakisikia. Sasa kwa kutumia siku za mkononi hatuwezi tukapambana na magendo. Kwa sababu leo unapomkamata hapa anakimbilia sehemu nyengine au anatoa taarifa sehemu nyengine. Lakini tukiweza kutumia *radio call,* tutaweza kudhibiti hata rushwa itaondoka kwa sababu lazima tuzungumze pamoja na kwamba askari wanadhamana na kila kitu, lakini pesa ni pesa, pesa mtihani wakati mwengine wanahongwa na wanaachia watu na magendo. Lakini kama watatumia *radio call* suala la magendo, suala la rushwa litaweza kuondoka lakini katika sehemu hii inayofuata inayozungumzia suala la uzuiaji wa magendo.

Mhe. Spika, Sheria ya Ukamataji Magendo mimi nafikiri hii moja kwa moja ihusishwe na uhujumu wa uchumi, kwa sababu magendo ya aina yoyote ni sawa sawa na kuiibia serikali, ina maana unapoiibia serikali unawaibia wananchi mapato ambayo mapato yale yangesaidi kwenda kutoa huduma kwa wananchi. Mhe. Spika, mimi nadhani kwamba ni vizuri suala la magendo tukalihusisha moja kwa moja na uhujumu wa uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, hapa imeelezwa vizuri katika kifungu cha 25 kwamba mpaka vile vyombo ambavyo vitakavyohusika basi katika kusafirisha magendo hayo vyombo hivi vitataifishwa. Sasa mimi nilikuwa na omba tu Mhe. Spika, elimu itolewe kwa sisi wengine ni wamiliki wa magari tunamiliki vyombo mbali mbali, lakini magari yale wewe unamkabidhi dereva na dereva anafanya shughuli zake. Sasa kwa kweli anakuja mtu unaweza ukaja ukamsikia kwamba amepata kiinua mgongo, amenunua gari, gari ile imsaidie katika kumuendeshea maisha yake yaliyobakia, matokezeo yake yule dereva ambaye aliyempa sio mwaminifu, akenda kupakia magendo akaja akaambiwa gari yako imekamatwa na magendo imetaifishwa hapo hapo *pressure* na kufa. Kwa hivyo nafikiri hapa ni elimu inatakiwa ile kutolewa kubwa sana hasa kwa wale ambao wanaomiliki vyombo vya magari, lakini vile vile vya baharini kwa sababu mtu ambaye anayepeleka magendo sio mwenye chombo mara nyingi, mwenye chombo anakuwa mtu mwengine na anayesafirisha magendo ni mtu mwengine.

Mhe. Spika, lakini vile vile bado kuna tatizo la mafuta ya petroli na *diesel* kuuzwa katika vidumu au katika vigeleni. Hili Mhe. Spika kwa kweli namuomba Mhe Waziri tunaona jitihada *ZRB* wanavyohangaika na hawa lakini kwa kweli hili suala tutafika pahala tulikomeshe, kwa sababu kuuza mafuta katika vidumu nje ya vituo ambavyo vimepewa leseni na serikali wakati wowote inaweza ikasababisha hata maafa ya moto na mambo mengine.

Mhe. Spika, lakini la mwisho kabisa nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu jana alivyokuwa akifanya majumuisho ya Mswada ule wa bajeti kuu ya Serikali alieleza kwamba anakusudia kuondoa ile nafuu hasa katika wale ambao waingizaji wa vyakula katika unga na sukari na tulijaribu kutoa *concerning* zetu sana kuhusu kwamba kumuomba Mhe. Waziri unafuu ule uendelee kuwepo ili kuweza kusaidia kuzuwia uongezekaji wa bei. Mhe. Spika, na tuliwahi kuzungumza wazi wazi kwamba tulikuwa hatuna tatizo sana na uwekezaji wa Kiwanda cha

Sukari kwa sababu ile mali ghafi ni miwa ambayo inayolimwa hapa Zanzibar na wanaofaidika zaidi ni wakulima wetu, lakini vile vile tunategemea pengine baadae wanaweza wakanunua miwa kwa wakulima wengine wa miwa.

Mhe. Spika, Lakini bado tunarudi katika suala la kulinda Kiwanda cha Unga wa Ngano, kitu ambacho tunachojua serikali tayari imeshatoa *favour* kwa kulinda kiwanda hichi kwa kusamehe ushuru wa ngano nzima inayoingia. Mhe. Spika, ngano nzima inayoingia haiingii kwa makontena, inaingia kwa *bulk,* inaingia meli nzima. Sasa ile tu peke yake ile *bulk* ya ngano kuingia nchini bila ya kulipia kodi, ina maana pale tayari kiwanda kile serikali imeshakilinda. Sasa leo unapokwenda kuwaondolea ile nafuu ambayo sasa hivi wanalipa karibu asilimia 10 ya ushuru ambao Mhe Waziri jana aliufafanua. Kwa kweli hapa akiondoa ile nafuu kwa sababu huko nyuma ilikuwepo hii nafuu na ikaongezwa ikatoka asilimia 10 ikenda mpaka asilimia 25. Matokezeo yake kiwanda hichi hichi au mwekezaji huyu huyu akaja akaongeza bei ya ngano karibu shs.15,000 kwa kila packet moja. Kwa hivyo kuna baadhi ya biashara ambao miongoni mwao mmoja yumo humu humu ndani Mhe. Raza alikuwa akileta ngano ndani ya Zanzibar, Batash alikuwa akileta ngano ndani ya Zanzibar, lakini baada ya kupandishwa ule ushuru kutoka asilimia 10 mpaka 15, matokeo yake wakashindwa na yule ambaye aliyepewa unafuu ili kulindwa akaweza kuongeza bei ikawa tafrani.

Mhe. Spika, lakini serikali hii tunashukuru wafanyabiashara baada ya malalamiko Mhe. Rais kipindi kile aliwahi kuwaita na baada ya kuzungumza nao akasema aah! kutokana na hali hii kwali bei ya chakula, bei hasa ya mkate, kwa sababu unapopandisha ngano utaongeza bei ya mkate, utaongeza bei ya andazi, utaongeza bei ya chapati, utaongeza bei ya mambo mbali ambayo yanayotumia ngano. Mhe. Spika, kwa hivyo bado mimi nilikuwa naomba nafikiri tuendelee kustahamili kwanza tusubiri kwanza, kwa sababu kwanza bajeti hii ya serikali safari hii tumeambiwa hakuna kodi yoyote ambayo itakayoongezeka, lakini ile nafuu iliyokuweko kwa wafanyabiashara wanaoingiza biashara ile ya chakula hasa unga ngano, ikiondolewa ina maana ni sawa sawa na kama imekuwa kumeongezwa kodi.

Mhe. Spika, Kwa hivyo kwa kweli suala hili bado nilikuwa namuomba Mhe. Waziri na hata humu sikuona eneo lolote ambalo linazungumzia ni asilimia ngapi ile nafuu itaandoka katika Mswada huu sijaiona. Sasa sijui kama itakuja kufanywa hivyo, itakuja kuwa katika *percentage* gani.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa kweli nakushukuru sana lakini vile vile kama nilivyosema nampongeza sana Mhe. Waziri na naomba basi Mwenyezi Mungu atupe afya na nguvu ili hii Shilingi Trilioni 1.3 *plus* alioiomba Mhe. Waziri kukusudia kukushanya mwaka huu aweze kuipata yote na ziada ya ili tuweze kufanya mambo mengine ya maendeleo.

Mhe. Spika, Ahsante sana nakushukuru.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Naomba sasa nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi.

**Mhe. Rashid Makame Shamsi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuichangia au kuchangia Mswada huu wa sheria hii ambayo itajulikana kama Sheria ya Kutoa Kodi na Kubadilisha Baadhi ya sheria za fedha na Kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali.

Mhe. Spika, kwa kweli Mswada huu unaendana na wakati na nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kuliona hilo lakini vile vile nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya Bajeti kwa ripoti yao na mapendekezo waliyatoa yahusianayo na Mswada huu. Niwapongeze pia ndugu zangu waliotangulia ndugu wajumbe kwa michango yao katika kuu-*support* Mswada huu.

Mhe. Spika, mimi nikiingia katika huu Mswada naomba niende katika ukurasa wa 33 sehemu ya 6 kifungu cha 16 (b), nilikuwa napendekeza neno "*proviso"* liwekwe katika *invited coma,* kwa sababu ni neno geni, si watu wengi wanalolifahamu labda watu wa Sheria na wengi hapa hatuna taaluma ya sheria.

Mhe. Spika, lakini vile vile katika ukurasa wa 36 Katika ukurasa wa 36 kwenye kifungu 25 (a) makosa yanayohusiana na magendo. Mhe. Spika, kwanza nipongeze juu ya marekebisho haya ya kifungu kwa sababu hapo nyuma suala hili kidogo lilikuwa na utata. Kwa hivyo kwa kuwepo kifungu ambacho kinaweka wazi makosa ya yanauohusiana na mtu atakayeshiriki katika suala zima la magendo. Nafikiri utata huo sasa utaondoka kwa sababu unamhusisha mtenda kosa mwenyewe, lakini hata yule ambaye amesaidia katika kutenda kosa, lakini pamoja na vyombo ambavyo vitakuwa vimeshiriki katika suala zima la kuchukua au kubeba magendo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, katika kwenye kifungu cha 25(a)(c), katika maelezo ambayo yameelezwa imetajwa bidhaa. Ninapenda ninukuu, "Gari yoyote, chombo cha usafiri baharini, ndege au kitu chengine chochote kilichotumika kwa kusafirisha watu hao wanyama, bidhaa, vitu au bidhaa nyengine vitataifishwa", *statement* inaendelea. Ninachotaka kuhoji tu ni kwamba kifungu cha (d) vile vile kimetaja bidhaa. Sasa inaoneka kama *repetition* au ni marudio kutoka kifungu cha (c) halafu tunaona tena kifungu cha (d), *otherwise* tupate maelezo ya nyongeza kwa nini kikawepo kifungu cha (d) kwamba bidhaa yoyote inayohusiana na kosa la magendo itataifishwa, wakati tumeona tayari kwenye kifungu cha (c) bidhaa imetajwa karibu mara mbili.

Mhe Spika, nije kwenye kiungu cha 25(b) ambapo inauzungumzia juu ya anayesaidia katika kuchangia. Mhe. Spika, maelezo ni mazuri sana kwamba hata yule ambaye atakuwa anashiriki au anachangia katika muhusika kutenda kosa la magendo vile vile hatua za kisheria zitafuata. Mhe. Spika, katika watu ambao wanahusika baadhi ya wakati kuchangia basi ni katika vyombo hivi vya usalama. Kuna baadhi ya askari ambao sio waaminifu wakati mwengine hawa hawa ndio wanaowapa chochoro au njia za wafanya magendo kuweza kutekeleza maovu yao. Sasa ningependa sana katika suala hili basi kusiwe na mzaha kama itabainika kama kuna askari ambao wanachangia hili basi na wao wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria hii.(*Makofi*)

Mhe. Spika, unaweza ukashangaa gari ambalo limepakia mafuta ya kupikia pengine matenki au mageloni 100 mpaka 300 linafikaje katika kisiwa cha Uzi, limepita wapi, limepita katika vituo mbali mbali pengine limepita Fuoni, likapita kituo cha Polisi cha Unguja Ukuu, lakini mafuta yale mwisho yanafika bandarini Uzi, utaweza kushangaa au yanakamatwa mafuta ya kupikia ya

kupikia Kizimkazi na yametokea mjini, yamepita vituo vingapi. Maana yake kuna watu lazima katika vyombo hivi vya usalama watakuwa wamehusika kwa njia moja au nyengine katika kuona kwamba magendo yale yanafika katika ile sehemu ambayo inataka kusafirishwa. Mhe. Spika, kwa hivyo Sheria hii ni nzuri na kipengele hichi kitawagusa hata wale askari ambao wanachangia kwa njia moja au nyengine katika kuona kwamba wahalifu wanatekeleza masuala haya.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Kikosi cha KMKM ni moja katika kikosi muhimu sana katika nchi yetu na sio katika masuala ya magendo, lakini KMKM wanasaidia hata ulinzi na usalama wa visiwa vyetu. Kwa hivyo nichukue fursa hii kwanza kuweza kuupongeza sana uongozi wa kikosi hichi na serikali kwa ujumla kwa kuona umuhimu wa kuwepo kwa kikosi hichi. Lakini tunawapongeza hata utoaji wa huduma, ukienda pale Hospitali ya Kibweni kwa kweli wanasaidia sana jamii, seuze hii kazi ya kuzuwia magendo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kazi ya kuzuwia magendo ni kazi ya hatari sana kwa sababu yule ambaye unamzuwia magendo hayo maana yake anauwezo naye kuhatarisha maisha yako wakati wowote. Kwa hivyo wenzetu wanafanya kazi ngumu, wanafanyakazi ya hatari. Sheria hii kwa kufikiria suala hili la zawadi kwa kweli mimi naipongeza sana serikali kwa sababu wenzetu wanahitaji kupewa moyo, wanahitaji kupewa motisha na hii itasaidia vile vile kutoshawishika na rushwa pale ambapo wanakamata magendo yale.

Mhe. Spika, lakini niiombe serikali kutokana na kazi hii hatarishi ambayo wanayoifanya wenzetu basi ni vyema vile vile kuwapatia Bima za maisha yao, kwa sababu hii ni kazi ya hatari na ni kazi ambayo ni ya kujitolea zaidi. Kikosi hichi kimeokoa fedha nyingi hususan katika kukamata magendo mbali mbali yakiwemo ya karafuu, fedha nyingi sana zimeokolewa lakini vile vile kimeweza kuokoa mali ambazo zimeibiwa, pengine aliyeibiwa ni mtu, kwa hivyo mali imekamatwa. Sasa kazi zao ni kubwa hata hii zawadi ambayo wanapewa basi iwe ina uwiano na thamani ya ile mali ya magendo ambayo wameikamata.*(Makofi)*

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la utata sana wenzetu juu ya vyombo ambavyo vinakamatwa. Vyombo vingi aidha vilikuwa vinakaa mpaka vinaharibika ambayo inakuwa ni hasara au wakati mwengine vyombo hivi vinakamatwa lakini baadae wanarejeshewa wenye vyombo vile. Sasa kutokana na marekebisho na uwepo wa sheria hii, hivi sasa kutakuwa kuna uwazi juu ya vyombo ambavyo vinakamtwa na kama vitakuwa vinafilisiwa maana yake serikali itakuwa ina uwezo wa kupiga mnada na mwengine kuingiza pato katika taifa letu.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi baada ya hayo niseme tu kwamba utaratibu na usimamizi wa kodi hivi sasa vile vile unaonekana kwamba utakuwa na urafiki kati ya mlipa kodi na chombo kinachohusika na ukusanyaji wa kodi. Hii ni faraja kubwa sana, ni faraja kwasabu suala la ulipaji wa kodi likiwa lina urafiki baina ya mlipa kodi na chombo kinachohusika, nafikiri watu wengi wanaweza kujitolea hata bila ya matatizo yoyote kuweza kutoa kodi katika biashara zao au katika kazi mbali mbali wanazozifanya zinazostahiki kulipa kodi serikalini.

Mhe. Spika, baada ya hayo nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia Muswada huu ambao ni muhimu sana katika suala zima la kuongeza pato katika uchumi wa nchi yetu.

Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

**Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini:** Nashukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi kwa dakika chache nilizioomba na mimi nichangie Mswada huu wa Mhe. Waziri wa Sheria za Kutoza Kodi na kubadilisha baadhi ya sheria za fedha na kodi kuhusiana na ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya serikali na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Nampongeza sana Mhe.Waziri na Serikali kwa ujumla kwa Mswada huu muhimu kwa sababu siku zote kuweka sheria ni jambo moja, lakini kuona utekelezaji wake na ufanisi wake ndiyo suala la msingi sana na unapoona sheria haitekelezeki au kuna vikwazo basi ni vyema kurekebisha haraka sana, hasa kuona kwamba kanuni zinatekelezwa au kama hazipo zinawekwa.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na mchango mdogo sana katika sehemu ya saba kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Namba 1 ya 2003, nipo kwenye sehemu ya 2(a) uzuiaji wa magendo. Mhe. Spika, na mimi niungane na walionitangulia suala zima la kikosi chetu hiki cha kuzuia magendo kazi kubwa na nzuri wanayofanya na hasa lazima tuwapongeze kwa kufanikisha kazi kubwa ya udhibiti wa magendo katika msimu huu uliopita wa karafuu. Mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kweli yametokana na vikosi vyetu vya SMZ lakini *notably* ndugu zetu wa KMKM. Sasa Mhe. Spika, kifungu ninachotaka kukizungumzia ni kifungu cha 4(a)(2). Katika kutumia uwezo wa mamlaka yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha kwanza afisa au baharia wakati akiwa kazini anaweza kuingia kufanya doria na kuingia bila vikwazo, dodooo hayo.

Mhe. Spika, sasa kubwa nataka kusisitiza kwamba afisa au baharia wakati anataka kufanya kazi zake au anafanya kazi zake, maafisa mara nyingi sana tunawaona wana beji pale ya kitambulisho na jina lake na *uniform* kamili na wanapendeza kabisa. Lakini mara nyingi kwa mabaharia wetu hasa walioko vijijini huwa hawavai *uniform* na wanakuwa katika nguo zao za kawaida. Sasa ile inatoa mwanya kwa watu wengine nao kujifanya maafisa wa KMKM au askari wa KMKM kwenda ku-*harass* watu na hata kufanya wao magendo juu ya magendo au kupitisha magendo.

Sasa ombi langu Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri mwenye dhamana wa vikosi kuhakikisha kwamba maafisa wetu, mimi nawasifu maafisa wengi wako *very smart*, utamuona afisa wa KMKM ana jina lake na nambari ya kitambulisho, lakini askari wetu wengi wa KMKM walioko vijijini tunajua bandari ziliopo. Leo nilimsikia Mhe. Omar Seif Abeid akitaja bandari za Pemba zile zilizoko kule vichochoroni nyingi mno, kwa sababu mle kote tunashukuru vikosi vyetu vipo lakini askari mara nyingi kule utawakuta hawapo katika *uniform*, wapo katika nguo za kawaida. Sasa inapotokea kesi kama hizi wao wajanja wanajifanya na wao askari, kwa hivyo wanayapitisha magendo. Ningemuomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri tusimamie suala la vitambulisho kwa askari wetu hasa wa KMKM waliopo kule vijijini.

Mhe. Spika, *item* ya pili na ya mwisho ni kifungu cha 22 katika mswada huo huo, kifungu hiki kinarekebisha au ni marekebisho ya kifungu cha 31, anasema kifungu cha 21 cha sheria hii kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha pili na kuongeza mara tu baada ya G. Lakini namba H zawadi zinazowezekana kupewa kwa maafisa au watu waliosaidia katika kufanikisha ukamataji wa mtu yeyote aliyetuhumiwa kufanya kosa la magendo.

Mhe. Spika, uzoefu na *practice* ambayo tumeisikia kwa wale mabaharia wengi wanalalamika kwamba wao ndiyo wanaofanya kazi ya kukamata magendo, wao wanajitosa baharini lakini wanapokamata magendo wakiyaleta huku, ile Sheria ile ya ugawaji, *fine* KMKM wanapata fungu lao, lakini lile fungu la KMKM wanaofaidika ni maafisa, wale mabaharia hawafaidiki. Kwa hivyo malalamiko yanakuwa makubwa aah! tumekamata mzigo bwana gunia za karafuu 300 lakini tulichopewa ni hiki hapa. Sasa hawaridhiki matokeo yake wanasema bwana basi sisi tutagawana huko huko. Sasa matokeo yake na wao wanaingia kwenye magendo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ningeomba sana kwamba wale wanayotenda ile kazi watizamwe kwa jicho la huruma, wao wapatiwe *the line share* ya ile zawadi. Hatukatai pana amri za kiaskari pale kwamba afisa, bosi lazima yeye apate kile kitu kikubwa *fine* apewe lakini yule aliefanya kazi aliyejitoa muhanga, kazungumza Mhe. Rashid vizuri sana hapa kwamba yule aliyejitoa muhanga maana yake mwenye magendo kajizatiti, sasa unapokwenda kumkamata anajua na yeye roho yake anaiweka rehani. Naomba sana Mheshimiwa ile *the line share* ya ile zawadi wafikiriwe kupatiwa wale. Kama si hivyo kama nilivyosema kule kule baharini wakiwakamata, wale wengine nao wakishaona hivi tukirudi huku hatuna chetu wanawaambia mtatupa kiasi gani, kule kule wanapatana, sisemi kwamba ndio kawaida lakini tunazipata hizo stori Unguja na Pemba ni ndogo tunayapata hayo mambo. Sasa Mhe. Spika, niongeomba sana nasisitiza sana suala la kuzawadiwa ipasavyo, wale askari ni jambo la msingi na lisimamiwe ipasavyo, vyenginevyo na wao tutawafanya wale vijana waingie kwenye magendo.

Mhe. Spika, sina zaidi naunga mkono hoja zote hizi na namtakia kheri Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini. Waheshimiwa Wajumbe sasa kabla sijamwita mtoa hoja naomba nimwite Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Amina Salum Ali.

**Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:** Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii niseme wazi kwamba naunga mkono marekebisho katika Mswada huu wote uliofanywa na yaliyowekwa wazi hapa na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Mimi Mhe. Spika, ningependa kujikita zaidi katika sehemu ya saba inayozungumzia marekebisho ya Sheria ya Kikosi Maluum cha Kuzuia Magendo.

Mhe. Spika, ningependa kuchukua nafasi hii kusema kwamba marekebisho haya muhimu sana na kwa kweli wakati umefika kufanya marekebisho kukipa nguvu zaidi kikosi hiki cha KMKM, kwa sababu ndiyo kikosi maalum kilichoundwa na serikali yetu kusimamia masuala yote ya magendo nchini. Mhe. Spika, wakati ule kikosi hiki kinaundwa ilionekana hatari ya kuigeuza

Zanzibar kuwa ni kisiwa cha magendo. Mimi ningependa kuwakumbusha wale vijana kama wamewahi kuona sehemu inayoitwa "*pirate of the Caribbean"* na wakati ule hao wenye magendo hawa walikuwa wamefurutu ada, ndiyo maana kikosi hiki kikaundwa na wanaitwa maharamia kwa lugha ya Kiingereza *pirate,* maana yake maharamia.

Mhe. Spika, kwa sababu Zanzibar ni kisiwa na kisiwa cha biashara si vyema tukaweza kugeuza kikawa kisiwa cha magendo, kule nchi za nje kuna visiwa vidogo vidogo vinaitwa majina kwa mujibu wa wale makapteni wa hizi meli hizi boti hizi zinazopeleka magendo, basi vile visiwa vimegawanya majina kwa mfano Tumbatu kinaitwa cha mtu fulani ambaye ni mmoja ya mwenye magendo mkubwa na kadhalika na kadhalika. Tunashukuru kwamba Zanzibar hatujafikia hali hiyo lakini magendo Mhe. Spika, yapo.

Mhe. Spika, ningeanza kuzungumzia kwanza tafsiri ya kifungu namba 18 cha tafsiri ya magendo kimeeleza wazi wazi na Wajumbe wamesoma, kwa sababu maana yake kulikuwa na wasi wasi watu walikuwa hawaelewi maana ya magendo lakini tafsiri hii imewekwa wazi kabisa, maeneo ya magendo tukachofanya, kitu gani cha magendo yote na marufuku yaliyokuwepo yameelezwa hapa.

Mhe. Spika, mimi nina uzoefu wa magendo ya karafuu. Magendo ya karafuu miaka ya nyuma huko yalituhangaisha sana na serikali ikachukua hatua mbali mbali kuhakikisha kwamba magendo ya karafuu yanapigwa marufuku na yanaondoshwa. Mwaka jana Sheria ya Karafuu ilibadilishwa na ikawekwa kali kabisa na yenye nguvu zaidi na ndiyo maana ukaona humu kuna vifungu vinafanana. Mimi niseme tu kwa uwazi kwamba Sheria ile kwa kweli imetuwekea urahisi sana katika suala zima la magendo na ndiyo maana magendo ya karafuu mwaka huu yakawa yamepungua kwa hatua kubwa sana. Kesi zimekuwa kidogo sana za magendo ya karafuu. Kwa hivyo marekebisho haya nayaunga mkono na ningeomba Wajumbe wote wayaunge mkono kwa sababu ndiyo yenye manufaa kwa nchi yetu.(*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini kumezuka magendo ya vyakula na bidhaa nyingine, hii ni kwa sababu wanajaribu watu kukwepa kodi. Kama kipindi cha mwezi mmoja huu au mwezi mmoja na nusu kesi nyingi nimezisikia za magendo ya mafuta ya kupikia na mafuta ya kula kwa binaadamu, kumeonekana mafuta yakichuliwa kupelekwa visiwani, kwa hivyo magendo ya vyakula yapo na bidhaa nyingine yapo. Hivyo ningewaomba wafanyabiashara ambao wanashughulikia mambo haya ya magendo kwa kweli wayaache kwa sheria hii itawakamata.(*Makofi*)

Mhe Spika, pia kwa sheria hii hata yule mtu anayehusika na shauri, anashirikishwa, anakuwa na yeye anatoa mbinu atakuwa kwenye makosa na sheria hii itamuhukumu, kama ilivyo Sheria ya Karafuu watu wakaogopa. Sheria ya Karafuu ilikwenda mbali kwamba chombo kama cha serikali au cha nani viongozi na wanaohusika yote waliambiwa watakuwa kwenye hatia wakaogopa watu wakaacha. Na haya magendo mengine ya sheria hii itawabana watu ambao wengine watakuwa wanajua au hawatojua. Kwa hivyo nawaomba jambo hili waliache sheria hii ni kali na itawahukumu.

Mhe. Spika, jengine katika sheria hii imeeleza mambo mengine ya magendo ya ziada humu na kutaifisha kwa chombo ikiwa ndege au nini vyombo vitataifishwa humu. Nyuma huko ilikuwa

sheria hii haikusema, kama ilivyokuwa kwa karafuu wale waliokuwa na jahazi zao miaka hii mwaka jana walikuwa na hadhari sana hawakuruhusu sana vyombo vyao kutumiwa na vyombo vingi vyao viliwekwa juu ya ardhi havikuwekwa baharini. Kwa hivyo Sheria hii ya KMKM itawafanya watu wengi mjigeuze mjibadilishe na muwe na hadhari kujua vyombo vyenu kama gari au nini mnavyowapa watu wenu wa kufanya biashara, muwachunguze muwajue kwamba hawashiriki kwenye magendo.

Mhe. Spika, nataka nitoe hadhari sana kwa wenzetu hawa wafanyabiashara kama nilivyosema pale mwanzo wawe na hadhari, ningewaomba tu wafanyabiashara kwa kweli wakaja tukazungumza na sisi wizarani kwetu na Wizara ya Fedha tukaona njia gani ya kuwawezesha kufanyabiashara iliyokuwa halali na wakaweza kupata mapato yao. Biashara ya magendo ni biashara ambayo haina tija na waiache kwa sababu itawasababishia matatizo ya kukwepa kodi na kutusababishia kugombana na wenzetu, kwa sababu inaonekana kwamba sisi huku Zanzibar ndiyo kisiwa ambacho kinachosababisha watu kuwa wanafanyabiashara hii ya magendo.

Mhe. Spika, nije katika marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara la Zanzibar Namba 10 ya 2017. Ukiangalia swada huu tuliokuwa nao umeishia nambari 22. Kwa hivyo mimi ningeomba nitoe mapendekezo kwamba marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar kuongeza vifungu 23 na kifungu nambari 24 ambacho kitasema kwamba, "Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi atakuwa Mwenyekiti wa Kamati za Uongozi na Katibu wa Baraza la Biashara".

Mhe. Spika, Baraza la Biashara ni jambo la mwisho kabisa kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wafanyabiashara, ndiyo eneo ambalo linawaweka pamoja wafanyabiashara na serikali. Kwa hivyo wafanyabiashara mambo yao, manung'uniko yao, changamoto zao wanatakiwa wazieleze pale. Na kwa upande wa serikali tunataka mapendekezo yetu, rai zetu na ushauri kwa wafanyabiashara na mikakati mipya ya biashara inatolewa pale kwenye Baraza la Biashara. Kwa hivyo tulipobadilisha Sheria ya Baraza la Biashara nambari 10 ya 2017, kuna mambo tumetakiwa tuanze kuyafanya. Naomba niseme la kwanza ambalo tunalotakiwa tulifanye ni kuanzisha Mabaraza ya Mikoa. Naomba niwajulisheni hapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba Mabaraza ya Biashara ya Mikoa yameshaanzishwa Mikoa yote mitano ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Mikoa ya Pemba wameshaanza kufanya mikutano yao ya Mabaraza ya Biashara. Mikoa ya Zanzibar na Mabaraza ya Biashara nina hakika kati ya mwezi huu watamaliza kufanya kazi. Ninachowaomba Waheshimiwa Wajumbe tukimaliza Kikao hiki cha Baraza letu la Wawakilishi kuna mambo yalizungumzwa humu kuhusu wafanyabiashara na yanayohusu mambo ya biashara ningewashauri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliopo hapa, hatua ya mwanzo ya wao kujua mambo ya biashara ni kwenye Mabaraza ya Biashara ya Mikoa, waende wakazungumze watoe ushauri wakae na wafanyabiashara katika mikoa yao ili kuwe na uwezo na nguvu za kuwapa uwezo wa kuwapa uwezo wafanyabiashara wadogo wadogo waliomo ndani ya mikoa ili na wao waweze kukua kuwa wafanyabiashara wakubwa.

Mhe. Spika, la mwisho kuhusu Baraza la Biashara kwamba hatua zinazofuata sasa hivi kwa kifungu hiki tu na vyengine ambavyo vinatakiwa vitekelezwe hatua itayofuata hivi karibuni,

kikao cha kwanza cha Baraza la Biashara kwa mujibu wa Sheria hii mpya Namba 10 ya 2017. Ombi langu wafanyabiashara tujiangalie tulikotoka, tuangalie hapa tulipo, tuangalie na sera zetu za uchumi na sera zetu za mikakati za viwanda tuone kwa kiasi gani tunaweza kuchukua nafasi na kuangalia fursa nyingi zilizokuja baada ya marekebisho yaliyofanywa na serikali kupitia Wizara ya Fedha na Wizara yetu kuona kwamba biashara Zanzibar inakua na uwekezaji katika viwanda Zanzibar vile vile unakua.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme naunga mkono marekebisho ya Mswada huu asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara. Sasa Waheshimiwa Wajumbe naomba kwa heshima na taadhima nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi ili aje akamilishe hoja yake.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima na kutuwezesha kuwepo leo katika Baraza hili kujadili miswada muhimu sana ya sheria zinzohusiana na matumiz ya fedha lakini kwa sasa tunahusiana na masuala ya ukusanyaji wa kodi na papato ya serikali.

Mhe. Spika, baada ya kumsukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu naomba nitoe shukurani kwako kwa mara nyingine tena, kwa kuweza kuendesha mjadala huu katika Braza hili leo hii. Lakini pia niishukuru sana Kamati ya Bajeti chini ya uongozi wake Mhe. Mohamed Said Mohamed, nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi yake kwa ujumla kwa mashirikiano makubwa katika kuandaa Mswada huu wa Sheria. Lakini pia niwashukuru Mawaziri tuliohusika hasa Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda na Mhe. Waziri Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.(*Makofi*)

Mhe. Spika, marekebisho ya sheria zinazofanywa zote zinahusiana na masuala ya kodi na mapato ya serikali. Kwa hivyo nawashukuru sana kwa michango yao lakini pia nimshukuru zaidi Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda kwa kutoa ufafanuzi hasa katika marekebisho ambayo tunakusudia kuyafanya katika Sheria ya Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mswada huu umechagiwa na Waheshimiwa Wajumbe saba, Waheshimiwa Wajumbe sita wamechangia moja kwa moja lakini mmoja amechangia kwa maandishi na naomba niwataje. Wa kwanza ni Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Jimbo la Mgononi ambae alitoa maoni ya kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohammed Said Mohammed. Wa pili ni Mhe. Mohammed Raza Mwakilishi wa jimbo la Uzini na wa tatu ni Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa jimbo la Shaurimoyo, wa nne Mhe. Rashid Makame Shamsi Mwakilishi wa jimbo la Magomeni, wa tano ni Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini Mwakilishi wa Jimbo la Dimani na wa sita ni Mhe. Balozi Amina Salim Ali Waziri wa Biashara na Viwanda. Aliyechangia kwa maandishi ni Mhe. Harusi Said Suleiman Mwakilishi wa Jimbo la Wete lakini pia ni Naibu Waziri wa Afya.

Nawashukuru wote kwa michango yao na maoni waliyoyatoa nitayachukua hasa katika usimamizi wa utekelezaji wa sheria hii, Sheria ya Fedha ya 2018. Mhe. Shehe Hamad Mattar

alitoa maoni ya kamati na niseme tu kuwa maoni yao yote waliyoyatoa ya kamati tumeyazingatia kazi hii tumeifanya pamoja. Kwa hivyo yale tumeyakubali na tumeyapokea na tumeyakubali na tumeyapokea kama ni marekebisho katika Mswada wa sheria hii.

Mhe. Mohammed Raza alizungumzia umuhimu wa wawekezaji lakini vile vile wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla. Kwanza kuelewa umuhimu wa kulipa kodi, hilo ni jambo ambalo Serikali mara zote inalisisitiza na tunatoa taaluma hasa kwa wananchi lakini pia wawekezaji na wafanyabiashara wote kujua kwanza umuhimu wa kulipa kodi. Lakini pili wakubali sasa kulipa kodi kwa hiyari na bila ya shuruti na tunakuwepo na fo*rum* kama Serikali na walipa kodi, wawekezaji na wafanyabiashara, pale wanapoona kuna mambo ambayo yanawakwaza basi ni vizuri tuyazungumze katika mijadala ile katika mashauriano, lakini sio kutumia mbinu za kukwepa kulipa kodi. Kwa sababu hapa tunaumiza uchumi wetu tunajiumiza na sisi wenyewe.

Mhe. Spika, kwa hivyo nakubaliana na ushauri wake kwamba wawekezaji ambao wanakwepa kulipa kodi tuwadhibiti, lakini wafanyabiashara pia wanaokwepa kulipa kodi nao wadhibitiwe, lakini na wananchi waelimike sasa kujua umuhimu wa kulipa kodi, wanaotakiwa kulipa risiti wakati wanaponunua huduma au bidhaa basi wafanye hivyo. Lakini zipo njia nyingi ambazo tunazifanya Mhe. Spika, kuhakikisha kuwa tunaimarisha makusanyo ya serikali na moja kuweka mifumo bora zaidi na tunataka kuweka mifumo ya kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya *EFD.*

Lakini vile vile sheria hii sasa inaweka utaratibu mzuri zaidi wa kudhibiti magendo kwa ajili ya kuongeza mapato ya Serikali na kupunguza mianya ya upotevu wa mapato haya ya Serikali, lakini jengine tunawajenga tunaweka utaratibu mzuri zaidi wa kudhibiti misamaha ya kodi inayotolewa. Kuna taratibu ambazo tumeziweka na tumeshazitolea maelezo kuweka muongozo sasa katika masuala mazima ya kodi ya zuio, lakini kuimarisha kazi za ufuatiliaji na ukaguzi na kubainisha vyanzo vipya vya mapato.

Kwa upande wake Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia suala la *harassment,* alisema kwamba huko nyuma *ZRB* ilikuwa inawa-*harass* walipa kodi. Kama nilivyosema jana na naomba nirudie kwamba *ZRB* haina dhamira wala nia ya kuwa-*harass* walipa kodi, walipa kodi na *ZRB* ni watu lazima wanahitaji kufanya kazi kwa pamoja kwa maelewano na taratibu zote zipo za kisheria za majadiliano na wale wafanyabiashara ambao hawaridhiki na utaratibu wa kodi wanazotozwa basi pia kuna utaratibu wa kisheria wa kupeleka malalamiko yao. Kwa hivyo hakuna sababu ya yeyote ama awe mlipa kodi, ama anayedai kodi kutumia ubavu

kwa sababu taratibu za kisheria zipo na inabidi zifuatwe, tutazidi kuelimishana na watendaji wetu ndani ya *ZRB, TRA* lakini vile vile na wananchi pia na wale walipa kodi kwa ujumla wao basi wajue kwamba kuna umuhimu wa kulipa kodi bila ya kushurutishwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma alizungumzia suala la kifungu cha 8 marekebisho ya kifungu cha 57 cha sheria mama hasa katika masuala ya misamaha, alisema kwamba ukimpata Waziri ambaye anatoa tu misamaha bila ya utaratibu tunaweza tukapoteza mapato ya serikali. Mhe. Spika, nimuhakikishie kwamba upo utaratibu wa kisheria na utaratibu huo ambao unawekwa ndani ya Mswada huu wa Sheria ndio unaweka udhibiti zaidi, kwamba Waziri hawezi kutoa msamaha mpaka ashauriane na Kamishna wa Mapato, ipo hapa ipo wazi katika udhibiti na kuondoa hofu aliyokuwa nayo Mhe. Hamza. Lakini hata sasa utaratibu uliopo kwamba Waziri anapata ushauri katika kusamehe kodi za serikali kupitia Kamati ambayo ipo *ZRB.* Kwa hivyo huo utaratibu upo na upo utaratibu pia wa baadhi ya kodi kusamehewa na mwenyewe Kamishna. Kwa mfano riba ingawaje ni mapato ya serikali lakini utaratibu upo kwamba Kamishna mwenyewe anaweza kusamehe, lakini anaweza kusamehe kwa asilimia hamsini kwa sababu haya ni mapato ya serikali.

Lakini kwa adhabu (*penalty),* Kamishna anaweza kusamehe *hundred percent* kwa sababu kwenye adhabu haya ni masuala ya ki-*administration,* mtu kachelewa kuleta *returns* hayahusiani hasa na kodi ya serikali. Kwa hivyo anaweza kusamehe kwa *hundred percent* na Waziri anaweza kusamehe *principle amount*, anaweza kusamehe riba, anaweza kusamehe *penalty*, lakini kwa kushauriana na Kamishna mwenye dhamana ya Mapato kwa maana ya Kamishna wa *ZRB.*

Pia Mhe. Spika, Mhe. Hamza alizungumzia suala la uwekezaji wa *Penny Royal*. Kwa ninavyolielewa mimi Mhe. Spika, ni kwamba masuala na hoja zote za muwekezaji huyu zimeshafanyiwa kazi, na kama ulikwenda ukaona kwamba wanaendelea na kazi zao kwa maana huku upande wetu sisi hatudai. Serikali imeweka vivutio maalum kwa ajili ya miradi ambayo tunaiita uwekezaji wa kimkakati (*Strategic Investment)*. Hiyo imeshawekwa kisheria *schedule* ya kwanza ya Sheria ya *ZIPA* Nambari 11 ya 2004 *paragraph* ya nne, sasa imeweka utaratibu wa miradi mikubwa ambayo tunaiita miradi ya kimkakati. Katika kuondosha tatizo lile alilokuwa nalo *Penny Royal* na hasa masuala ya msamaha wa *laundries* ndani ya Sheria ya zamani ya *ZIPA* kipindi kilikuwa ni miezi kumi na nane. Sasa Sheria hii imeondoa *proviso* hiyo iliyokuwepo kwa ajili ya kuondoa mgongano huo kwa sababu kwenye *Strategic Investment* sasa muda ambao wamepewa ni wa miaka

mitano, na huo ndio sasa anaoweza kuutumia na Sheria hii ikipita, basi kikwazo hicho cha muda wa miezi kumi na nane kinaondoka na kwa namna hiyo hoja zake zote zitakuwa zimeshatekelezwa.(*Makofi*)

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alilirudia tena suala la kuondolewa unafuu wa ushuru kwa kweli jana mimi nililitolea maelezo ya kina sana na niliamini kwamba sote tumeelewa na nahakika nae amenielewa vizuri sana, niseme tu kwamba katika suala hili hatumkusudii mtu wala muwekezaji yeyote lakini tunakusudia kulinda viwanda vyetu nchini. Kama nilivyosema ni suala la kisera na kama suala la kisera lazima Serikali tuwe na msimamo na msimamo wa Serikali bado naurudia ni kuendelea kutoa unafuu kwa ajili ya kukuza viwanda nchini, lakini vile vile kuleta ustawi wa jamii yetu hayo ndio malengo. Hatukusudii kusema kwamba tunauondosha kabisa lakini unapunguzwa na utaendelea kupunguzwa hadi pale utakapoondolewa kabisa pale ambapo tutakuwa sisi tumeshajitosheleza katika uzalishaji uwe wa sukari ama unga wa ngano.

Kuna hoja Mhe. Hamza Hassan Juma uliizungumza ni kweli unga wa ngano unapoingizwa nchini lakini hiyo hauchajiwi ushuru ni zero, lakini huo ni kwa mujibu wa viwango vya *East Africa Community* na sisi tunafuata tu, ngano nzima inapoingia katika *Region* nzima *East Africa* haitozwi kodi, ni zero na sisi ndio tunafanya hivyo, na muwekezaji huyu tunayemzungumza wa kiwanda cha unga wa ngano kwa kweli amefanya *investment* kubwa, ameongeza uwezo wa *storage* pale kutoka tani 18,000 hadi tani 100,000. Tuna haja na haki ya kusaidia kukuza fursa wa uwekezaji katika viwanda vyetu na hili haliko kwa kiwanda kile tu lakini tunazungumzia katika kiwanda pia hichi cha Sukari.

Lakini hivi karibuni tumeondosha *Trade leavy* kwa ajili ya mali ghafi za viwandani hasa viwanda ambavyo vinazalisha maji vilivyopo hapa kwa njia ya kuvisaidia na kuweza kukuza viwanda vyetu, lakini vile vile kusaidia ajira katika nchi yetu na mchango wa viwanda hivyo uweze kuongezeka katika uchumi wetu. Sasa hivi viwanda ambavyo vinachangia *percentage wise*, tukichukua sekta nzima ya viwanda ndio asilimia 17 lakini ukichukulia viwanda vyenyewe ni asilimia 6, ni kiwango kisodo sana ambacho Serikali inabidi lazima tufanye kazi hiyo ya kuvilinda viwanda hivi, kwa sababu jana nilisema hakuna nchi ambayo inaendelea bila ya kuwekeza katika viwanda.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kulikuwa na suala jengine ambalo lilizungumzwa la vifaa na Mhe. Hamza pia alizungumzia suala la KMKM. Katika sehemu ambayo Serikali imefanya kazi kubwa katika kipindi hichi basi ni kuwezesha Kikosi chetu cha

KMKM. Fedha nyingi sana zimetumika katika kikosi, ununuzi wa boti tatu za doria lakini pia kwa mara ya mwanzo tumekuwa na boti ya kuzima moto baharini, pia boti za uokozi, kuna boti nyengine ambazo zinatarajiwa kufika hivi karibuni. Kwa hivyo tumeweza kukiongezea uwezo sana Kikosi chetu cha KMKM, lakini pia kimepatiwa vifaa vingi na vifaa vya mawasiliano wanavyo. Sasa kama kuna upungufu bado kupitia vikao ndani ya Serikali tutaangalia kama kuna tatizo hilo, lakini katika jitihada zilizofanyika katika kipindi hichi ni kuhakikisha kwamba suala hilo la vikosi vyetu na vikosi vyengine vyote vya ulinzi katika nchi yetu vimewezeshwa kikweli kweli. Naomba hilo tulikubalie na tuone kwamba jitihada ya serikali ni nzuri sana katika eneo hilo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna suala jengine ambalo Mhe. Mjumbe alilizungumza la kwamba uzuiaji wa magendo uhusishwe na uhujumu uchumi, ndicho kinachofanyika na hata Sheria hii imetoa adhabu kali kweli kweli, imetoa adhabu hata kwa wale watakaosaidia lakini pia kuna adhabu ya kutaifishwa mali, lakini vifungu pia vilivyotoka hapa katika Sheria hii ni vifungo vikali sana vya miaka saba. Lakini nakubaliana na wewe kuna haja ya kuendelea kutoa taaluma kwa wananchi kwanza kuzielewa sheria.

Jambo muhimu sana ambalo tunahitaji kulihimiza kwa wananchi wetu sote kwa pamoja ni kwamba kuwataka wananchi wetu wajifunze kutii sheria mbali mbali bila ya shuruti. Hapa pana matatizo kidogo lazima wajifunze kutii sheria za nchi. Sasa wale watakaotaka kushindana na Sheria hizo basi hatua kali zitachukuliwa na moja ya Sheria ambazo kali kwa kweli mimi nimeziona kwa sababu hata yule atakayemsaidia, kifungo chake ni miaka saba lakini atakayezuia afisa au baharia kuweza kuingia katika chombo au kufanya kazi yake naye miaka saba, ni adhabu kali na hii inatoa funzo kwa wananchi kuweza kutii sheria bila ya shuruti.(*Makofi*)

Mhe.Spika, Mhe. Rashid Makame Shamsi alizungumzia suala la *Proviso* kuliwekea *Invented comma*. Ninafikiri *comment* yake tumeichukua, ni kweli inahitaji kuwekewa. Lakini pia alizungumzia kifungu cha 25 (f) cha ukurasa wa 36, alihusisha kifungu kidogo(c) kwamba kinahusu gari na vyombo lakini vile vile kinahusisha na bidhaa na yeye akaona kwamba inajirudia katika kifungu chengine kidogo cha (d). Sasa akiisoma vizuri Mheshimiwa hiyo unaona kifungu cha (c) kinazungumzia zaidi ni gari na vyombo na zile bidhaa zitakazokuwemo kwenye ile gari na vyombo, lakini ukija huku sasa kwenye (d) ni bidhaa peke yake na bidhaa yoyote kwa hivyo hakuna *repetition* wala hakuna mgongano.

Mhe. Spika, lakini kuna suala jengine zima hili la magendo ni muhimu Waheshimiwa Wajumbe tukajua tafsiri ya magendo na isihusishwe na mtu kanunua bidhaa (*invalid*), kanunua bidhaa kwa ujumla bidhaa kubwa kasafirisha kwenye gari kama amefuata taratibu hayo sio magendo, ikiwa hakufuata taratibu sasa hayo yanaweza yakachukuliwa kwamba ni magendo au kutuhumiwa kwamba alikuwa anataka kusababisha kufanya magendo.

Mhe. Spika, Kifungu cha 22 cha Mswada wa Sheria hii kinarekebisha kifungu cha 31 cha Sheria mama kuhusiana na zawadi, na hii zawadi naomba hili niliseme pia kujibu ile hoja ya Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwamba maafsa ndio wanaopewa zile zawadi, ukitizama kifungu cha sheria hii inayofanyiwa marekebisho kwamba zawadi atapewa afisa ama mtu yeyote, si lazima askari mtu yeyote atakayefanikisha kukamatwa kwa mtu anayetuhumiwa, lakini pia na kuthibitishwa.

Kwa hivyo kama kuna watu wanageuza sasa itakuwa pia wanakwenda kinyume na sheria hii, lakini sheria ipo wazi na imeweka tafsiri vizuri sana kwamba yule atakayezawadiwa basi ni yule atakayesababisha mtu yeyote yule kutuhumiwa lakini pia kuthibitishwa kufanya kosa la magendo.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame alizungumzia suala kwamba tumetunga sheria lakini muhimu sasa kutekelezwa kwa sheria hii. Ninakubaliana na yeye na juhudi kubwa zinafanywa kuhakikisha kwamba sheria zetu zinasimamiwa kikamilifu ili madhumuni yaliyokusudiwa yaweze kupatikana.

Mhe. Spika, pia alizungumzia suala la pongezi kwa Kikosi cha KMKM kuweza kuzuia magendo hasa katika msimu uliopita wa karafuu. Pongezi hizo kama serikali tunazipokea na ninadhani hayo Mheshimiwa kwa kifupi ndio yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe na naamini nimeyatolea ufafanuzi wa kutosha.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa niwahoji wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha wanyanyue mkono, wanaokataa, nadhani waliokubali inaoneshwa wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Spika, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu.

## KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

## Mswada wa Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mapato ya 2018

## SEHEMU YA KWANZA

### Utangulizi

Kifungu cha Kwanza Jina fupi na kuanza kutumika

## SEHEMU YA PILI

### Marekebisho ya Sheria na Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba Saba ya mwaka 2009

Kifungu cha Pili Kusomwa

Kifungu cha tatu - Marekebisho ya kifungu cha tano pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha Nne - Marekebisho ya kifungu cha 18 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha Tano - Marekebisho ya Kifungu cha 29 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha Sita - Marekebisho ya Kifungu cha 31 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha Saba - Marekebisho ya Kifungu cha 31(a)

Kifungu cha Nane - Marekebisho ya Kifungu cha 57 pamoja na marekebisho yake.

### SEHEMU YA TATU

### Marekebisho ya Sheria ya Ushuri wa Stamp Namba 7 ya mwaka 2017

Kifungu cha tisa Kusomwa

Kifungu cha 10 - Marekebisho ya kifungu cha 77 pamoja na marekebisho yake.

**SEHEMU YA NNE**
**Marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi ya Zanzibar Namba 1 ya mwaka 2006**

Kifungu cha 11 Kusomwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 12 - Kuongeza kifungu kipya cha 21(a) pamoja na marekebisho yake.

**SEHEMU YA TANO**
**Marekebisho ya Sheria ya Kutoza Kodi ya Mafuta Namba 7 ya Mwaka 2001**

Kifungu cha 13 Kusomwa.
Kifungu cha 14 - Kufuta kifungu cha tano

**SEHEMU YA SITA**

**Marekebisho ya Sheria ya Ukuzaji na kulinda vitega Uchumi Zanzibar NaM. 11 ya mwaka 2004**

Kifungu cha 15 Kusomwa pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 16 - Marekebisho ya kifungu cha 19 pamoja na marekebisho yake.

**SEHEMU YA SABA**
**Marekebisho ya Sheria Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya Mwaka 2003**

Kifungu cha 17 Kusomwa.
Kifungu cha 18 - Marekebisho ya Kifungu cha Pili pamoja namarekebisho yake.
Kifungu cha 19 - Marekebisho ya Kifungu cha 4 pamoja namarekebisho yake.
Kifungu cha 20 - Kuongezwa sehemu mpya ya 2(a) pamoja namarekebisho yake.
Kifungu cha 21 - Kuongeza kifungu kipya cha 25(a) na 25(b) pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 22 - Marekebisho ya Kifungu cha 61 pamoja na marekebisho yake.

**SEHEMU YA NANE**
**Marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Biashara Zanzibar Nam. 10 ya 2017**

Kifungu cha 13 Kusomwa
Kifungu cha 24 Marekebisho ya Kifungu cha 15 Pamoja na Marekebisho Yake

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na mrekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kuwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango wanyanyue mikono, wanaokataa, nadhani inavyoonekana waliokubali wameshinda.(*Makafi*)

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wajumbe mpaka hapo Mhe. Waziri wa Fedha amekamilisha shughuli zote. *Ok* kuna hatua moja ya kusoma mara ya tatu Mhe. Waziri wa Fedha njoo ukamilishe taratibu.

**Mswada wa Sheria ya Kutozwa Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo**

*(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi:** Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kutozwa Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi, Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na hayo, usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za (SMZ):** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa hatua hiyo sasa itakuwa imebaki hatua moja tu ya Mhe. Rais nafikiri kukamilisha hii. Katibu mambo yaliyobaki.

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe tuna kama dakika 18 zimebaki na tuna ajenda moja kwenye *order paper* ni taarifa ya Serikali ya Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Sasa sijui Mhe. Waziri sijui muda huu utakutosha kwa ajili ya kuwasilisha ripoti yako. Haitoshi?

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:** Haitoshi.

**Mhe. Spika:** Haitoshi basi kama ni hivyo naomba tusitishe hizi shughuli mpaka saa 11:00 jioni ambapo Waziri wa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto atakapokuja kuwasilisha halafu tutaweza kukamilisha hayo. Kwa hivyo huu muda uliobaki. \\

Naam! kuhusu utaratibu Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamuo wa Pili wa Rais.

**UTARATIBU**

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa Wajumbe wamefanya kazi kubwa kwa kupitisha Sheria hii kwa uzuri sana na kwa kuwa shughuli iliyobaki ni Kauli ya Serikali haichukui muda mrefu, tunaomba tutengue Kanuni ili tuweze kukamilisha shughuli hii iliyombele yetu ili tuweze kumaliza shughuli hizi katika kipindi hichi cha mchana.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo nakuomba uturuhusu tuwaombe Wajumbe tutengue Kanuni ya 23(1) ili tuweze kuendelea na shughuli zetu na tuzimalize shughuli zetu za leo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa hoja imetolewa na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, …

**Mhe. Mohamed Said Mohamed:** Kuhusu Utaratibu. Mhe. Spika, nikushukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi..

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa subiri nihoji kwanza halafu nitakuruhusu. Waheshimiwa naomba niwahoji, Waheshimiwa Wajumbe , Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ametoa hoja kuhusu kutengua Kanuni ya wakati. Sasa naomba niwahoji wale wote ambao wanakubaliana na Mhe. Waziri wanyanyue mikono, watu wamenyanyua mikono miwili miwili, wanaokataa, inavyoonesha waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*

*(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)*

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) sasa.

**UTARATIBU**

**Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa):** Mhe. Spika, nilikuwa nikiomba utaratibu kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, alikiomba Kiti chako kimruhusu ili atoe hoja ile lakini bila ya wewe kumruhusu Mhe. Spika, wewe moja kwa moja umekwenda kutuhoji huku bila ya wewe kuruhusu. Sasa jambo hilo lakini ndio limeshapigiwa kura naheshimu sana maamuzi ya Baraza lako.

**Mhe. Spika:** Alitoa hoja Mheshimiwa mwisho watu wakanyanyuka kwa maana ya kumuunga mkono, kwa hivyo ndio maana nimehoji kuunga mkono kile ambacho kilikuwa kimeendelea. Katibu shughuli inayofuata.

**TAARIFA YA SERIKALI**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA HAKI ZA WATOTO KATIKA KILELE CHA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA ILIYOWASILISHWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI - ZAZIBAR**

**Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:** Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru. Lakini pia naomba niwaonyeshe wananchi kitabu ninachozungumza sasa hivi ili watakapopata nafasi waweze kukitumia. Sasa rabda nimpe mtu wa kamera aweze kukipiga picha kwa sababu kimeandikwa neno zuri linasema MATUMAINI. Watoto sasa hivi wana MATUMAINI juu ya serikali yao kwamba maisha yao yatakuwa salama na tutafuatilia. Kitabu chenyewe ni hiki kinaitwa MATUMAINI kuna picha ya watoto wawili wa kike na wakiume.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa wasaa wa kuweza kufika siku ya leo tena. Pia nipende kukushukuru wewe pekee pamoja na watendaji wako wote katika Afisi yako ambao wamefanya kazi na kutupa ushirikiano wa hali na mali katika kipindi chote ambacho tumekuwepo hapa. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wetu Dkt Ali Mohammed Shein ambae amekuwa ni kiongozi na chacho kubwa sana kwenye masuala yanayohusu watoto, wanawake na wazee katika nchi yetu kuhakikisha kwamba wanapata haki zinazostahiki.

**DIBAJI**

Taarifa ya Utekelezaji wa Haki ya Mtoto ya Zanzibar kwa mwaka 2017/2018 inatoa hali halisi ya Zanzibar inavyochukua juhudi katika kuyafanyia kazi mapendekezo na maazimio ya Jumuia za Kimataifa, Kikanda na Sera za Kitaifa kuhusu haki na Maendeleo ya watoto. Taarifa hii ni inatoa taswira kwa Sekta za Umma na Binafsi zenye jukumu la utekelezaji wa Haki na Ustawi wa Mtoto namna zilivyotekeza Mipango, Mikakati katika kufikia Ustawi na upatikanaji wa Haki za Watoto kwa mwaka huu. Ripoti hii ni miongoni mwa zana muhimu ya kufanyia kazi katika kuchambua, kutafakari na kuchukua hatua mbadala katika kulinda haki za mtoto katika maeneo ya Makuzi, Hifadhi na Maendeleo ya Mtoto. Katika maandalizi ya ripoti hii, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto imeshirikiana na taasisi za Serikali na zisizokuwa za Serikali ambazo zina jukumu la kuona kuwa watoto wanaishi vyema kama ambavyo Jumuia ya Kimataifa pamoja na Sheria na Sera ya Mtoto Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea napenda sana kwa heshima na taadhima nishukuru sana Kamati yetu ambayo imekuwa ikifanya kazi baga kwa bega chini ya uongozi wa Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) pamoja na wanakamati wote, licha ya kwamba wametangaza Baraza hili mabadiliko ya Kamati, lakini tunaamini hata akiwa mbali ataendelea kutuchangia na kutusaidia na kutushauri na wanakamati wake wote.

**SEHEMU YA KWANZA**

**UTANGULIZI**

Zanzibar ni moja kati ya nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda inayohusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Mikataba hiyo ni mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto wa mwaka 1989 (CRC) na mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto mwaka 1991 (ACRWC). Masuala ya Mtoto ni mambo yasiyokuwa ya Muungano huratibiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa takwimu Sensa ya Watu na Makaazi Tanzania ya mwaka 2012, idadi ya watu Zanzibar ni 1,303,569 kati ya hao 638, 268 sawa na asilimia 49.0 ni watoto wenye umri wa miaka 0-17. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa watoto 318,223 sawa na asilimia 47.6 ni wanaume na watoto 320,045 sawa na asilimia 50.5 ni wanawake. Kundi hili la watoto ni muhimu katika mustakabali mzima wa maendeleo ya Taifa letu na Afrika kwa Ujumla.

Kila ifikapo Tarehe 16 Juni mataifa ya Afrika huadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika. Madhumuni ya maadhimisho hayo ni kuwakumbuka watoto wa Kiafrika waliouawa kikatili huko SOWETO Afrika ya Kusini. Watoto ambao walikuwa wakiandamana kwa amani kupinga utawala wa kibaguzi uliokuwa ukiendeshwa na Makaburu ambao mfumo wake wa utoaji wa elimu uliwabagua Waafrika weusi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaungana na nchi nyengine za Afrika kuadhimisha siku hii.

Kila mwaka Umoja wa Afrika hutoa ujumbe maalum, katika maadhimisho haya, ujumbe wa mwaka huu ni **(“Hakuna Mtoto atakaeachwa nyuma katika Maendeleo ya Afrika”).**
Ujumbe huu umezingatia agenda ya Dunia Maendeleo Endelevu ‘2030’ ili kuwafikia Watoto walioachwa nyuma kimaendeleo.

## MAANA YA MTOTO

Mtoto ni mtu yeyote alie chini ya umri wa miaka 18 kwa mujibu wa Sheria ya Watoto Zanzibar namba 6 ya mwaka 2011, pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto ya mwaka 1989 (CRC). Hivyo, mtoto ni binadamu na ni sehemu ya familia na jamii, mwenye majukumu kwa ajili ya maendeleo ya baadae.

Aidha, Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 imeweka uhuru na Haki za binadamu ambapo Watoto wanafaidi Haki hizo. Haki kuu za msingi ni Haki ya Kuishi, Haki ya Kuhifadhiwa / kulindwa, Haki ya Kuendelezwa. Haki ya Kushiriki na kushirikishwa.

Hata hivyo, haki kwa mujibu wa mazingira yetu ni kama vile usawa wa watu wote, faragha, usalama wao, haki ya kujieleza, haki ya kidini, haki ya kujumuika na haki mbele ya sheria na mengineyo.

## CHIMBUKO LA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

Chimbuko la Siku hii ni kuwakumbuka Watoto wa Kiafrika (Weusi) waliouawa kikatili Mjini SOWETO, Afrika ya Kusini mwaka 1976, wakati wakipinga ubaguzi wa rangi na utumiaji wa Lugha ya Kibaguzi dhidi yao katika maskuli. Utawala wa kibaguzi wa Makaburu haukuwathamini wazalendo wa Afrika ya Kusini ambapo ulikuwa ukiwapa watu wa jamii hiyo mateso makubwa yaliyokuwa yakiwakumba pia na watoto wasiokuwa na hatia.

Kufuatia mauaji hayo, Umoja wa Nchi Huru za Afrika mwaka 1991 uliamua kuiteua na kuiadhimisha Siku ya Tarehe 16 Juni ya kila mwaka kukumbuka tukio hilo la kidhalimu walilofanyiwa Watoto wa Kiafrika. Pia, Umoja wa Afrika huitumia siku hii kuwa ni sehemu ya kuongeza uelewa wa jamii juu ya Haki na Maslahi ya Watoto.

## SEHEMU YA PILI
## UTEKELEZAJI WA HAKI ZA MTOTO KWA MWAKA 2017/2018

Sehemu hii inaelezea utekelezaji wa Haki za Watoto kwa kipindi cha 2017/18 ambapo itajikitika katika misingi mikuu minne ifuatayo:

i. Haki ya Kuishi.
ii. Haki ya Kuhifadhiwa / kulindwa.
iii. Haki ya Kuendelezwa.
iv. Haki ya Kushiriki na kushirikishwa.

### HAKI YA KUISHI

Haki hii inahusiana na mahitaji ya msingi ya mtoto yakiwemo chakula, hali nzuri ya kuishi na afya njema, pamoja na huduma ya maji safi na salama ambayo imetekelezwa kama ifuatavyo:

### a) Kulinda Afya ya Mtoto.

Wizara ya Afya ina jukumu la kulinda afya ya mtoto ili kumuwezesha kuishi salama na kumkinga dhidi ya maradhi. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, wizara imetoa elimu ya afya juu ya matumizi sahihi ya huduma ya vyoo katika skuli za msingi 132 Unguja na Pemba. Pia Wizara iliandaa na kusambaza vipeperushi 13,500 vinavyoelimisha juu ya umuhimu wa kuosha mikono kabla ya kula na baada ya kutoka chooni ili kujikinga na maradhi ya kipindupindu.

#### i. Huduma za chanjo

Ili Mtoto aweze kukua vizuri, anahitaji kupatiwa huduma za chanjo tokea akiwa tumboni na baada ya kuzaliwa hadi afikapo miaka mitano. Katika utekelezaji wa upatikanaji wa huduma hiyo, Wizara imewapatia watoto huduma ya chanjo Unguja na Pemba kama ifuatavyo;

- Asilimia 84 ya watoto walio chini ya mwaka mmoja walipatiwa chanjo ya PENTA 3 kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 78 ya mwaka 2016.

- Chanjo ya Polio ilitolewa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 15 na wagonjwa waliopata ulemavu walioko katika kundi hilo walifuatiliwa kwa karibu. Pia, Ufuatiliaji wa watoto walioasi chanjo na wale ambao hawajachanjwa nao ulifanyika.

Matokeo ya ufuatiliaji huo yalionesha kuwa wagonjwa 15 walipata ulemavu Unguja na Pemba, na imegundulika kuwa kupooza huko hakukusababishwa na maradhi ya Polio. Wizara imetoa mafunzo kwa wafanyakazi 50 juu ya kutibu ugonjwa ya kupooza.

**Ugawaji wa Matone**

Wizara ya Afya pia imetoa matone ya vitamin A na dawa za minyoo kwa watoto 202,055 walio na umri wa chini ya miaka mitano ili kuwaongezea kinga watoto dhidi ya maradhi mbali mbali. Lengo ni kuwafikia watoto 206,202 wenye umri wa miezi 6-59. Hii ni sawa

(asilimia 98). Kwa upande wa utoaji dawa za minyoo watoto 183,453 ambapo asilimia 97.9 walipatiwa dawa hizo.

Ugawaji wa matone na utoaji wa dawa za minyoo umeongezeka kutoka asilimia 78 kwa mwaka 2017 hadi asilimia 98 kwa mwaka 2018. Kinga hizi zinawakinga watoto dhidi ya magonjwa yakiwemo upungufu wa damu, kuharisha, suruwa, magonjwa ya hewa, utapiamlo na mengineyo.

**Chanjo ya Saratani ya Shingo ya Kizazi**
Wizara inaendelea kutoa chanjo ya saratani ya shingo ya kizazi kwa watoto wa kike wenye umri wa miaka 9-14. Chanjo hiyo iliyozinduliwa tarehe 10/4/2018 na Mke wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mama Mwanamwema Shein. Lengo ni kuwakinga watoto wa kike na jamii na maradhi haya.

**ii. Huduma ya Lishe**

**Utapiamlo**
Kwa mujibu wa taarifa kutoka Wizara ya Afya, watoto 1,354 wamebainika kuwa na tatizo la utapia mlo. Kiwango hicho ni sawa na asilimia kumi na mbili nukta tatu (12.3) ya watoto 166,813 waliopimwa. Kati ya hao 122 wana tatizo la Utapiamlo mkali na watoto 1,232 wana Utapiamlo wa kati. Kiwango cha utapia mlo mkali kimepungua kutoka watoto 143 kwa mwaka 2017 hadi watoto 122 mwaka 2018.

**Hali ya unyonyeshaji**
Hali ya mwitiko wa kinamama wa unyonyeshaji wa watoto wachanga wenye umri wa siku (moja) 1 hadi miezi sita (6) ni mdogo. Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2014 *'National Nutritional Survey' (NNS 2014)* asilimia 20 ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama hadi miezi sita tu. Kitu ambacho kinatisha wakina mama wengi wanakimbia jukumu la kunyonyesha watoto kwa sababu aidha ya mazingira mbali mbali ya kazi, lakini pia labda kwa ajili ya kutaka waendelee kuwa ma- *mis*

Wizara inatekeleza mikakati mbali mbali ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa unyonyeshaji, kuwatumia watoa huduma za afya wa kujitolea, pia kupitia vyombo vya habari. Pia Maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji yamefanyika kuanzia tarehe 1-7 Agosti 2017 na kauli mbiu ni `***UNYONYESHAJI NA KAZI UNAWEZEKANA***'

**Maradhi ya Kichocho**
Jumla ya wagonjwa 273 wa maradhi ya kichocho wamegunduliwa na wamepatiwa matibabu. Wengi kati ya hao ni watoto wanaocheza kwenye maji yanayotuwama. Kwa mujibu wa utafiti mwaka 2017, umeonyesha kuwa maradhi haya yamepungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2016 hadi asilimia 1.7 mwaka 2017. Hata hivyo bado yapo maeneo ambayo yanaongezeko kubwa ya maambukizi ya maradhi hayo, maeneo hayo ni Mwera, Chaani, Bandamaji, Kinyasini, Makoba kwa Unguja na Vitongoji, Kinyasini na maeneo ya Kiuyu, Minungwini Uwandani kwa Pemba.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri, kumradhi Mheshimiwa hicho kitabu chako kina kurasa 19 pamoja na kwamba tumetengua kanuni ya wakati sasa hivi ndiyo kwanza uko ukurasa wa 5 kwa maana hiyo kwa hesabu hiyo tunaweza tukenda mpaka saa 9 halafu kuna Mwenyekiti pia wa Kamati. Mimi ningependekeza tu sijui kama mnaweza mkaona kama inafaa hichi kitabu kingie kwenye *Hansard* kama kilivyo hivyo anavyokiwasilisha Mhe. Waziri halafu Mwenyekiti wa Kamati ambayo na wao kama wanaweza *briefly* sana wakatusomea ripoti yao na yenyewe pia ikaingia kwenye *Hansard* kama walivyoiyandaa halafu tunaweza tukaamua kuhusiana na jambo hili. *(Makofi)*

Sasa makofi maana yake Waheshimiwa watakuwa wameniunga mkono. Mhe. Waziri nakupa sasa uendelee.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:** Mheshimiwa nasema tu kwamba bahati nzuri kitabu hiki kimegaiwa kwa kila mtu anacho na wamepata nafasi ya kukisoma tunaamini kabisa watakipitia na watatoa michango. Nipende kusema tu napenda niwashukuru watu walioweza kuchangia katika suala hili kukamilisha kitabu chetu. Pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria ya Utumishi wa Umma Utawala Bora, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati, Kijiji cha Kulelea watoto (SOS), Bodi ya Ushauri ya Watoto wa Zanzibar *(Tanzania Youth Icon (TAYI))* na wengine wote ambao wametusaidia pamoja na UNICEF, *Save the Children*, USAID, na michango mbali mbali ambayo mingi ilitoka kwa Wawakilishi wenyewe katika kipindi chote walichokuwa wanachangia Wizara yetu.

Mhe. Spika, kwa hayo napenda na nashukuru na naomba yote yaingie kwenye *Hansard* kama ulivyosema na Mungu awabariki.

**Ugonjwa wa Malaria**

Wizara imeimarisha udhibiti wa Malaria kwa kupiga dawa majumbani kwenye wilaya zilizoonekana kuwa na matukio ya Malaria. Wilaya hizo ni Magharibi ‘A na B’, Kati, Kusini, Kaskazini A, Kaskazini ‘B’ kwa Unguja na Chake Chake, Wete na Micheweni kwa Pemba.

Jumla ya nyumba 67,971 zilipigwa dawa kati ya nyumba 63,672 zilizopangwa kupatiwa huduma hiyo. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 107 ya lengo lililokusudiwa. Upigaji wa dawa husaidia kukinga vifo vya watoto hasa walio chini ya miaka mitano.

Kwa upande wa Pemba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imetoa huduma za lishe kwa watoto 17,207 walio katika skuli za maandalizi kupitia Mabaraza ya Miji ya Mkoani, Chake Chake, Wete na Halmashauri ya Micheweni. Watoto 8,415 walipatiwa chanjo sambamba na mama wa watoto hao kupewa elimu ya mama kwa mtoto mara baada ya kujifungua.

***Jadweli namba 1: Watoto Waliopatiwa Chanjo na Lishe Kiwilaya 2017/18***

| S/N | WILAYA | WATOTO WALIO PATIWA CHANJO. | WATOTO WALIO PATIWA LISHE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mkoani | 1,493 | 2,522 | 4,015 |
| 2 | Chake Chake | 6,033 | 1,338 | 7,371 |
| 3 | Wete | 5,368 | 2,977 | 8,345 |
| 4 | Micheweni | 4,313 | 1,578 | 5,891 |
| | **Jumla** | **8,415** | **17,207** | **25,622** |

***Chanzo: Hotuba ya Bajeti: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ 2018***

**v. Matibabu Nje ya Nchi**

Watoto 271 walipelekwa nje ya nchi kwa matibabu zaidi kwa mwaka 2017. Miongoni mwao, watoto 30 walipelekwa nchini Israel kwa upasuaji wa moyo na watoto 241 walipelekwa nchini India kwa matatizo mbali mbali ya kiafya. Ongezeko hili ni kubwa kwa mara Nane nukta Saba Nne (8.74) ya wagonjwa walipelekwa Nje ya Nchi kwa mwaka 2016.

**Huduma ya Maji Safi na Salama**

Ili watoto aweze kuishi pia anahitaji maji safi na salama kwa ajili ya kulinda afya zao dhidi ya maradhi yakiwemo ya mripuko. Katika kutekeleza hilo, Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imefanikisha upatikanaji wa Maji Safi na Salama kwa mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo. Kupitia taasisi ya Ras al- khaimah visima 33 vimechimbwa Unguja na Pemba. Maeneo yaliyonufaika na mradi huo ni Mbweni ZSSF, Skuli ya Uzini, Mitakawani, Cheju–Mapopwe kwa Unguja, na Ole-Kianga, Mkanyageni-Bogoa, Kiwani, Kifundi/Matangatuwani na Mtambwe, Kusini/Mkanjuni kwa Pemba.

Kupitia mradi uliofadhiliwa na Serikali ya China Uchimbaji wa Visima na usambazaji maji Vijijini**,** ujenzi wa Matangi 3 umekamilika katika maeneo ya Kisongoni, Kiboje na Miwani. Aidha, ulazaji wa mabomba kwa masafa ya kilomita 20.178 umekamilika. Hatua iliyobaki ni kuunganisha mabomba katika nyumba za wananchi. Upatikanaji huu wa maji safi na salama, umesaidia kuimarisha afya za watoto na kupunguza maradhi ya mripuko.

ZAWA kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeimarisha Miundombinu ya Maji, Kujenga na kuvifanyia ukarabati vyoo katika Skuli 23 za Mkoa wa Mjini Magharibi. Utekelezaji huu umeimarisha huduma za usafi na huduma za vyoo kwa watoto wanaosoma katika Skuli hizo, hivyo kuendelea na masomo yao kwa ufanisi.

ZAWA inasambaza maji Safi na Salama kwa kutumia magari maalum katika kuimarisha upatikanaji wa huduma hiyo kwenye maeneo yenye upungufu hasa kwa kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Utaratibu huu unaipunguzia familia usumbufu wa kutafuta maji na kutumia muda huo katika uzalishaji mali watoto wanapata muda mzuri wa kupata haki nyengine za msingi kama vile kushughulikia masomo yao na kucheza.

Kupitia msaada wa Shirika la Kimataifa la kuwahudumia Watoto (UNICEF) mradi wa usambazaji maji safi na salama katika eneo la Tomondo Wilaya ya Magharibi ‘B’ unakamilisha ufungaji wa pampu kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi.

**HAKI YA KUENDELEZWA**

Haki hii inajumuisha kumuendeleza mtoto kielimu na maadili mema. Utekelezaji wa Haki hii inajumisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Kazi Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto.

**Elimu ya Mandalizi**

Katika kumpatia mtoto haki ya elimu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora zimesimamia Madrasa, Vyuo vya Kur-ani na skuli za maandalizi/vituo 324 kwa mwaka 2017/18. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wanapata elimu ya dini, maandalizi na msingi mapema wakiwa na umri kati ya miaka minne na kumi na nne.

**Uandikishaji wa Wanafunzi**

Jumla ya watoto 72,151 (69.4%) (wanawake 36,648: wanaume 35,503) wameandikishwa kujiunga katika skuli za maandalizi mwaka 2018/2019, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 66.1 ya uandikishaji wa mwaka 2017/2018. Aidha, watoto 49,442 (58.8%) waliopata elimu ya maandalizi ambao ni sawa na asilimia wameanadikishwa kuanza darasa la kwaza katika mwaka 2018.

**Vifaa vya Kujifunzia**

Wizara ya Elimu pia, imetoa madaftari 737,000, chaki, madaftari ya mahudhurio, madawati na viti. Huduma hizo zimetolewa katika Skuli za Chutama, Ndijani, Sharifumsa na Kiombamvua.

**Huduma za Maktaba**

Wizara imeendelea kukuza uelewa na utamaduni wa kusoma kwa watoto kwa kipindi cha mwaka 2017/18 kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha huduma za Maktaba ya watoto, ambapo Maktaba zimefanyiwa matengezo makubwa yakiwemo kupaka rangi, kuchora picha ukutani, kuweka mazulia, mito, rafu za kuwekea vitabu, pamoja na kuweka viti, meza, vifaa vya kuchezea watoto. Kunakili vitabu vipya katika 'CD' kwa ajili ya kutumika kwa njia ya Televisheni ili kuwavutia watoto na watumiaji wengine wa Maktaba. Hadi sasa watoto 12,353 wanapata huduma za Maktaba kwa uhakika Unguja na Pemba. Jumla ya vitabu 29,470 vilivyopatikana kwa njia ya msaada kutoka Shirika la "*Book Aid*" la Uingereza vimegaiwa katika Taasisi 142 za elimu, zikiwemo skuli za msingi 89, skuli za Sekondari 49. Jumla ya vitabu 6,829 vimegawanywa katika skuli 142 zilizomo katika Mikoa yote ya Zanzibar.

ii. Aidha, vitabu 572 viligawanywa kwenye Vyuo Vikuu vikiwemo Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Kumbukumbu ya Abdulrahman Al Sumeit cha Chukwani. Vitabu vimegawanywa kwa vituo vikiwemo Kituo cha Walimu cha Dunga na Kituo cha Walimu cha Taifa Beit el Ras.

iii. Jumla ya Programu 52 za watoto zikiwemo 28 za ndani na 24 za nje juu ya Maktaba ziliandaliwa ambapo watoto 2,914 wameshiriki katika programu hizo Unguja na Pemba.

iv. Wizara imeadhimisha Siku ya Kimataifa ya kusoma na kuandika (*International Literacy Day*) katika eneo la Skuli ya Mahonda Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, ambapo jumla ya watu 655 walishiriki wakiwemo wanafunzi 550.

Ufanikishaji na utekelezaji wa haki hizo umeweza kutoa tathmini ya kuridhisha inayoonesha jinsi Serikali ilivyotoa kipaumbele ili kumjenga mtoto kielimu, maadili mema, tabia, kisaikolojia na kuwa raia mwema kwa siku za baadae.

**HAKI YA KUHIFADHIWA /KULINDWA**

Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ukiukwaji wa haki zake za msingi kama vile kutelekezwa, kubakwa, kukoseshwa huduma bora za msingi na kutumikishwa.

**Hifadhi ya Mtoto**

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto imefuatilia kesi za watoto 129 zilizoripotiwa katika Mahkama za Watoto za Vuga na Mahonda kwa Unguja na Kaskazini na Kusini kwa Pemba. Kati ya kesi hizo, kesi (45 zimepatiwa hukumu, 8 zimefutwa na 76 zinaendelea).

Wizara imetoa elimu kwa Timu 11 za viongozi wa dini 88 (55 Unguja na 33 Pemba). Lengo ni kuwajengea uwezo wa kumkinga mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa mujibu wa imani za dini zao. Timu hizo zimewafikia na kuwapa elimu wazazi 31,151 (Unguja: 22,873; Pemba: 8,279).

Serikali inawatunza Watoto 44 (Wanawake 22: Wanaume 22) katika nyumba ya kulea watoto Mazizini na kupatiwa huduma za msingi kama vile elimu, huduma za afya, malezi, mavazi na chakula.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto inasimamia uendeshaji wa Vituo vya Kulea Watoto Yatima 7 (Unguja 6; Pemba 1). Hadi mwezi Aprili, jumla ya watoto 444 (Wanaume 360; Wanawake 84) wanalelewa katika vituo hivyo Unguja na Pemba. Idadi hiyo imepungua ukilinganisha na mwaka 2016/2017 ambapo watoto 481 (wanaume 393 na wanawake 88) walikuwa wakilelewa katika vituo 9 (7 Unguja na 2 Pemba). Upungufu huo unatokana na kufungwa kwa kituo kimoja kutokana na kukosa vigezo vya sheria vya uendeshaji wa kituo.

***Jadweli namba: 2 Watoto Wanaotunzwa Katika Vituo Mbalimbali Unguja na Pemba 2017/18***

| S/N | JINA LA KITUO | IDADI YA WANAUME | IDADI YA WANAWAKE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SOS | 136 | 46 | 182 |
| 2 | ISLAH ORPHANAGE CENTER | 12 | 4 | 16 |
| 3 | AFRICA MUSLIM AGENCY (U) | 48 | 0 | 48 |
| 4 | AFRICA MUSLIM AGENCY (P) | 118 | 0 | 118 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | MONTESSORI ORPHANAGE | 9 | 6 | 15 |
| 6 | ISTIQAMA ORPHANAGE (P) | 8 | 0 | 8 |
| 7 | MAZIZINI ORPHANAGE HOME | 20 | 21 | 41 |
| 8 | MARKAZ FYSABILLILLAH FUONI | 9 | 7 | 15 |
| | **JUMLA** | **360** | **84** | **444** |

***Chanzo: Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii 2018***

**Makosa yanayofanywa na Watoto**

Chuo cha Mafunzo kimepokea wanafunzi 19 (18 wanaume na 1 mwanamke) ambao walitiwa hatiani kwa kutenda makosa ili waweze kurekebishwa kwa ajili ya kulinda haki zao. Aidha, watoto 34 kati yao (33 Wanaume na 1 mwanamke) wamewekwa rumande kwa ajili ya kusubiri kesi zao. Katika kuhakikisha kuwa haki za mtoto zinalindwa Chuo hicho kimefanya yafuatayo:-

a. Kimeanzisha mradi wa elimu Vyuo vya Mafunzo ambapo watoto hao wanapatiwa mafunzo maalum.

b. Kimetoa mafunzo maalumu kwa maofisa juu ya ulinzi wa watoto katika Vyuo vya Mafunzo.

c. Kimeandaa muongozo wa kushughulikia madai ya udhalilishaji ndani ya vyuo vya mafunzo.

d. Mafunzo maalum ya ‘Mandela Rules’ yametolewa yenye lengo la kuongeza ujuzi wa watendaji wa vyuo vya Mafunzo katika kusimamia haki na maslahi na ustawi wa wanafunzi na mahabusu.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto imezindua na kutekeleza Mpango Kazi wa miaka mitano (2017-2020) wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto mwezi Agosti 2017. Utekelezaji wa Mpango huo unalenga kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa Wanawake na Watoto nchini. Aidha, Operesheni Maalum ya uendeshaji wa kesi za udhalilishaji imeanzishwa na imeondosha dhamana kwa kesi zote za udhalilishaji. Jamii imeongeza mwamko wa kuripoti matukio ya udhalilishaji yanapotokea katika maeneo yao na kuchukuliwa hatua.

Kituo cha Kurekebisha Tabia za Watoto wanaokinzana na Sheria kimeimarishwa, ambapo watoto 42 (Wanawake: 3; Wanaume: 39) wamepata ushauri nasaha na kuweza kurekebisha tabia zao, na mmoja (1) amerudia tabia zake za awali. Vijana hao wamepatiwa mafunzo ya Kompyuta, lugha ya Kiingereza, ushauri nasaha na elimu ya stadi za maisha.

**Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu**

Katika kuendeleza Programu ya Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Magumu Zaidi (MVC) kwa kushirikiana na Kijiji cha watoto cha SOS Zanzibar kimefanywa utambuzi wa Watoto katika Shehia nne (4) Kisiwa cha Tumbatu na jumla ya watoto 522 walisajiliwa. Baada ya kusajiliwa, Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii huwaunganisha na fusra katika maeneo ambayo jumuia za kiraia, kiserikali ama watu binafsi huweza kuwasaidia kulingana na mahitaji yao.

**Jadweli namba: 3** ***Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu Zaidi***

| **Shehia** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Uvivini | 55 | 45 | **100** |
| Jongowe | 98 | 105 | **203** |
| Mtakuja | 57 | 58 | **115** |
| Gomani | 49 | 55 | **104** |
| **Jumla** | **259** | **263** | **522** |

**Chanzo: Idara ya Wazee na Ustawi wa Jamii 2018**

Wizara imeongeza posho kutoka shilingi 20,000/ hadi shilingi 30,000/- kwa mwezi kwa familia 159 (Unguja 98; Pemba 61) zinazoishi katika mazingira magumu, pia inazipatia maziwa familia 11 (Unguja 4; Pemba 7) zenye watoto mapacha zaidi ya wawili.

Wizara imepokea na kufuatilia matukio 406 (Unguja 233; Pemba 173) ya ukatili na uvunjwaji wa haki za mtoto. Kati ya hayo, matukio 138 yalihusu madai ya huduma na matunzo, 95 mvutano wa malezi kwa Unguja. Aidha, matukio 87 yalihusu madai ya huduma za matunzo na mvutano wa malezi 87 kwa Pemba.

Kutokana na hali hiyo watoto 334 kati ya 406 (Unguja 186; Pemba 148) wameathirika na migogoro na mivutano hiyo. Kati ya hao wanaume 112 kwa Unguja na 75 kwa Pemba. Aidha, mivutano ya malezi imewaathiri watoto 147 wa kike (Unguja 74; Pemba 73).

**Ugawaji wa Visaidizi kwa Watu Wenye Ulemavu**

Kupitia Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Idara ya Watu wenye Ulemavu ilitoa visaidizi kwa watoto 82 (Wanawake: 34; Wanaume: 48) wenye ulemavu Katika Mikoa yote ya Zanzibar. Watoto hao wana umri kuanzia miaka miwili (2) hadi 17. Visaidizi hivyo vimeongeza ufanisi wa watoto wenye ulemavu katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku, ikiwemo kwenda skuli, kushiriki michezo na kuimarisha ushiriki wao na usawa kama wenzao.

**Uendeshaji wa Kesi za Watoto**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) imepitia na kurekebisha Sheria ya Adhabu Nam 6/2004 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai 7/2004. Sheria hizo zimetiwa saini Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein mnamo mwezi Machi 2018 na zimeanza kutumika. Sheria hizo mbili mbali ya kuweka vyema masuala ya mwenendo wa makosa ya jinai lakini pia imezingatia masuala yanayohusu udhalilishaji wa wanawake na watoto ili kulinda haki zao. Ofisi inaendelea kuwajengea uwezo waendesha Mashtaka ili wawe na ujuzi wa jinsi ya kuendesha kesi zinazohusu udhalilishaji wa watoto.

Ofisi ya DPP inaendelea kusimamia mashtaka katika ngazi ya Mahkama Kuu, Mahkama za Mikoa, Mahkama za Wilaya na Mahkama za Watoto kwa kesi za udhalilishaji ambapo kwa sasa Ofisi inaendelea na kesi kwa awamu, hadi kufikia mwezi wa Mei 2018 awamu nne zimefikiwa.

*Jadweli Namba: 4. Kesi zilizofunguliwa Mahkama za Watoto: Julai – Disemba 2017*

| SN | MAHKAMA YA WATOTO | KESI ZILIZOFUNGULIWA | | KESI ZILIZOTOLEWA HUKUMU |
|---|---|---|---|---|
| | | Julai–Septemba 2017 | Oktoba–Disemba 2017 | |
| 1 | Vuga | 14 | 0 | 5 |
| 2 | Mahonda | 5 | 0 | 5 |
| 3 | Mikoa | 29 | 0 | 11 |
| | **Jumla** | **48** | **0** | **21** |

**Chanzo: DPP 2018**

Idadi ya kesi zilizofunguliwa kwa kipindi cha Julai - Disemba 2017 ni 48, kati ya hizo kesi 21 zimetolewa hukumu. Kwa kipindi cha Januari - Mei 2018, kesi 121 zilifunguliwa na kesi 9 zilitolewa hukumu.

*Jadweli Namba: 5. Kesi zilizofunguliwa Mahkama za Watoto: Januari – Mei 2018*

| SN | Mahkama ya Watoto | Kesi zilizofunguliwa | | Kesi zilizotolewa Hukumu |
|---|---|---|---|---|
| | | Januari–Machi 2018 | Aprili–Mei 2018 | |
| 1 | Vuga | 14 | 05 | 5 |
| 2 | Mahonda | 3 | 0 | 2 |
| 3 | Mikoa | 79 | 20 | 2 |
| | **Jumla** | **96** | **25** | **9** |

**Chanzo: DPP 2018**

**Kitengo cha Kupambana na Ajira za Watoto**

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kupitia Kamisheni ya Kazi Kitengo cha Kupambana na Ajira za Watoto, kimezikagua skuli 10 katika Wilaya tatu za Unguja na kugundua kuwa watoto 521 waliokuwepo katika ajira ya watoto wanaendelea na masomo. Idadi hiyo ni kati ya watoto 5,065 waliotolewa katika ajira ya watoto awali ambao wamerudishwa skuli.

*Jadweli namba: 6 Watoto Waliotolewa katika Ajira za Watoto 2017/18*

| SN | WILAYA | IDADI YA SKULI ZILIZOFIKIWA | WATOTO WALIOTOLEWA KATIKA AJIRA YA WATOTO. | WANAOENDELEA KATIKA MASOMO YA SEKONDARI | WALIOMALIZA | WALIOTOROKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kaskazini ‘A’ | 4 | 207 | 63 | 144 | 10 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Kati | 3 | 69 | 22 | 42 | 13 |
| 3 | Kusini | 3 | 245 | 83 | 143 | 10 |
| | **Jumla** | **10** | **521** | **168** | **329** | **33** |

***Chanzo: Kamisheni ya Kazi, Kitengo cha Ajira ya Watoto 2018.***

Jumla ya watoto 329 (63%) wamefanikiwa kumaliza masomo ya Sekondari, watoto 168 (32%) wanaendelea na masomo yao na watoto 33 (6.3%) walitoroka. Wizara inaendelea kuwafuatilia watoto 168 waliotolewa katika ajira za watoto ambao wanaendelea na masomo.

Aidha Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya ajira za watoto kwa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari. Jumla ya vipindi kumi (10) vimeandaliwa na kurushwa hewani, ambapo vipindi sita (6) vilirushwa kupitia ZBC TV na vipindi vinne (4) kupitia ZBC Redio.

Taasisi 24 zimepatiwa elimu kuhusiana na athari za ajira za watoto na jinsi ya kuzuia ajira hizo katika taasisi zao kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005. Matokeo yanaonesha kuongezeka mwamko wa jamii katika kuwaendeleza watoto kielimu, hivyo imepelekea kupunguza wimbi la watoto kujiingiza katika ajira hizo.

## HAKI YA KUSHIRIKI NA KUSHIRIKISHWA

Haki hii inahusiana na kuwapa watoto fursa na uhuru wa kutoa maoni yao kujiunga na kuunda vikundi vyao vyenye maadili mema ili kuelimishana na kupata taaluma zinazowahusu. Katika kutekeleza haki hizi Wizara kupitia mabaraza ya watoto imetekeleza yafyatayo:-

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto imetoa mafunzo juu ya Haki na Wajibu wa mtoto kwa washiriki 220 (Wanawake 110; Wanaume 110). Mafunzo hayo yalifanyika katika Wilaya zote 11 za Zanzibar na yaliwajumuisha watoto walio kwenye mazingira magumu na wenye mahitaji maalumu.

Wizara imewajengea watoto juu ya kutambua Mikataba ya Kimataifa juu ya Haki za Mtoto. Washiriki 100 wakiwemo watoto na wazazi wao (Wanaume: 50 Wanawake: 50) kutoka Wilaya nne za Pemba. Kwa Unguja washiriki walikuwa 123 (Wanawake; 63; Wanaume:60).

Mabaraza ya Watoto 67 (Unguja: 25; Pemba: 42) yameimairishwa kwa kujengewa uwezo wa kiutendaji juu ya shughuli za mabaraza. Watoto 574 (Wanawake: 350; Wanaume: 224) Unguja na Pemba wameelimishwa juu ya kujikinga na vitendo vya udhalilishaji na kujitambua. Nakala 3,500 za ‘Mimi Salama Na Wewe Salama’ zimesambazwa.
Vipindi 12 vimeandaliwa kwa kuwashirikisha watoto wenyewe na kurushwa kupitia Swahiba Fm, Zenji Fm, Chuchu Fm, ZBC Redio, na Online KTV. Vipindi hivyo vilihusu haki, wajibu wa watoto, Ushiriki katika Mabaraza ya watoto, Njia za kujikinga na udhalilishaji na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imegawa vifaa vya michezo katika skuli3 za Sekondari kwa lengo la kumkuza mtoto kiakili, kimwili na kisaikolojia ili waweze kuepukana na maradhi nyemelezi na kujiepusha na vishawishi visivyofaa. Vifaa hivyo ni pamoja na “Track Suit” 300, Koni 90, Televison mbili, Kompyuta Mpakato mbili, Projector mbili, DVD mbili. Pia Redio 10

zimegawiwa katika skuli 8 za sekondari zenye kufundishwa somo la michezo. Skuli hizo ni Mwanakwerekwe ‘A’, na ‘C’, Haile Selasie, Hamamni, Mwembeladu, Jambiani, Ndijani na Mkwajuni.

Aidha, idadi ya kopi 112 za Vitabu Visaidizi vya Kufundishia somo la Michezo nazo zimetolewa ili kuziwezesha Skuli zinazohusika kufundishia.

Baraza la Sanaa Sensa ya Filamu na Utamaduni kwa kushirikiana na Idara ya Michezo na Utamaduni ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imefanikiwa kuandaa mafunzo ya uibuaji na uendelezaji wa vipaji ambayo yametolewa kwa walimu wakuu wanaofundisha somo la utamaduni na sanaa katika skuli teule za msingi kwa Unguja na Pemba.

## SEHEMU YA TATU

### CHANGAMOTO

Katika kusimamia utekelezaji wa Haki ya Mtoto, kumejitokeza changamoto mbali mbali katika kila sekta iliyohusika. Changamoto za msingi zinahusu maeneo yafuatayo:

i. Kuwepo kwa mivutano ya kifamilia kati ya wazee wawili (baba na mama) kunachangia kuathirika kwa watoto wa familia hizo. Miongoni mwa athari wanazozipata ni kudhalilishwa, kukosa elimu na kujiingiza katika ajira za watoto.

ii. Baadhi ya watoto hufanya makosa katika umri mdogo na kusababisha kufungwa katika Vyuo vya Mafunzo.

iii. Watoto kukaa muda mrefu rumande wakati wa kusubiri hukumu ya kesi zao.

iv. Kuwepo watoto wanaotunzwa katika Vyuo vya Mafunzo kinyume na Sheria ya Watoto namba 6 ya mwaka 2011.

v. Kutokuwepo jengo maalum la kuhifadhia watoto wakiwa rumande/Chuo cha Mafunzo.

vi. Kutokuwepo kwa nyumba salama ya kuwatunza watoto wenye matatizo ya kifamilia na kisheria.

vii. Ufinyu wa bajeti ya kugharamia mahitaji halisi ya usimamizi wa Haki za Watoto kwa mamlaka zinazohusika.

### MAPENDEKEZO

Katika kuimarisha utekelezaji wa Haki za Mtoto, ripoti hii inapendekeza mambo yafuatayo:

i. Kuongeza uelewa wa familia na jamii juu malezi na matunzo bora ya watoto pamoja na kuwashirikisha wadau wengi zaidi katika juhudi za kutambua na kusimamia Haki za Mtoto.

ii. Kuimarisha mfumo wa haki jinai kwa watoto wanaokinzana na sheria ili kurahisisha utoaji wa maamuzi kwa wakati.

iii. Viongozi katika ngazi zote watilie maanani umuhimu wa Mabaraza ya Watoto na Kamati za Malezi za Shehia ili ziweze kusimamia malezi bora ya watoto katika jamii ndani ya Shehia zao.

iv. Kuwepo na usimamizi na utekelezaji bora wa Sheria mpya za Adhabu na Mwenendo wa Kesi za jinai pamoja na Sheria nyenginezo zinazomlinda mtoto.

v. Kuongezwa kwa kiwango cha Bajeti kwa taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali zinazohusiana na usimamizi na utekelezaji wa Haki za Watoto.

**HITIMISHO**

Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, yanatoa fursa muhimu kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, kutafakari hatua mbali mbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa maazimio yaliyowekwa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada zake za makusudi amefanikisha utekelezaji wa majukumu ya msingi katika kulinda Haki na Ustawi wa Mtoto. Ushiriki na uwajibikaji wa taasisi za ndani na washirika wa Maendeleo zimechangia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na utekelezaji wa mwaka 2016/17.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji naomba sasa nimwite Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi lakini na yeye mwenyewe ripoti yake iingie kwenye *Hansard*.

**Mhe, Ali Suleiman Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma maoni ya Kamati kama ifuatavyo.

Mhe. Spika**,** kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema, tukaweza kukutana tena leo hii ikiwa tuko ukingoni mwa Mkutano huu wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii, ili kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusiana na Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Mtoto Zanzibar kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Spika**,** Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inatoa pongezi za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa juhudi kubwa za kuyafanyia kazi mapendekezo na maazimio ya Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na Sera za kitaifa kuhusiana na Maendeleo ya watoto hapa nchini.

Aidha Kamati inatoa pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohammed Shein kwa kusimamia vizuri sekta za Umma, na Binafsi zenye jukumu la utekelezaji wa Haki na Ustawi wa mtoto na hatimae kupatikana kwa haki hizo za watoto hapa nchini.

Mhe. Spika**,** Hotuba ya Mhe. Waziri punde imemalizika imeeleza mambo yote na tunayathamini maelekezo hayo na kwa kuwa Waheshimiwa Wajumbe wote wamepata kitabu watapitia na

watasoma litakalotubidi tulifanyie kazi katika maeneo yetu ya majimbo yetu kwa kuwaelimisha wananchi.

Mhe. Spika, inaonyesha kwamba, Serikali kwa kutambua thamani, utu na umuhimu wa mtoto hapa nchini, kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 imejidhatiti katika kusimamia misingi mikuu ya haki za mtoto ambazo ni kuishi, kuhifadhiwa (kulindwa), kuendelezwa na kushirikishwa. Kamati imeridhika na juhudi hizi na kuomba serikali kujidhatiti na kuhakikisha juhudi hizo zinaendelezwa.

Mhe. Spika**,** Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Mtoto mwaka huu, pamoja na kueleza mafanikio makubwa katika kutekeleza haki ya Mtoto ya Kuishi, bado mkazo zaidi unahitajika katika kulinda afya ya mtoto hasa katika ungojwa wa Utapia Mlo.

Mhe. Spika**,** ingawa kiwango cha utapia Mlo mkali kimepungua kutoka watoto 143 kwa mwaka 2017 hadi watoto 122 mwaka 2018 , bado Kamati yangu inashauri kuongezwa mikakati zaidi ili hatimae kulitokomeza kabisa tatizo hilo hapa nchini.

Mhe. Spika**,** Kamati yangu imeshtushwa na taarifa ya utafiti unaoonyesha kwamba, mwitikio wa akinamama wa unyonyeshaji wa watoto wachanga wenye umri wa siku moja hadi miezi sita kuwa ni mdogo. Kamati inasikitishwa na taarifa hii na kuwaomba watendaji wote wanaohusika masuala ya kuwalinda watoto kiafya pamoja na jamii kwa ujumla kutilia umuhimu suala la Unyonyeshaji, kwani kamati inaamini kwamba suala hili lina manufaa mengi kwa mama na mtoto.

Mhe. Spika**,** Aidha Kamati ina tarifa kwamba Maziwa ya mama ni lishe kuu iliyo bora kwa watoto, kwa kuwa humpa virutubisho vyote kwa kiasi na ulinganisho sahihi kwa maendeleo na ukuaji wa kawaida hadi kufikia miezi sita, Kulinganisha na maziwa mengine.
Pia Kamati inashauri Maadhimisho ya wiki ya unyonyeshaji yahamasishwe na kupewa nguvu zaidi ikiwa ni njia moja wapo ya kuongeza taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa unyonyeshaji wa maziwa la mama.

Mhe. Spika**,** Kamati yangu pia imeridhika na juhudi za Serikali za kuokoa maisha ya watoto wetu hasa wale wanaoshindikana kutibiwa hapa nchini, Ingawa kamati haipendelei watoto wetu kuongezeka kuugua, lakini inapongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa kuokoa na kupeleka watoto wengi zaidi kupatiwa huduma muwafaka zaidi za kiafya nje ya nchi kwa mwaka huu.

Mhe. Spika**,** Kamati yangu pia imeridhika na Utekelezaji wa kumuendeleza mtoto kielimu na kimaadili. Mafanikio ya kuandikisha watoto 49,443 kuaza darasa la kwanza mwaka 2018 ni hatua nzuri kabisa hapa nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba hatua hii iende sambamba na uboreshaji wa majengo yetu ya skuli, ubora wa elimu inayotolewa na kiwango kizuri cha wanaomaliza na kufaulu vyema masomo yao. Kamati pia inatoa pongeza kwa Serikali kupitia Wizara husika kwa kukuza uelewa na utamaduni wa kusoma kwa watoto wetu.

Mhe. Spika**,** Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inaendelea kusononeshwa na Utekelezaji wa hifadhi na kumlinda mtoto dhidi ya ukiukwaji wa haki zake za msingi. Kamati inasikitishwa na mwendelezo wa Kesi za udhalilishaji wa watoto na kesi za matunzo ya watoto mambo yanayopelekea kuwakosesha huduma za msingi kama vile elimu, huduma za afya, malezi, mavazi na chakula.

Mhe. Spika**,** kuhusiana na makosa yanayofanywa na watoto tunaishauri Wizara na serikali kwa ujumla kuwafuatilia na kuwapa ushauri zaidi watoto wanaokinzana na sheria na hatimae wawe watoto wema wenye kujiepusha kabisa na vitendo hivyo.

Mhe. Spika**,** Kamati hainabudi kuipongeza Serikali kupitia Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa kutoa visaidizi kwa watoto 82 ambao wana mahitaji maalum ambavyo vimeweza kuwaongezea ufanisi katika maisha yao. Hatua hii ya serikali ni nzuri na inafaa kupongezwa na kila mwenye uchungu na watoto wetu hawa wenye mahitaji maalum.

Mhe. Spika**,** vile vile, suala la Ajira za Watoto bado linahitaji nguvu za makundi yote, pamoja na kwamba tumeripotiwa kwamba vijana 521 waliokuweko katika ajira ya watoto wameokolewa na ajira hiyo bado kunaatarifa ya kuendelea na kazi hiyo katika baadhi ya maeneo hivyo bado tatizo hilo zilidi kufuatiliwa na kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Spika**,** Kamati ya maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inapendendekeza na kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu changamoto zilizotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee , Maendeleo ya Wanawake na Watoto kuhusiana na utekelezaji wa Haki za mtoto pamoja na kukubaliana na mapendekezo yote aliyoyaeleza.

Mhe. Spika**,** Kabla sijamaliza kusoma Maoni ya kamati , kuhusiana na Ripoti hii, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa walioonyesha wakati wa kupitia Ripoti hii. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue kwa majina kama iifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Ali Suleiman Ali (SHIHATA) | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Maryam Thani Juma | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mussa Foum Mussa | Mjumbe |
| *7.* | Ndugu Himid Haji Choko | Katibu |
| *8.* | Ndugu Mussa Issa Mussa | Katibu |
| *9.* | Ndugu Amina Abeid Hemedi | Mkalimani |

Aidha Mhe. Spika**,** naomba kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati , Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Salha Mohammed Mwinjuma Mwakilishi wa Viti Maalum vijana (Mkoa wa Kusini Unguja) pamoja na Wajumbe na Makatibu wote wa Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyonipa kwa muda wote wa Kamati hii. Mashirikiano yao makubwa yameniwezesha kuiongoza Kamati hii kiurahisi kwa muda wote.

Mhe. Spika**,** pia napenda kumpongeza sana Mkalimani wa alama Ndugu Amina Abeid Hemed, kwa kazi kubwa aliyoifanya na hatimae kuwawezesha wajumbe wote wa kamati kufuatilia mwenendo wa kamati yetu. Pia nawashukuru Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara zinasosimamiwa na Kamati hii kwa ushirikiano wao na kuomba mashirikiano hayo yaendelezwe kwa Kamati mpya kama itakayoundwa na Mhe. Spika ambaye ameshaiunda.

Mwisho niseme tu Mhe. Spika, nawapongeza Wajumbe wangu wote nayapongeza Mawizara matatu, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Vijana, Wazee, na Watoto, dooh! Samahani, vijana hawamo, Wizara ya Kazi na Uwezeshaji, Watoto, Wanawake na Wazee, inatosha hivyo hivyo. Lakini pia Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Vizara ya Vijana, Maendeleo ya Michezo na mengineyo hawa wote nawapongeza.

Lamwisho niseme Mhe. Spika, nawambia Mawaziri wote, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna, tumeshirikiana kwa miaka miwili na nusu kwa moyo safi kabisa, na naweza kuthubutu kusema kwamba nawapongeza Wajumbe wenzangu hatukukwaruzana, tumekwenda vyema, tumefikia hapa tulipo na nawatakia kazi njema na mimi nikiwa mmoja wapo. Tunapokwenda tukafanye kazi kuliko tulikotoka kwa sababu wajibu wetu kuisaidia serikali yetu kuhakikisha kwamba haya tunayoyazungumza na tunayoyafatilia kwa maslahi ya jamii na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya hayo Mheshimiwa niseme kwa mara nyengine tena nakushukuru kwa kunipa fursa hii kusimamia katika Baraza lako tukufu kusoma maoni ya Kamati kuhusiana na taarifa ya utekelezaji haki za Mtoto Zanzibar kwa mwaka 2017/18. Pia nawashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) Waheshimiwa ripoti imewasilisha na Waheshimiwa ripoti imewasilishwa na Mhe. Waziri na tumesikia pia maoni ya Kamati lakini hakuna mtu ambeye ameomba kuichangia. Kwa hivyo naomba nichukue nafasi hii sasa kuhoji tu kama mmeipokea hii ripoti. Wale wote wanaounga mkono hii ripoti waliyoipokea wanyanyue mikono, wanaokataa, inaonyesha waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*
*(Hoja imaamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa baada ya shughuli hizo kwenye *order paper* itakuwa hakuna shughuli kwa maana ya kwamba hatutoweza tena kuja jioni, lakini kabla ya sijakhirisha naomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Maadhili kuwa wasubiri kwenye makochi hapo juu watakapomaliza chaguzi za Kamati zao nyengine ili Kamati hiyo iweze kufanya uchaguzi wake pia. Hili ni ombi kutoka kwa Katibu wa Kamati hiyo.

Baada ya tangazo hili sasa naomba niakhirishe shughuli za Baraza mpaka kesho saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 7:07mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 28/06/2018 saa 3:00 za asubuhi)*